SUPA JACKPOT
TZS. 1,099,164,188
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Serikali** yasema ugonjwa Marburg haupo tena nchini

UKURASA 4


HOTUBA
Ijumaa Aprili 7, 2023 Nipashe 11
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA SERIKALI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2023/2024

UKURASA 11

Nipashe
Ijumaa Aprili 7, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581273
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

## RIPOTI YA CAG

# Nchi inatafunwa

UKURASA 2



**Vyura Kihansi watunzwa kwa bil. 6/- Marekani**

**Wadaiwa hewa bil. 21/- TTCL**



**Hasara Bil. 204/- NHIF**



**Bil. 20/- Boeing mbili kutotumika**



CAG Charles Kichere



**Wahamiaji haramu watafuna bil. 3.7/- magerezani**



**Mikopo mil. 896/- vikundi hewa 48**



**Matumizi ndege bil. 70/- mapato bilioni 45/-**

## Uwekezaji MSD waleta neema kwa wagonjwa wa figo

UKURASA 4

## ... Wabunge wataka utekelezaji maagizo aliyotoa Rais Samia

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA, YANGA NA MECHI ZA KIUMENI UK.24
**MAONI** UK.6




Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere (katikati) akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana. Kulia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Halima Mdee na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mashirika ya Umma (PAC), Naghenjwa Kaboyoka. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CAG aanika nchi inavyotafunwa

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

NCHI inatafunwa! Ndicho unachoweza kusema kutokana na matumizi mabaya ya fedha za umma na harufu ya ufisadi iliyoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kupitia ripoti yake ya mwaka 2021/22.

Katika ripoti hiyo iliyowasilishwa bungeni jana asubuhi na baadaye CAG Charles Kichere kutoa mukhtasari wake kwa waandishi wa habari, kuna mambo mbalimbali yanayoashiria matumizi mabaya ya fedha za umma.

Miongoni mwake, ni matumizi ya mabilioni ya shilingi ya kugharamia matunzo ya vyura wa Kihansi huko Marekani; Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), kulipa posho za wafanyakazi Sh. milioni 38.72 zaidi ya viwango vilivyoidhinishwa katika mwongozo; vikundi hewa kuidhinishiwa mamilioni ya shilingi ya mikopo ya halmashauri na kutotolewa kwa mabilioni ya kugharamia Mpango wa Kutoa Elimu msingi Bila Malipo, maarufu Elimu Bure.

Pia limo suala la kodi ya mapato iliyoripotiwa katika taarifa za fedha za Shirika la Mawasiliano Tanzania, taarifa za marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) Sh. bilioni 36.82 zikitofautiana na kodi ya mapato katika mfumo wa serikali (Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (ERCS) unaotumika kurekodi mapato yanayohusiana na sekta ya simu (Sh. bilioni 33.3).

Eneo lingine ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitengo cha Ushirikiano wa Viwanda (BICO) kilitekeleza miradi 98 toka mwaka 2017/18 hadi mwaka 2019/20 ya ukarabati miundombinu ya chuo kikuu kwa thamani ya Sh. bilioni 12.87 ingawa BICO haikuwa imesajiliwa kufanya kazi hizo na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB).

CAG Kichere amesema kuwa jambo hilo ni kinyume cha kifungu cha 10 cha Sheria ya Usajili ya Makandarasi ya mwaka 1997 kama ilivyorekebishwa na kifungu cha (9) na (10) cha Sheria ya Usajili wa Makandarasi (marekebisho) ya mwaka 2008.

## VYURA

Kwa mujibu wa CAG Kichere, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linagharamia dola za Marekani 130,000 kwa mwaka kwa ajili ya kutunza vyura hao, ambapo inakadiriwa takribani ya dola za Marekani milioni 2.86 zilitumika kwa miaka yote 22 ya kuhudumia vyura.

Katika mwaka wa fedha 2021/2022 ilifanya malipo ya shilingi milioni 611.92 (sawa na dola za Marekani 260,000).

CAG Kichere katika ripoti yake amesema: "Nimebaini kuwa mkataba kati ya Tanzania na bustani za wanyama za Marekani ulimalizika mnamo Juni 2020 na kuongezwa muda wa miaka miwili hadi Juni 2022.

"Japokuwa hakukuwa na mpango wowote wa kurudisha vyura hao Tanzania, ikizingatiwa kuwa tayari miaka 22 imepita tangu vyura 500 wapelekwe kwenye bustani za wanyama za huko Marekani.

"Napendekeza Shirika la Umeme Tanzania, kupitia Wizara ya Nishati na Wizara ya Maliasili na Utalii, iweke mpango mkakati wa kurudisha vyura wa Kihansi ili kuepuka gharama kwa Shirika la Umeme Tanzania."

## UPIGAJI TPA

Aidha, alisema Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) hadi kufikia Juni 30, 2022 ilikuwa na waidhinishaji wa akaunti zake 12 za benki, ambao hawakuwa wafanyakazi wa mamlaka hiyo baada ya kuhamishiwa kwenye taasisi zingine za serikali.

"Ni maoni yangu kuna mapungufu yaliyobainika yanatokana na ukosefu wa mipango ya usimamizi ya kuteua waidhinishaji wa akaunti kwa wakati, hivyo kuongeza hatari ya wafanyakazi wasio wa TPA kutoa fedha bila kujulikana na kuidhinishwa na mamlaka.

"Napendekeza kuwa TPA ihakikishe benki zote zina waidhinishaji waliothibitishwa kuwa ni wafanyakazi wa TPA na kuwajulisha benki mara moja kuhusu mabadiliko yanayohusiana na waidhinishaji wa akaunti za benki,"amesema.

Kuhusu malipo yaliyofanywa na Hifadhi za Taifa (TANAPA), CAG Kichere alisema amebaini kuwa malipo hayo yalifanyika kwa wafanyakazi mbalimbali kwa fedha taslimu, badala ya akaunti za benki katika miaka ya fedha 2019/20 na 2020/21.

## MCHEZO MAFUTA GHAFI

Amesema mafuta yenye kiasi cha lita milioni 3.29 yakihusisha kodi ya Sh. bilioni 2.6 yalibainika kuhifadhiwa kwenye matangi ya kampuni za mafuta kwa zaidi ya miezi sita bila kibali cha nyongeza ya siku kutoka kwa Kamishna Mkuu wa TRA.

Mafuta hayo yaliingizwa nchini, chini ya utaratibu wa ghala la dhamana na mitaji kutolewa kwenda nchi jirani au kubadilishwa utaratibu wa kuuzwa ndani ya nchi.

## ATCL MAUMIVU

Katika ripoti yake, CAG Kichere amesema Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) katika mwaka wa fedha 2020/21 lilipata hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 36.12, na mwaka 2021/2022 imepata hasara ya Sh. bilioni 35.2.

Amesema asilimia 96 za tiketi za ndege zilizotolewa na kampuni ya ndege, zilibatilishwa na mawakala.

"Tiketi inayobatilishwa ni tiketi ambayo imefutwa na kampuni ya ndege ambayo wakala wa usafiri alitoa tiketi. Malipo yote yaliyofanywa kwa ajili ya tiketi hiyo yanapaswa kurejeshwa kwa abiria," amesema.

Kichere amesema kwa mujibu wa ukaguzi tiketi 38,455 zilifutwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 na asilimia nne zilifutwa na ATCL na asilimia 96 za tiketi hizo zilifutwa na mawakala.

Kati ya tiketi hizo, tiketi 476 zilifutwa pia baada ya tarehe ya kutumika kinyume na miongozo ya Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga. Hii inaweza kusababisha upotevu wa mapato na wateja kushindwa kupata tiketi kwenye mfumo ikionyesha tiketi zimejaa, wakati kiuhalisia zina nafasi.

# Ukiukwaji mkubwa 'plea bargaining'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amebaini kuwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na maofisa wake walikiuka taratibu za makubaliano ya kukiri kosa katika kukamata, kuendesha mashtaka na kushughulikia kesi.

Katika ripoti ya ukaguzi maalum aliyoitoa jana kwa umma ya mwaka 2021/22, Kichere alisema ukiukwaji huo unaonyesha ukosefu wa uwazi katika uandikishaji mikataba ya kukiri kosa, ambao unahitaji uchunguzi zaidi wa uwezekano wa uwepo wa ukiukwaji wa maadili na matumizi mabaya ya mamlaka.

CAG alisema katika ukaguzi maalum kuhusu usimamizi na uendeshaji wa Mikataba ya Makubaliano ya kukiri kosa iliyosimamiwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilibainika washitakiwa wa makubaliano ya kukiri kosa hawajafanya malipo ya fidia ya Sh. bilioni 170.61 kama ilivyokubalika katika makubaliano ya kukiri kosa na hukumu za mahakama.

Pia alisema DPP alishindwa kukusanya ahadi hizo na hakuchukua hatua za kuwasilisha maombi ya kukamata mali kwa wale walioshindwa kutekeleza makubaliano ya ahadi.

Aidha, iligundulika kuwa DPP alikusanya Sh. bilioni 10.16 ambazo hazikuwa na uhusiano na mchakato wa kesi za kukiri kosa. Kadhalika, alisema ukaguzi ulibaini kasoro katika taratibu za kufuatilia mali na fedha zilizotaifishwa, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa daftari sahihi la kurekodi fedha na mali zilizotaifishwa.

"Kasoro hizi zilisababisha athari mbaya kama ile kupungua kwa thamani ya mali zilizotaifishwa na hasara ya kifedha kutokana na mali zilizosahaulika," alisema.

Pia alisema ukosefu wa taarifa za msingi za mali zilizotaifishwa baada ya uamuzi wa Mahakama, kunaonesha mapungufu katika usimamizi na ufuatiliaji wa mali zilizotaifishwa na ukaguzi ulibaini mapungufu katika usajili na umiliki wa magari yaliyotaifishwa na kutofanyika kwa tathmini ya mali zilizotaifishwa.

"Kulikuwa na mashaka juu ya usimamizi sahihi wa fedha zilizotaifishwa kutokana na kushindwa kurejeshwa kwa kiasi kikubwa cha fedha zilizotaifishwa kutoka kwenye mabenki ya biashara yaliyopo ndani na nje ya nchi. Kwa ujumla, ukaguzi umebaini haja ya uwepo wa taratibu bora za ufuatiliaji na usimamizi wa mali na fedha zilizotaifishwa," alisema.

HABARI KITAIFA

# Wabunge wataka agizo la Rais Samia ripoti CAG litekelezwe

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WABUNGE wametaka utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kuwataka watendaji waliotajwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2021/22 litekelezwe.

Akichangia jana bungeni mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa Fedha 2023/24, Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko, alisema Waziri Mkuu (Kassim Majaliwa) atakapohitimisha hoja ya bajeti hiyo, alieleze bunge kama watu hao wamepisha uchunguzi na chanzo cha ubadhirifu wa fedha za umma.

Wakati mbunge huyo akichangia Waziri wa Fedha na Mipango, Dk.Mwigulu Nchemba, alisema kinachoonekana kwenye ripoti hiyo ni uwazi wa Rais Samia kwenye uendeshaji wa serikali.

"Waziri Mkuu aje atuambie hawa watendaji waliotakiwa kupisha kama alivyosema Rais wamepisha? na lazima tujue chanzo cha ubadhirifu huo ili kukomesha ubadhirifu huu nchini," alisema Matiko.

Alisema amefuatilia suala la ndege ambayo ilinunuliwa kwa Dola za Marekani milioni 92 sawa na Sh. bilioni 220 na malipo ya awali yaliyotolewa yalikuwa Dola za Marekani milioni 55.

"Kwenye malipo yaliyokuwa yamebaki wameongeza malipo tena kufikia Dola za Marekani milioni 86 wakati nchi ina mahitaji mengi, tunategemea wahisani, tungependa aje atueleze, lazima bunge tusimamie na kuishauri serikali fedha hizi ni nyingi sana tukisema tuelekeze kwenye madarasa tungejenga madarasa 3,800 tusingeona msongamano wa watoto darasani."

"Tungesema fedha hizi tuelekeze kwenye vituo vya afya zingeenda kujenga vituo 234 ili kusaidia Watanzania wanaokufa kwa kukosa huduma za afya."


"Nyumba za walimu zingejengwa zaidi ya 2,000 wangeondokana na kukaa mbali na kutembea umbali mrefu, inasikitisha hawa watendaji kubadili malipo haya, Waziri wa Fedha mlipaji mkuu anatoka kwake tunataka kujua haya yote yanayotokea, ni mengi yanatokea huko kwenye fedha za walipa kodi,"alisema.

Mwigulu alisema utaratibu wa malipo uliowekwa nchini ni imara na vitu havipiti hivyo na hakuna malipo ya kila mwezi ambayo yanafanyika bila Rais Samia kujua.

"Malipo yakija tunawianisha na mapato na kuombea ridhaa kutoka kwa Rais, hata hilo la ndege lilivyoletwa yaliletwa mahitaji wizara tuliona yamekuja na ongezeko ambalo kama ni la kimkataba tupate ushauri kwa Mwanasheria Mkuu wa serikali hatukuwa nayo, tulikata malipo na utaratibu wa kimalipo ilibidi kutoa taarifa kwa mamlaka ambayo inaidhinisha na ilichukua hatua ya kusema hayo malipo yasilipwe,"alisema.

Alisisitiza hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa wale waliofanya mchezo huo wa kuongeza malipo ya ndege.

Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe, alisema fedha za bakaa kwenye halmashauri imekuwa ni tatizo na zingine zinafujwa na kusababisha wananchi kukosa miradi kwa uzembe wa watu wachache.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba akiwasilisha ripoti ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya ukaguzi wa serikali kuu kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wahamiaji haramu gerezani waigharimu serikali bil. 5/-

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WAHAMIAJI haramu 3,110 walioko katika magereza mbalimbali ambao wameshakamilisha adhabu za vifungo hawajarejeshwa makwao, hali inayoigharimu serikali Sh. bilioni 5.68 kwa mwaka.

Hayo yalibainika jana katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya ukaguzi kwa mwaka 2021/22 mbele ya waandishi wa habari jijini hapa.

Katika ripoti hiyo iliyowasilishwa jana, CAG Charles Kichere alisema kifungu cha 24 cha Sheria ya Uhamiaji (Sura ya 54) ya mwaka 2016 kinafanya kuwa ni kinyume cha sheria kwa wahamiaji haramu kuingia au kubaki Tanzania.

Alisema Kanuni namba 538 ya Kanuni za Kudumu za Magereza za mwaka 2003 inaeleza kuwa mtu anayesubiri kufukuzwa na kuwekwa kizuizini gerezani kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Wakimbizi ya mwaka 1998, anatakiwa kuchukuliwa kama mfungwa ambaye hajahukumiwa na kwa mujibu wa sheria na kanuni zote zinazotumika kwa tabaka hili la wafungwa.

CAG alisema katika ukaguzi wake alibaini Jeshi la Magereza lina wahamiaji 4,419 haramu kutoka nchi mbalimbali, huku 1,264 wakiendelea kutumikia vifungo, 45 wamewekwa mahabusu na 3,110 wanaotakiwa kurejeshwa makwao.

"Uwapo wa wafungwa ambao wamemaliza vifungo vyao lakini bado wako gerezani katika kipindi cha mwaka mmoja hadi mitano unatokana na kutokutolewa amri ya kuachiliwa huru na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi," alisema Kichere.

Alisema gharama za kuwahudumia wahamiaji hao ni kubwa, huku chakula cha mfungwa mmoja kilitengewa bajeti ya Sh. 5,000 kwa siku na kitendo cha kuwa na wahamiaji 3,110 katika magereza hayo huigharimu Sh. bilioni 5.68 kwa mwaka, hivyo kuipa mzigo serikali.

"Jeshi la Magereza limeitaka Idara ya Uhamiaji kuchukua hatua stahiki za kuwarejesha makwao wahamiaji haramu wanaomaliza vifungo vyao ili kuepuka gharama za ziada. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ametoa maagizo ya kuzuiwa ili kuwabakisha wafungwa wa kigeni wanaohitaji kurejeshwa makwao." alisema.

Hata hivyo, alisema kuwafukuza wahamiaji haramu ni suala la kidiplomasia linalohitaji mashauriano na mabalozi wa nje ya nchi huku akitoa wito kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kufanya juhudi zaidi kuhakikisha maagizo yanatolewa kikamilifu ili kuwarejesha raia wa kigeni walioachiliwa huru ili kupunguza gharama zisizo za lazima.

# Vikundi hewa 48 vyatafuna mil. 896/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amebaini uwapo wa vikundi hewa 48 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilivyopewa mikopo ya Sh. milioni 895.94.

Pamoja na kupewa mamilioni hayo, maofisa maendeleo ya jamii wa kata husika hawakufahamu lolote kuhusu vikundi hivyo.

Kutokana na hilo, ameshauri Ofisi ya Rais TAMISEMI ichukue hatua stahiki kwa watumishi waliotoa mikopo kwa vikundi ambavyo hapakuwa na taarifa za kuwepo kwao, ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwenye vyombo vya uchunguzi.

CAG Kichere alibainisha hayo katika ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2021/22, aliyowasilisha jana bungeni na kuzungumza na waandishi wa habari.

Katika ripoti hiyo, CAG alishindwa kujiridhisha juu ya kuwepo kwa vikundi hivyo kwenye Mamlaka tatu za Serikali za Mitaa.

Alitaja halmashauri hizo kuwa ni Jiji la Dar es Salaam vikundi 34 (Sh.milioni 698.7, Manispaa ya Temeke vikundi tisa (Sh. milioni 178.5) huku Halmashauri ya Wilaya ya Meru vikundi vitano (Sh. milioni 18.7).

"Nina shaka juu ya uamuzi wa mamlaka hizo za serikali za mitaa wa kutoa mikopo kwa vikundi ambavyo hata maofisa maendeleo ya jamii wa kata husika hawana taarifa zao. Hii inaashiria matumizi mabaya ya fedha za umma."

Aidha, alisema tathmini yake kuhusu mikopo iliyotolewa kwa vikundi ilibaini mamlaka tisa za Serikali za Mitaa zilikuwa zikitoa mikopo ambayo haijarejeshwa ya Sh.bilioni 2.25 kutoka kwenye vikundi 627 vilivyositisha shughuli zao za biashara.

"Nimebaini kuwepo na ongezeko la mikopo ambayo haikurejeshwa kutoka kwenye vikundi hadi kufikia Sh.bilioni 39.72 kwenye mamlaka 78 za Serikali za Mitaa,"alisema.

"Napenda kusisitiza pendekezo langu la mwaka uliopita kwamba, Ofisi ya Rais TAMISEMI iangalie uwezekano wa kutumia Benki za Serikali, kama vile Benki ya Biashara Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania na Mameneja wa Mifuko wenye uzoefu na utaalamu wa kutosha katika kutathmini, kutoa na kusimamia urejeshwaji wa mikopo ili kuhakikisha mikopo inatolewa kwa ufanisi na inafuatiliwa na kulipwa; kwa gharama ndogo za uendeshaji," alisisitiza.

Aidha, alishauri Ofisi ya Rais TAMISEMI kuandaa sera ya mikopo isiyolipika 'NPL' ili kusimamia mikopo inayotolewa kwa vikundi kwa lengo la kupunguza upotevu wa fedha zinazotolewa kama mikopo.

**FEDHA ELIMU BURE**

Katika mwaka wa fedha 2021/22, alisema Serikali haikutoa ruzuku ya fedha za kugharamia elimu bure Sh. bilioni 5.8 kati ya Sh. bilioni 33.07 zilizohitajika katika mamlaka 25 za serikali za mitaa.

"Kutolewa kwa fedha pungufu kunaathiri matokeo ya wanafunzi kitaaluma, kwani shule nyingi hazina mahitaji muhimu kama vile miundombinu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia,"alisema.

Alipendekeza Hazina na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhakikisha fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya kugharamia utoaji wa elimu bure zinatolewa kwa mamlaka za serikali za mitaa, ili kuimarisha utoaji wa elimu bora nchini.



Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Puma Energy Tanzania, Fatma Abdallah, akiwashukuru wageni waalikwa mbalimbali baada ya futari iliyoandaliwa na kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam juzi, iliyohudhuriwa na Kaimu Shekhe wa Mkoa huo, Walid Alhad Kawambwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uwekezaji MSD waleta neema wagonjwa wa figo

**Idda Mushi na Elizabeth Zaya,** DODOMA

GHARAMA za usafishaji damu nchini zinatarajia kupungua baada ya serikali kuleta vifaa vya huduma hiyo, kutokana na uwekezaji uliofanyika Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

Akizungumza na waharirI wa habari jijini Dodoma jana, Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavere Tukai, alisema awali gharama ya huduma hiyo ilikuwa kubwa kutokana na ukosefu wa vifaa na kwamba serikali imeleta mashine 140 kwa ajili ya kazi hiyo ambazo zimeshasambazwa kwenye vituo 14 vilivyotengwa kwa ajili ya huduma hiyo.

Alisema kabla ya kuletwa kwa mashine hizo zilipatikana katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, jambo lililosababisha gharama kuwa kubwa zaidi na wananchi wengi kushindwa kumudu.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, mashine hizo zimefungwa kwenye vituo vitano vya kutolea huduma hiyo vya Hospitali ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Mwananyamala, Tumbi mkoani Pwani, Sekou Toure mkoani Mwanza na Chato mkoani Geita.

Meneja Uhakiki Udhibiti Ubora wa MSD, Mwanashehe Jumaa, alisema licha ya hospitali hizo kufungiwa mashine hizo, tayari bodi hiyo imeshafanya ukaguzi katika vituo vingine vinne zaidi vya kutolea huduma na viko tayari kufungiwa mashine hizo wakati wowote kutoka sasa.

Alitaja vituo vingine ni pamoja na hospitali za rufani za mikoa za Dodoma, Lindi, Morogoro na Mawenzi mkoani Kilimanjaro.

"Kila kituo kinatarajia kupokea mashine 10 za kusafisha damu na kuna vituo vingine vitano vilivyobaki ambavyo tunaandaa mazingira rafiki kwa ajili ya kufunga mashine hizi, hii itasaidia sana kupunguza gharama kwa wagonjwa.

"Kwa wiki mgonjwa hulazimika kusafisha figo angalau mara tatu, lakini wengine walishindwa kutokana na umbali pamoja na gharama," alisema Mwanashehe.

Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa MSD, Etty Kusiluka, alisema mashine hizo zimekuja wakati mwafaka kwa sababu changamoto ya magonjwa ya figo imekuwa kubwa nchini kutokana na sababu mbalimbali na kwamba ujio wake utarahisisha upatikanaji wa huduma bora na nafuu kwa wananchi. Mmoja wa washiriki wa warsha hiyo, Imelda Mtema kutoka Global TV, alipongeza MSD kwa kuleta mashine hizo akisema yeye ni shuhuda wa watu walipoteza wapendwa wao kutokana na kushindwa kumudu gharama za matumizi ya huduna hiyo ya kusafisha damu.

Novemba, mwaka jana, akizungumza na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Benard Konga, alisema gharama za usafishaji damu ni miongoni mwa ambayo yamekuwa mzigo mkubwa kwa mfuko huo.

Alisema kwamba kwa mwaka wa fedha 2021/22, NHIF ilitumia fedha nyingi katika kulipia magonjwa yasiyo ya kuambukizwa, ikiwamo huduma ya kusafisha damu ambayo wanachama wake walitibiwa.

Konga alisema huduma ya usafishaji damu imekuwa ikifanywa na watoa huduma za afya kwa kati ya Sh. 240,000 hadi Sh. 250,000 kwa awamu moja ambapo kwa wiki mgonjwa hushauriwa kufanya kati ya mara tatu hadi nne kwa wiki sawa na zaidi ya Sh. milioni moja kwa wiki na milioni 52 kwa mwaka.

# Anusurika kifo baada ya kujikata sehemu za siri

**Na Vitus Audax,** MWANZA

ANSELUMU Sebuka (42) mkazi wa kitongoji cha Kasuzu, Kata ya Namagondo, Ukerewe mkoani Mwanza, amenusurika kifo baada ya kukata uume wake kwa kutumia kisu chenye ncha kali na kubaki ukining'inia kwa madai ya kuhofia kutengwa na ndugu zake.

Sebuka alifikia uamuzi huo Aprili 4, mwaka huu, majira ya saa 2:00 usiku kwa kile kinachodaiwa kuwa alikuwa anatuhumiwa na ndugu zake kuiba mali mbalimbali za familia na za jamii inayomzunguka na kwenda kuziuza.

Mbali na kuiba na kuuza mali hizo, anadaiwa pia kujiingiza katika ulevi uliokithiri, hivyo familia yake iliamua kumtenga kutokana na tabia zake mbaya.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbroad Mutafungwa, katika taarifa yake iliyotolewa juzi, alisema tukio hilo lilimkuta mwanamume huyo ndani ya chumba chake akiwa amejaribu kujiua kwa kukata uume kwa kutumia kisu chenye ncha kali.

Mutafungwa alisema chanzo cha tukio hilo ni ugomvi wa kifamilia uliosababisha mwanamume huyo kupata msongo wa mawazo na baada ya kumkuta katika hali hiyo alipelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe kwa ajili ya matibabu na hali yake inaendelea vizuri.

Kamanda Mutafungwa aliwataka wananchi kufuata njia sahihi za kutatua matatizo yao hususani kuwaona wataalamu wa afya ya akili ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na msongo wa mawazo na kukosa uvumilivu wa migogoro mbalimbali katika jamii.

Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi mkoani Mwanza linamshikilia Mathayo Mishaka (40), mkulima na mkazi wa kijiji cha Sumaha, akituhumiwa kumchapa mtoto wake Milembe Mihayo (11) na kumsababishia kifo.

Ilielezwa kuwa baada ya mahojiano, mtuhumiwa huyo alikiri kuhusika na mauaji ya binti yake kwa kumchapa na fimbo sehemu za mwili wake baada ya kumkuta nyumbani kwa babu yake mdogo aitwaye Dotto Masanyiwa akikokuwa ameagizwa, wakiwa bafuni na mvulana aliyekimbia baada ya kufumaniwa wakiwa wamevua nguo wakitaka kufanya mapenzi.

Baada ya kupigwa mtoto, huyu aliendelea kupata maumivu makali bila kupelekwa hospitalini ndipo baba yake huyo mzazi akamwagiza mke wake mdogo, Sofia Mashaka, amkande miguu binti iliyokuwa imevimba kutokana na kipigo.

# Serikali yasema ugonjwa wa Marburg haupo nchini

**Na Romana Mallya**

WIZARA ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imewahakikishia mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao nchini kwamba Tanzania ni salama kuhusiana na ugonjwa wa Marburg.

Vilevile, imesema hakuna hali ya kutisha wala sababu ya kuzuia raia wao kuja Tanzania na kuomba ushirikiano na nguvu ya pamoja ya utafiti wa magonjwa ya milipuko, ili kuyatafutia ufumbuzi yasitokee tena.

Machi 16, mwaka huu, katika vijiji viwili mkoani Kagera kuliripotiwa vifo vya watu watano na wengine wanane kuugua na uchunguzi ulibaini ni Marburg na tayari serikali imeudhibiti na mpaka sasa hakuna kesi mpya. Kutokana na ugonjwa huo, watu 200 waliwekwa karantini.

Kwa mujibu wa Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Stergomena Tax, hadi jana kati ya watu watatu waliokuwa wamelazwa, mmoja ameruhusiwa.

Akizungumza katika mkutano kati ya wizara hiyo na mabalozi hao kuhusiana na ugonjwa huo, Balozi Tax alisema tangu kutangazwa kuwapo kwa ugonjwa huo nchini, mikakati mbalimbali ya kuudhibiti imefanyika na kwa sasa nchi ipo salama.

Waziri huyo alisema zipo taratibu zimewekwa kwa wanaoingia, wanaangaliwa na upo ufuatiliaji wa hali ya juu unaofanyika.

"Nimekutana na mabalozi kuwapatia taarifa ya hali ilivyo kuhusiana na ugonjwa ambao mwanzo haukujulikana uliotokea Kagera lakini baada ya hatua za haraka kuchukuliwa na serikali uliweza kujulikana kama ni Marburg.

"Taarifa niliyowapa Waheshimiwa Mabalozi ni kwamba walipatikana wagonjwa wanane kama ilivyotolewa taarifa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, watano walifariki, watatu walibaki hospitali na kati yao, mmoja ameruhusiwa jana na anaendelea vizuri, waliobaki nao wanaendelea na matibabu," alisema Waziri Tax alisema wamekutana na mabalozi hao kwa kuwa ndio wanaowakilisha nchi zao Tanzania, hivyo ni muhimu wafahamu hatua zilizochukuliwa na hali ilivyo.

"Kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Afya juzi, hali ipo vizuri, ugonjwa kwa sasa umedhibitiwa, tangu wale wagojwa wa mwanzo hakujawa na wagonjwa wengine," alisema.

Alisema mabalozi wameridhika kwa hatua za haraka na madhubuti zilizochukuliwa na kuipongeza serikali na kuahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania.

"Waandishi wa habari niwaombe muendelee kuitolea taarifa vizuri, isipotolewa vizuri inaweza kuathiri uchumi wetu, tutajikuta watu wanaacha kuja nchini kwetu na kwa maana hiyo tutakuwa na athari kubwa za kibiashara na kiuchumi, tuendelee kupashana habari," alisema.

Alisema nchi yoyote inayojitambua na inataka kuendelea lazima ifanye utafiti, ndio maana Tanzania vipo vituo vya utafiti katika masuala hayo.

"Utafiti unaendelea katika maeneo mbalimbali, ombi langu kwa mabalozi, nimewaomba kukusanya nguvu ya pamoja kwamba, utafiti humu ndani tunafanya lakini maarifa na uzoefu tunatofautiana.

"Ndiyo maana nikasema tukusanye nguvu za ndani, tukusanye nguvu za kanda au kiafrika na kukusanya nguvu kimataifa kwa sababu haya magonjwa ya milipuko yamekuwa yakitokea mara kwa mara, na kulikuwa na maswali chanzo ni nini? Inakuaje?Mambo yote hayo tunaweza kuyafanyia kazi kwa pamoja na kukusanya nguvu na kwenda kwa kasi zaidi na kutatua hili tatizo.

"Tunapenda baadhi ya haya magonjwa yaweze kutatuliwa yasitokee tena, hiki ni kitu kikubwa kinahitaji nguvu kubwa, kiakili na kirasilimali humu ndani tunafanya lakini, tunataka na wenzetu waje tufanye nao," alisema.

# Spika ataka kipaumbele ajira za afya, walimu wanaojitolea

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk.Tulia Ackson ameielekeza serikali kuangalia namna ya kuandaa taarifa za watumishi wa afya na walimu wanaojitolea kila mwaka, ili kuwapa kipaumbele kwenye ajira zinazotangazwa.

Dk.Tulia aliyasema hayo jana bungeni mara baada ya Naibu Waziri wa Afya, Dk.Godwin Mollel kujibu maswali ya Mbunge wa Viti maalum (Chadema), Felista Njau.

Spika huyo alisema kuna haja ya Waziri wa Afya na Waziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kuliangalia suala hilo kwa kuwa haipendezi watumishi wa afya na walimu wanaojitolea shule za msingi na sekondari kukosa ajira.

"Haipendezi sana wao kukosa ajira ina maana wao hawana sifa ya kupata ajira kwa sababu ajira zikitangazwa ukiangalia jimboni kwako hakuna hata mmoja aliyepata, sasa tunajiuliza huwa wanaojitolea hawana sifa? na wale wanaokaa nyumbani wanasifa kuzidi wengine,"alisema.

Alitaka zitengenezwe taarifa za kila mwaka, ili kuwazingatia wanaojitolea kuwapa kipaumbele katika ajira zinazotangazwa.

"Hatua hii itatupunguzia changamoto kipindi hiki ambacho majengo mengi yanajengwa lakini pia kwenye elimu ni muhimu sana wale wanaojitolea kupewa kipaumbele,"alisema.

Katika swali lake, Mbunge Njau alihoji lini serikali itawaajiri wataalamu wanaojitolea kwa muda mrefu kufanya kazi katika hospitali mbalimbali nchini.

Dk.Mollel akijibu swali hilo alikiri kuwa hospitali zimekuwa na watumishi wanaojitolea, Wizara imetoa mwongozo wa kuwalipa nusu mshahara kwa mapato ya ndani.

"Hata hivyo hospitali zetu za Mikoa, Kanda na Taifa zimeweza kuwalipa hadi asilimia 40 ya watumishi wote wanaojitolea mshahara kamili kwa kutumia mapato ya ndani,"alisema.

Aidha, alisema wizara itashirikiana na Wizara ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuona namna bora ya kuwapa kipaumbele kwenye ajira watumishi ambao wamekuwa wakijitolea kwenye vituo vya huduma za afya kuliko walioko nje kusubiri ajira.

Katika swali la nyongeza, Mbunge Njau alisema mahitaji ya watumishi wa afya nchini 336,453 waliopo ni 114,582 sawa na asilimia 34 tu, upungufu ni 221,946.

"Upungufu huu ni mkubwa serikali ina mpango gani ili kunusuru afya za watanzania?, Serikali haioni umuhimu wa kutengeneza kanzidata kwa ajili ya kuwatambua wahudumu wote wanaojitolea ili wapate kipaumbele kwenye ajira?,"alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri huyo aliahidi kuzingatia ushauri wa kuweka kanzidata kwa ajili ya kuwatambua wanaojitolea wakati wa ajira wapewe kipaumbele.

# Kamishna mstaafu ataja mwarobaini kupunguza malalamiko dhidi ya polisi

**Na Restuta James**

NAIBU Kamishna wa Polisi (DCP) mstaafu, Mboje Kanga, ametaja mwarobaini wa kupunguza malalamiko ya wananchi kwa Jeshi la Polisi kuwa ni kufanyika tathimini ya mafunzo, mfumo wa ajira na upandishaji vyeo.

Alisema hayo jana jijini Dar es Salaam baada ya kuwasilisha maoni yake mbele ya Tume ya Kuboresha Mifumo ya Hakijinai na kueleza kuwa ziko kasoro chache kwenye maeneo hayo ambazo zinaathiri utendaji wa polisi.

"Ziko kasoro chache chache ambazo zikifanyiwa kazi zinaweza zikatusaidia tukawa na jeshi ambalo ni zuri, linalofuata maadili, lenye kujituma na uzalendo mkubwa," alisema.

Kanga alizungumzia pia ukamataji wa wahalifu na dhamana, alisema ni maeneo yanayopaswa kuangaliwa kwa kuwa yanaibua malalamiko kwa polisi kutokana na askari kukamata mhalifu kinyume cha utaratibu.

DCP Kanga alisema kuna ukamataji salama ambao haujengi chuki kati ya askari na mhalifu na baada ya kufikishwa kituoni, askari anapaswa kuzingatia haki na kumpa mtuhumiwa dhamana kwa makosa yanayostahili haki hiyo.

"Wakati mwingine malalamiko yanatokea kwa sababu unakuta kosa lina dhamana lakini unakuta haiwi hivyo," alisema.

Kuhusu ucheleweshaji wa upelelezi, alipendekeza kuwa serikali itenge fedha za kuwezesha kazi hiyo, vitendea kazi na shajara (stationary). Pia alipendekeza kuwapo kwa ushirikiano wa karibu kati ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (DPP) na Idara ya Upelelezi wa makosa ya Jinai ili majalada yanayopelekwa kwenye ofisi hiyo yashughulikiwe kwa wakati.

DCP Kanga alipendekeza wapelelezi wapewe muda maalum wa kupeleleza kesi hususani ndogo ndogo ili kupunguza msongamano mahabusu.

**TUME YAHAMIA ZANZIBAR**

Taarifa iliyotolewa na Tume hiyo kwa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, ilisema ikiwa visiwani Zanziba, itakutana na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili, Hemed Suleiman Abdullah.

Tume hiyo itakutana pia na Rais mstaafu, Dk. Ali Mohamed Shein, Jumanne ijayo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, tume itakutana na viongozi wa dini, watoto, vijana, wanawake na wazee.

Kadhalika, itatembelea Chuo cha Mafunzo Kinua Miguu na kuongea na wakufunzi, itakagua Chuo cha Polisi Ziwani na maofisa wa polisi pamoja na askari wa vyeo vya chini.

Tume hiyo itakuwa na mikutano ya wazi ili kupokea maoni ya wananchi katika ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdulwakil. Pia itakutana na viongozi wa dini pamoja na wawakilishi wa asasi za kiraia katika mikoa yote ya Uguja na Pemba.

# NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA 2. KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | IGELEGELE BUGARIKA NA BUJINGWA-MWANZA | 27/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MANGWE EMMAUEL WAMBURA | VIWANJA VIWILI VYENYE HATI MILIKI | MANGWE EMMANUEL WAMBURA | ILALILA-MWANZA | 28/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | CHRISTOPHER MANGARAYA WAMBURA | KIWANJA | CHRISTOPHER MANGARAYA WAMBURA | BUJINGWA-MWANZA | 28/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | HAWA HATIBU MUNISI | NYUMBA | RESTUS JULIUS KIMATH | NYASAKA-MWANZA | 24/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | FRIDA FRANCIS KAJUNA | NYUMBA | FRIDA FRANCIS KAJUNA | GEITA | 28/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JAMES JACOB KALULEMA | NYUMBA | JAMES JACOB KALULEMA | MAHINA KANYERERE-MWANZA | 18/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | SIKITU HAMIS YAHAYA | NYUMBA | HAJI ABEID KASUBI | NYASAKA ILEMELA MWANZA | 19/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | DICKSON ANICETH GREEN | NYUMBA | DICKSON ANICETH GREEN | LUKOBE-MWANZA | 19/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | FELISTA MATOKE NYANGWE | NYUMBA YENYE HATI NA.45634,KIWANJA NA.183 KITALU 'B' | SOPHIA KIBOKO CHACHA | KISEKE-MWANZA | 25/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JUMANNE MOHAMED KAPOLI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MATHIAS CHARLES NDETTO | KISESA-MWANZA | 08/05/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | FALLACK ADAM RUTUNGO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MADADIA ALLY SANKA | MKOLANI NYAMAGANA | 28/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JEREMIA DIBOGO MITOKO | NYUMBA HATI NAMBA 53828, KIWANJA NA. 312, KITALU "A" | VICTOR ELIAS MWIJAGE | NYASAKA ILEMELA | 25/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | ISIMBULA MAULID RAJABU | KIWANJA | ISIMBULA MAULID RAJABU | MURIET -ARUSHA | 25/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ARUSHA | MASANJA AJMES WANNA | KIWANJA | MASSANJA JAMES WANNA | MURIET -ARUSHA | 20/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ARUSHA | JOHN LEONARD MAIGE | KIWANJA | JOHN LEONARD MAIGE | MURIET -ARUSHA | 20/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | ABDILLAHI SAIDI KANYWANYI | NYUMBA | ABDILLAHI SAIDI KANYWANYI | YOMBO VITUKA-SIGARA | 25/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | NYUMBA | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | MBAGALA KIBURUGWA | 17/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | SEVERINI BONAVENTURA LYIMO | NYUMBA | SEVERINI BONAVENTURA LYIMO | MBEZI MTONI-MTONGANI | 27/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | MAGRESTH RHOBI SASI | NYUMBA | MAGRESTH RHOBI SASI | MBONDOLE MSONGOLA | 28/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | KAIMU SAID AMANZI | NYUMBA | KAIMU SAID AMANZI | MVULENI-MSONGOLA | 28/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | ZULFA SHAFII MALENDA | NYUMBA | HALIMA SHAFII MALENDA | NZASA -CHARAMBE | 14/04/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | ZAINABU RASHIDI LUKWELE | NYUMBA | OMARI SAIDI MAINGO | MKURANGA | 20/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | AMRI BAKARI MAKANYA | NYUMBA | MWANAHAMISI KASSIM YUSUPH | KITUNDA | 19/04/2023 SAA 8:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | FAISAL SALUM HASSAN | 1.NYUMBA 2.GARI T396 DJR HINO RAINBOW | FAISAL SALUM HASSAN | 1.KIGOGO-KIGAMBONI 2.TEMEKE | 24/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | SHERAL SELEMANI HUSSEIN | GARI TATA BUS T357 DSR | SHERAL SELEMANI HUSSEIN | MBAGALA MAJIMATITU | 17/04/2023 SAA 06:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | YUSUPH MOHAMED ALLY | NYUMBA | YUSUPH MOHAMED ALLY | SAGULO PUGU | 25/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | TRAZIAS ISHENGOMA | NYUMBA | TRAZIAS ISHENGOMA | MBAGALA MWANAMTOTI | 24/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | MBAWALA ACADEMCY | NYUMBA | RAMADHANI JUMANNE MBAWALA | CHAMAZI MSUFINI | 24/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | HAMAD ABDALLA MNEMBWE | NYUMBA | HAMAD ABDALLA MNEMBWE | TANDALE | 20/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | HALIMA JUMA MZUNGU | NYUMBA | MIRIAM HARUNA MZUNGU | BOMANG'OMBE HAI | 22/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | SAMWEL JOHN GONZA | NYUMBA | SAMWEL JOHN GONZA | BOMANG'OMBE HAI | 25/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | SHAFII SWALEHE MRUMA | NYUMBA | SHAFII SWALEHE MRUMA | MATINDIGANI-PASUA | 29/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | PETER AMANI CHIWONE | NYUMBA | PETER AMANI CHIWONE | SHABAHA-MOSHI | 02/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | MWANTUM RASHID MOHAMED | NYUMBA | MOHAMED KASIM MADI | BOMANG'OMBE HAI | 04/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | HASSAN HUSSEIN NGAIRY | KIWANJA CHENYE HATI MILIKI | HASSAN HUSSEIN NGAIRY | BOMANG'OMBE HAI | 08/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | EMANUEL DANIEL SORORWA | NYUMBA | FRANK THOMAS KIVUYO | KITONGOJI CHA ILKIUSHIN KATA YA OLTURUMET ARUSHA | 26/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | ABOUBAKER O. HASSAN AND OR SAINECHA | KIWANJA HATI NAMBA 113599 KITALU 'G' TEGETA NA KIWANJA HATI NAMBA 105871 KITALU '12' KIBADA | ABOUBAKER O. HASSAN | TEGETA NA KIBADA | 28/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 24/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | BRAITON RUBEN MWANKEMWA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | BRAITON RUBEN MWANKEMWA | IVUMWE -MBEYA | 17/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 20/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BARAKA PAUL DABAVUNJE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | BARAKA PAUL DABAVUNJE | UYOLE-MBEYA | 17/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | LYDIA NICODEMU MWANDUMBYA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | ASIFIWE MWAIPAJA | IGANZO-MBEYA | 27/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 28/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | MWANJELWA , MBEYA MJINI | 28/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | KITETE-MBEYA | 28/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BENARD ANAEL CHUNGU | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | BENARD ANAEL CHUNGU | IYOTO-MBEYA | 12/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | THOMAS JOSEPH KAPINGA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | THOMAS JOSEPH KAPINGA | IGANZO-MBEYA | 12/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | MAMU PHARMACY | GARI MITSUBISHI CANTER T516 DKX | AHMAD KASSIM OMARY | POSTA-ILALA | 24/04/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 28/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK033735 | DAVID ABEL MLAU | CHARAMBE -MBAGALA | 28/04/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0715868000/0754376493/0714939933/0759648448/0759282344/0753575752**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kauli ufisadi zimewachosha wananchi, hatua zichukuliwe

**TAARIFA** za ubadhirifu, serikali kupata hasara na miradi kufanyika chini ya kiwango kulingana na fedha zilizotolewa zimekuwa wimbo wa kawaida kusikika masikioni mwa Watanzania katika miaka ya sasa. Viongozi wa juu wanaposimama wimbo umekuwa huo huo kwamba kuna harufu ya ufisadi mahali iwe katika utekelezaji wa mradi au fedha zilizotolewa kwa ajili ya kazi fulani.

Hata Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuanzia mkurugenzi wake mkuu hadi wakuu wa taasisi wa mikoa, kila wanapotoa taarifa za uchunguzi, suala la kuokoa fedha zilizokuwa hatarini kuingia katika mifuko ya wajanja au kuwapo kwa ubadhirifu mahali fulani, kwao ni jambo la kawaida.

Hivi karibuni pia, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, aliwasilisha taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha wa 2021/22 kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Katika taarifa hiyo alianika madudu katika taasisi mbalimbali za serikali yanayoonyesha kuwa kuna upigaji wa kutisha kwenye mikataba na matumizi ya fedha zilizotolewa na serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kama vile haitoshi, juzi Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati akiwasilisha Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Ofisi ya waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2023/24, alisema miradi 119 ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 46.04, inachunguzwa baada ya kubainika kuwa na kasoro mbalimbali katika utekelezaji wake.

Waziri Mkuu alibainisha kuwa miradi hiyo ni kati ya miradi 810 yenye thamani ya Sh. trilioni 6.89 iliyofuatiliwa na kwamba inaendelea kufanyiwa uchunguzi ili hatua stahiki zichukuliwe. Licha ya kubainisha hayo, serikali itaendeleza mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi kwa kuweka kipaumbele katika kuzuia vitendo vya rushwa. Kauli ya Waziri Mkuu kuhusu uwapo wa miradi inayofuatiliwa na kuchunguzwa baada ya kubainika kuna kasoro katika utekelezaji halikuwa geni masikioni mwa Watanzania wengi. Kwa maneno mengine, kauli hiyo ilitarajiwa kutokana na ukweli kwamba suala la ubadhirifu na upigaji wa fedha za umma katika maeneo mbalimbali na kwenye taasisi za serikali ni jambo la kawaida.


Pamoja na kwamba ni jambo la kawaida, swali ambalo limo vichwani mwa Watanzania wengi ni je, hadithi kama hiyo isiyo na mwisho itaendelea kusikika hata lini kutoka katika vinywa vya viongozi? Swali lingine ni je, wanaohusika na vitendo hivyo vyenye kuleta picha mbaya katika serikali kwa nini hawachukuliwi hatua ili iwe mfano kwa wengine, na wameshindikana ndiyo maana wimbo huo unajirudia? Kama alivyosema Rais Samia baada ya kupokea ripoti ya CAG, ni dhahiri kwamba watu hao wapo lakini waliopewa dhamana ya kusimamia nidhamu na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya watu hao wamelegalega ndiyo maana watu hao wapo na wanaendelea kufanya mambo kama hayo.

Jambo la kujiuliza ni kwamba watu, wakiwamo wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa na makatibu wakuu na naibu makatibu wakuu wa wizara, kabla ya kuingia ofisini wanakula kiapo cha maadili. Sasa inakuwaje baada tu ya kuingia kazini wanahusishwa na ubadhirifu au kushindwa kuwasimamia watu wa chini yao na matokeo yake taarifa za madudu zinasikika?

Wakati umefika sasa kwa taasisi kama TAKUKURU na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali (DPP) kwa kushirikiana na mamlaka zingine, kuchukua hatua zinazostahili dhidi ya wanaohusika na madudu hayo.

Ni imani kwamba kwa kufanya hivyo, kutakuwapo hofu kwa baadhi ya watumishi na maofisa wanaopewa dhamana ya uongozi katika taasisi za serikali. Watu hao watatambua kuwa iwapo wataingia katika ufisadi wa fedha za umma, ni wazi sheria itachukua mkondo dhidi yao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Ni vema sana kwa hili la Askofu Malasusa nawe umekemea ushoga

Na Halfani Chusi

**ASKOFU** wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheli Tanzania (KKKT) Alex Malasusa, amewataka walimu, wazazi na viongozi wa dini kuungana kukemea vitendo vya ushoga akidai sio suala la kuiachia serikali pekee.

Malasusa, alitoa rai hiyo kwenye maadhimisho ya miaka 30 ya elimu yaliyoandaliwa na Dayosisi ya Mashariki na Pwani ya KKKT, yaliyohudhuriwa na wanafunzi pamoja na wachungaji kutoka makanisa mbalimbali.

Akitoa hotuba yake kwenye maadhimisho hayo alisema kipindi tunachopitia ni kigumu sana watoto wanaiga mambo kutoka kwenye mitandao ya kijamii ambayo sio utamaduni wetu.

"Kama unafuatilia habari unasikia mambo ya hovyo yanaigwa kutoka nje na sio utamaduni wetu, na yanaletwa ili tuyazoee kichwani tuone kama kitu cha kawaida mambo ya ushoga ni ya kishetani wala hatumung'unyi maneno," anasema askofu na kuongeza:

"Ni mambo ya ajabu hata wanyama hawafanyi hivyo, nataka wanafunzi wazazi na walimu mjue kuwa ushoga ni mambo ya kishetani. Kama wako waliokengeuka tuendelee kuwaombea wala hatupaswi kuwatuhumu."

Malasusa alitumia mkutano huo kuwaagiza walimu wote nchini pamoja na viongozi wa dini mbalimbali kuzuia vitu vinavyoweza kuingia kwenye ubongo wa mwananfunzi na kubadili fikra kwa kuiga tabia zisizofaa kama ushoga.

"Hapa niseme, kutoka wanafunzi wa awali mpaka chuo kikuu ushoga kwetu mwiko, hebu semeni wanafunzi ushoga mwiko," kauli iliyoungwa mkono kwa kushangiliwa kwa mwitikio 'hatutaki kumuona mtu shoga'.

"Ukiona mtu anazungumzia hilo chukua jina lake peleka kwa mchungaji au nitakuja mwenyewe tena nasikia wachungaji mnasema mnasubiri serikali mpaka itusemee hapana hili ni la kiroho tutapambana nalo wenyewe, tutasimama imara sisi ndio wakupambana," aliyeonekana kukerwa na vitendo hivyo

Pia, akawakumbusha wachungaji wote nchini kutumia sikukuu ya Pasaka na mfungo wa Kwaresma, kukemea suala hilo kwa nguvu akikumbushia kuwa kanisa lake la (KKKT), lilianza kukemea ushoga tangu mwaka 2010 kwa kuandika chapisho linalosema 'Ushoga Basi'.

Ni jambo, linalopaswa kuungwa mkono kwa nguvu zote ni ukweli usiopingika kuwa ushoga sio utamaduni wa kitanzania, lakini kadri siku zinavyosonga mbele kizazi kinazidi kuharibika.

Hali hiyo inachangia kuwapoteza wanaume wenye uwezo wa kuzalisha, na waswahili husema 'bidhaa adimu inatoweka' mbali na hivyo wazazi pia wanapaswa kusimama kidete kwenye malezi.

Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza anasema miongoni mwa mambo ambayo mara nyingi huchangia watoto kujiingiza kwenye ushoga ni pamoja na malezi mabovu ya wazazi kwa watoto.

Tamaa za kutaka vitu vya thamani ilhali mtu hana uwezo, makundi ya watoto waliopotoka kimalezi, pamoja na kuiga utamaduni kutoka nchi nyingine kupitia mitandao ya kijamii.

Nadhani hata hivyo, hatua ya busara iliyoko mbele yetu ni kwamba kadri mwenendo huo ninaodiriki kuuita ni ujinga na umekosa busara, sasa sehemu kubwa ya jamii kwa uwiano uleule wa kushamiri taarifa hizi wamekuwa wakali kwelikweli.

Ni jana tu, nilikuwa nafuatilia mjadala bungeni, hata kumsikia mbunge mmoja akija juu na kutaka nguvu za pamoja kutoka serikalini, wao wakiwa sehemu ya timu hiyo wapambane kwa nguvu zote kuhakikisha wanakomesha hayo, tena akitumia kauli iliyonivutia nyendo zinazopingana na imani ya Mungu, vilevile sheria zetu kwa ngazi zote.

Hapo kuna maana vita hivi vishuke mbali kwa ngazi za ustawi wa jamii, kuunda mwenendo wetu kimaisha na mustakabali wa tabia hata kumfanya kila anayethubutu kueleka ng'ambo ya tabia hiyo ajikute yu mkosaji kuanzia mbele ya Mungu, kisheria, na hata tabia zetu za kila siku.Zao la kinachojengwa mahali hapo ni kwamba tabia isiyokubalika mashariki hadi magharibi, kusini hadi kaskazini.

Wenzetu wa Uganda wakaamua kwa amri kali, na kisha wakaelekea kwenye sheria kali huku wahusika wa kidini wakiongea lugha moja.

HABARI KITAIFA

# Serikali, Marekani yaeleza neema ziara ya Makamu wa rais Kamala

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax pamoja na Balozi wa Marekani Nchini, Michael Battle, wamezungumzia fursa zilizotokana na ziara ya Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, likiwamo la kufungua maeneo mapya ya ushirikiano.

Ziara hiyo ambayo ilifanyika kwa siku tatu kuanzia Machi 29, mwaka huu, imetajwa kama sehemu ya kuitangaza Tanzania duniani.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana viongozi hao wametaja mafanikio na vipaumbele ambavyo Marekani imepanga kuisaidia Tanzania kwenye nyanja tofauti ikiwamo elimu, afya na usalama.

Waziri Tax alisema kupitia ziara hiyo, Marekani inatarajia kujenga kiwanda kikubwa Tanzania, ambacho kitakuwa cha pekee barani Afrika cha kuchakata madini aina ya Nikel yanayotumika kutengenezea betri za gari za umeme kwa ajili ya soko nchini humo na duniani ifikapo mwaka 2026.

"Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa na Kampuni ya Life Zone Metals, na kampuni ya TechMet zinazomilikiwa kwa ubia na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Fedha la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (DFC). Kiwanda hiki kitatoa ajira kwa watanzania, na kuchangia katika pato la Taifa," alisema.

Alisema Mkataba wa Msaada wa Maendeleo kati ya Tanzania na Serikali ya Marekani kupitia USAID wa kiasi cha Dola za Marekani bilioni 1.1 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kijamii na kiuchumi ulisainiwa.

"Hati ya Makubaliano kati ya nchi hizi mbili ilisainiwa, kupitia makubaliano hayo, Marekani itatoa ushauri wa kitaalam na kujenga uwezo kwa wataalam kuhusu usimamizi wa bandari za Tanzania, hususan katika upanuzi wa bandari, vifaa vya kisasa na uendelezaji wa Bandari.

"Marekani iliahidi kutoa nyongeza ya Dola za Marekani milioni 1.3 kupitia Shirika la misaada la Marekani USAID kwa ajili ya kusaidia sekta ya afya kuendelea kukabiliana na magonjwa ya mlipuko," alisema.

Waziri Tax alisema Marekani imeahidi kutoa zaidi ya Dola bilioni 1.0 kwa ajili ya kuwawezesha wanawake wa Afrika walio katika sekta ya umma na binafsi kushiriki shughuli za kiuchumi na kijamii.

Pia alisema ahadi nyingine ni kuingia makubaliano na Tanzania yatakayowezesha Marekani kuuza bidhaa za usafirishaji, uchukuzi, teknolojia ya digitali na nishati safi zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 500.

"Marekani kupitia Shirika la Msaada la Marekani USAID kutoa Dola za Marekani 600,000 kwa ajili ya kushirikiana na kampuni za mawasiliano na teknolojia ya sekta binafsi, ili kupanua huduma za nishati safi na kutoa umeme kwa takriban vituo 100 vya afya katika maeneo ya magharibi, kati, na kusini mwa Tanzania," alisema.

Kadhalika alisema mradi huo utawezesha kampuni za mawasiliano ya simu kuimarisha huduma za takwimu na kuwezesha vituo vya afya kutumia mifumo ya kidijitali katika utoaji wa huduma;

Pia alisema itaendelea kuwekeza katika Mpango wa Dharura wa Rais wa Kusaidia UKIMWI (PEPFAR) na Tanzania kunufaika, ambapo Dola milioni 433 kuwekezwa katika kipindi cha miaka miwili ijayo.

Waziri Tax alisema Marekani itaipatia Tanzania Dola milioni moja kwa ajili ya miradi inayolenga kuondoa vikwazo vya uhuru wa kujieleza kwa umma na vyombo vya habari vya Tanzania;

Balozi wa Marekani nchini, Michael Battle alitaja kipaumbele kingine ni kuwekeza katika demokrasia, utawala bora na maendeleo akikumbushia kuwa Machi 29 mwaka huu, Shirika la Marekani la Ushirikiano wa Kimataifa (USAID) na serikali ya Tanzania walitia saini makubaliano ya miaka mitano.

"Chini ya makubaliano hayo, USAID itafanya kazi kwa karibu na serikali ya Tanzania kwa kutoa msaada katika maeneo ya ukuaji, uchumi, afya, elimu, demokrasia na utawala bora.

"Eneo jingine kuimarisha bioanuai na usalama wa chakula, shirika la USAID, linatarajia kutoa shilingi bilioni 19 kuzindua programu ya heshimu bahari ya miaka mitano ya kuimarisha uthabiti wa kiikolojia na tija ya mfumo wa ikolojia yake" alifafanua Balozi

Alisema wanatarajia kuzindua mradi wa kilimo tija watakaotoa Sh. bilioni 37, zitakazosaidia wakulima wa chakula duniani na kuwapatia wale wa kitanzania pembejeo, rasilimali na utaalamu unaohitajika hasa kilimo cha mbogamboga na matunda.

Alisema eneo lingine ni kwenye ukuzaji wa elimu, ushiriki wa vijana na kuwajengea wanawake uwezo wa kiuchumi ambapo mwezi Julai mwaka huu, wanatarajia kuwakutanisha wahitimu 100 wa programu ya mafunzo kwa wajasiriamali wanawake (AWE), kutoka nchi tofauti Afrika.

Pia alisema katika sekta ya afya watasaidia kukuza ushirikiano na kukabiliana na mlipuko wa virusi vya Marburg.

Alisema mkakati uliopo kwenye eneo hilo ni kuendeleza mpango wa dharura wa Rais wa Marekani kupambana na UKIMWI (PEPFAR) ambao mwaka huu, ulisherekea miaka 20 tangia kuanzishwa kwake.

**Imeandaliwa na Romana Mallya na Halfani Chusi**



Baadhi ya Wahariri na wanahabari kutoka katika Jukwaa la wahariri Tanzania (TEF) wakipata Futari kwa pamoja iliyoandaliwa na mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Kampuni ya SICPA Tanzania wakati wa Mkutano wa 12 wa Mwaka wa Kitaaluma wa Wahariri katika iliyofanyika Mkoani Morogoro wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtoto wa Rais apinga nyumba kubomolewa

**Na Mwandishi Wetu**

MTOTO wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Balozi Ali Karume amepinga kuvunjwa kwa nyumba za Maendeleo Kilimani mpango ambao amesema unakwenda kinyume cha uamuzi uliopitishwa na Baraza la Mapinduzi kwamba nyumba hizo zifanyiwe matengenezo ili kulinda historia yake.

Balozi Karume aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari nyumbani kwake, Maisara, Mjini Unguja, kuhusu kumbukumbu ya miaka 51 ya kifo cha Hayati Abeid Amani Karume inayofanyika Aprili 7, kila mwaka.

Alisema kwa mujibu wa sheria na katiba, ardhi ni mali ya serikali lakini serikali inaweza kuchukua ardhi ya mwananchi iwapo katika eneo hilo kunajengwa mradi wa maendeleo wa huduma za jamii na wananchi lazima walipwe fidia na si mradi wa biashara.

Pia alisema kama wananchi wa Kilimani hawataki nyumba zao zivunjwe wanapaswa kupeleka msimamo wao serikalini na si kulalamika mitaani kwa sababu wana haki kwa mujibu wa Katiba na sheria ya kukataa mradi huo.

"Baraza la Mapinduzi chini ya Rais mstaafu Dk. Ali Mohamed Shein, lilipitisha uamuzi kuwa nyumba za Kilimani zifanyiwe matengenezo makubwa na si kuvunjwa baada ya kukumbwa na uchakavu," alisema Balozi Karume.

Alisema bahati mbaya kwa wakati huo serikali haikuwa na fedha za kufanyia matengenezo nyumba hizo, lakini uamuzi huo uliendelea kubaki na kuwa mpango wa siku za baadaye katika kulinda nyumba za maendeleo zilizojengwa na Rais wa Kwanza wa Zanzibar baada ya Mapinduzi ya Januari 12. 1964.

"Katika nyumba hizo mama angu alipata fleti moja na mimi nikapokea taarifa kupitia jirani yetu akaniambia nyumba za Kilimani umesikia zinavunjwa kupisha mradi wa uwekezaji wa nyumba za kisasa lakini hatujui tutahamishiwa wapi?" alihoji Balozi Karume.

Aidha, alisema Baraza la Mapinduzi ndilo lenye uwezo wa kufuta uamuzi wake lakini inashangaza serikali imeamua kuvunja nyumba za kilimani, ili kumpisha mwekezaji ajenge nyumba za makazi ya biashara.

Balozi Karume alisema wakati wa utawala wa Dk Shein, yeye akiwa Waziri wa Ujenzi, Miundombinu na Mawasiliano, alimwagiza kufanya ziara katika nyumba za Kilimani baada ya kupokea malalamiko kuwa nyumba hizo zinakabiliwa na uchakavu na baadhi ya wakaazi wake wanatumia kuni kwa ajili ya kupikia na kusababisha uharibifu zaidi.

"Nilipofanya ukaguzi katika nyumba hizo tuliandika ripoti na kupeleka kwa rais na baadaye suala hilo lilijadiliwa baraza la mapinduzi na kufikia maamuzi nyumba hizo zianze kufanyiwa matengenezo ili kulinda historia yake," alisema Balozi Karume.

Alisema katika nyumba 406, serikali kupitia Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC) wana nyumba 14 na zilizobakia ni mali ya wananchi ambao walipewa kama fidia kupisha mradi wa ujenzi wa nyumba hizo.

Alisema nyumba hizo zimejengwa na rais wa kwanza baada ya mapinduzi januari 1964 ukiwa ni msaada kutoka serikali ya Ujerumani na kila mwananchi ambae nyumba yake ilivunjwa katika eneo hilo alifidiwa nyumba moja kwa ajili ya makazi.

Katibu wa Kamati Maalum, Itikadi na Uenezi wa CCM Zanzibar, Khamis Mbeto, alisema wananchi wa Kilimani ndio waliomuomba Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kuzifanyia matengenezo nyumba hizo kwa madai zinakabiliwa na uchakavu.

"Rais Dk. Mwinyi alifanya ziara ya kuwatembelea wagonjwa katika eneo hilo lakini alipokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa eneo hilo kuwa nyumba hizo zimekabiliwa na uchakavu kabla ya kuja na mradi wa kujenga nyumba mpya na wanaoishi katika nyumba hizo kupisha ujenzi kwa muda na baada kumalizika kukabidhiwa nyumba zao," alisema Mbeto.

"Kama wananchi hawataki kuhama nyumba hizo zitakapokuja kubomoka wasije kuilaumu serikali kwa sababu nia ya serikali ni kuvunja nyumba hizo na kujenga zingine chini ya mradi wa Mwinyi City," alisema.

Wakizungumza katika mkutano wa hadhara wa kujadili ujenzi wa nyumba hizo, walisema hawapo tayari kuondoka katika makazi hayo na serikali kama ina nia ya kuwasaidia kuzifanyia matengenezo na sio kujengwa majengo mapya.

"Nyumba hizi historia yake kubwa tulivunjiwa nyumba na tukapewa fidia za nyumba nashangaa leo tunaambiwa nyumba zinavunjwa alafu tuhamishiwe ng'ambo ya mji," alisema Abdallah Ali.

# Kiwanda bubu chafungiwa kisa takataka za hospitali

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limekifungia kiwanda cha kukusanya na kusaga chupa za plastiki eneo la Kisarawe II wilayani Kigamboni, baada ya kukutwa na taka za hospitali kinyume na taratibu.

Kutokana na hali hiyo, NEMC imetoa siku saba kwa mmiliki wa kiwanda hicho kufika katika ofisi za NEMC kujibu tuhuma za kukutwa na taka hizo.

Kaimu Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria wa NEMC, Thobias Mwesiga, alitoa maelekezo hayo jana baada ya kufanya ukaguzi wa kimazingira na kutembelea na kushuhudia shughuli mbalimbali zinazofanyika kwenye kiwanda hicho kinyume na sheria.

Alisema kwa kuwa wamebaini pia kiwanda hicho hakina vibali, mhusika huyo atachukuliwa hatua za kisheria kwa kutozwa faini kutokana na kukiuka taratibu na ataelekezwa utaratibu namna ya kusajili kiwanda chake kwa mujibu wa sheria.

"Faini itakayotozwa kwa mwenye kiwanda haitakuwa pungufu ya Sh. milioni tano na faini hiyo ni ya fedha ambayo anailipa kwa serikali," alisema Mwesiga.

Pia alisema NEMC imeziagiza hospitali zote nchini kufuata utaratibu wa namna ya kuteketeza taka zinazotokana na shughuli za hospitalini.

"Sheria za mazingira na kanuni zake inazitaka hospitali zote nchini kuwa na mfumo na utaratibu mzuri ndani ya hizo hospitali kuteketeza taka zao wenyewe, kuwa na vifaa ambavyo taka zinazozalishwa katika hospitali hazirudi kwenye mazingira," alisema.

Meneja wa NEMC Kanda ya Mashariki Kusini, Hamad Taimuru, alisema watampa maelekezo mwenye kiwanda pindi atakapofika kwenye ofisi za NEMC ndani ya siku saba na kuanzia sasa wamesimamisha rasmi shughuli zote ambazo zimekuwa zikifanywa kwenye kiwanda hicho mpaka taratibu zote zitakapofuatwa.

"Hii haiwezi kukubalika kwani hata hawa wanaofanya kazi kwenye kiwanda hiki wanafanya kazi pasipokuwa na vifaa maalumu hivyo wanaweza kupata na wao madhara kwenye taka hizo za hospitali, madhara kwa sasa ni mengi," alisema Taimuru.

Pia alisema watahakikisha watembelea katika hospitali kuona takataka zao wanazihifadhi na kuzipeleka wapi na kuonesha uthibitisho unaoonyesha sehemu ambayo wanazipeleka takataka hizo.

Mmiliki wa Kiwanda hicho, Salumu Madongo, alithibitisha kuwa kiwanda chake hakina kibali kutoka NEMC lakini vibali vya kiwanda anavyo, hivyo atafika katika ofisi za NEMC ili kupewa utaratibu na kuweza kupata kibali cha mazingira.

Kuhusu taka za hospitali kukutwa katika kiwanda chake, alisema ni kutokana na wale ambao wanakusanya chupa za plastiki na kuzipeleka pale ndio walipeleka taka hizo zikiwa ndani ya mfuko wa kubebea chupa za plastiki.



Mkurugenzi wa Masoko na Mawasiliano wa kampuni ya GF, Salman Karmali (katikati), akibadilishana nyaraka na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Dk. Venance Mwasse, baada ya kutiliana saini mkataba wa kuwakodisha mitambo ya kuchimbia madini wachimbaji wadogo nchini, wakati wa mkutano wa wachimbaji wadogo wa madini, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Ofisa Mauzo wa kampuni ya GF Trucks & Equipment's Ltd, Peter William. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watanzania watakiwa kutokomeza usonji

**Na Mary Kadoke**

MWENYEKITI wa Taasisi ya Biashara ya Africa-India (AIBO), Indrabhuwan Singh, amewataka Watanzania kuwa na mtazamo chanya kwa watoto wanaoishi na usonji na kuhakikisha kuwa wanakuwa na sauti moja katika kutokomeza dhana potofu inayorudisha nyuma uelewa na malezi bora kwa kundi hilo.

Alitoa wito huo katika kongamano la kuadhimisha Siku ya Uelewa wa Usonji Duniani lililofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, lililobeba kaulimbiu ya 'Thamini Familia na Marafiki Wanaoishi na Ugonjwa wa Usonji'.

Singh alisisitiza umuhimu wa wadau wote kuungana katika kuelimisha umma jinsi ya kuishi na watoto hao na kutafuta njia mbadala wa kutatua changamoto zilizopo, ili kupunguza athari kwa kuimarisha mikakati iliyopo.

"Usonji si ugonjwa. Nadhani ni muda sasa jamii na wadau wakae katika meza moja ili kupambanua matibabu yatakayolenga kupunguza tabia hatarishi na kukuza ujuzi wao. Nina uhakika watoto wote ni sawa kwa sababu Mungu aliwaumba sawa wanatofautiana na mitazamo tu. Yatupasa kubadilisha mitazamo ya malezi kwa watoto," alisema.

Kwa mujibu wa Singh, usonji ni janga linalokuwa kwa kasi na kwamba suala linalofanya kutokuwepo na taarifa na makisio ya ukuaji wake na hivyo kutoa wito kwa wadau kuona haja ya kushikamana na kutafuta mbadala wa kupunguza madhara kwa wahanga.

Naye Mkurugenzi wa Kituo cha Afya cha Imran, Dk. Imran Hassan, alisema mbinu zinazoweza kutatua changamoto wa usonji ni pamoja na kukuza ushirikiano baina ya wadau pamoja na kutoa elimu katika nyanja ya saikolojia.

"Inafurahisha kuona ongezeko la wataalamu wakipambana na kutatua changamoto zinazowakumba watoto wenye usonnji. Hatua hii imekuwa sambamba na kufungua shule maalum zinazojikita kuhudumia kundi hili maalum," alisema Dk. Hassan.

Aliongeza kuwa: "Si dhambi kuiga kwa wale waliofanikiwa. Tusimame kwenye mabega ya wabobezi katika suala hili. Kiuhalisia hatuhitaji kusimama kwenye mabega yao ili tuwe warefu zaidi yao bali kujifunza kutoka kwao."

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Ignasia Mbata, aliiomba serikali kuunga mkono jitihada za kupunguza changamoto zinazolikumba kundi hili hata kwa matembezi ya hisani, ili kuunga mkono wazazi wanaojiona wapweke na kutengwa hasa wanapojifungua watoto wenye changamoto hii.

"Mara nyingi jamii inawatenda watoto wenye usonji wakiamini kuwa hawana haki ya kufurahia haki zao mbalimbali kama watoto wengine. Jamii inatakiwa itambuwe kuwa wao pia ni sehemu ya jamii na ugonjwa huo sio ambukizi wala mama hachangii kwa namna yoyote wakati wa mimba mtoto kuwa changamoto hiyo," alisema.

Usonji ni tatizo linalojitokeza mapema utotoni, mtoto huwa na upungufu kwa kupenda kujitenga na kutotaka kuwa karibu na watu 'impared social interaction'. Mara byingi hupata matatizo ya lugha na shida ya mawasiliano 'impared language and communication skills'.

Makadirio ya kitaifa yanaonesha kuwa mtoto mmoja kati ya 100 ana usonji katika nchi kama Uingereza, Sweden, Japan na Marekani.

# Wanawake wafundwa kufanya utafiti kuhusu wachumba kuepusha migogoro

**Na Joseph Mwendapole,**
MOROGORO

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), umewashauri wanawake wanaotaka kufunga ndoa kufanya utafiti kama mwanamume anayetaka kumwoa hana ndoa nyingine ili kuepuka migogoro inayoweza kuibuka baadaye.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki mkoani Morogoro na Kabidhi Wasihi Mkuu wa RITA, Angela Kemanzi, wakati wa mjadala wa kazi za wakala kwenye mkutano wa 12 wa wanachama wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).

"Mwanamke anawajibika kuchunguza kwanza kama ndoa anayotaka kuingia ni ya kwanza au kuna iliyowahi kufungwa, wenzetu waislamu haina shida kwasababu dini inaruhusu kuoa zaidi ya mke mmoja lakini kwa wakristu mtu akifunga ndoa haruhisiwi kufunga nyingine," alisema Kemanzi.

Alisema RITA imewahi kupata migogoro ya wanaume kufunga ndoa zaidi ya moja na kuongeza kuwa inayotambuliwa ni ndoa ya kwanza na ile ya pili hufutwa.

Wakati huo huo, Kemanzi aliwahamasisha wananchi kuandika wosia na kuchana na dhana potofu kwamba kuandika wosia ni kujichulia kifo.

Alisema wosia unarahisisha kupunguza migogoro mara mtu anapofariki dunia kwa kuwa uzoefu unaonyesha kuwa mirathi zimekuwa zikichukua muda mrefu kukamilika kutokana na migogoro.

"Kuna kesi nyingi za mirathi haziishi unakuta watu wanavutana miaka na miaka kwa mfano tuna kesi ya mirathi tangu mwaka 1998 mpaka leo watu wanavutana tu.

"Na haya yote yanatokea kwasababu mambo hayakuwekwa sawa na marehemu wakati wa uhai wake, iwapo mhusika angeacha wosia unaokubalika kisheria mambo yangekuwa rahisi tu kwasababu ungefuatwa wosia," alisema.

Kwa mujibu wa Kemanzi, kumekuwa na tatizo la baadhi ya wasimamizi wa mirathi kutaka kujiona kama sehemu ya mirathi jambo ambalo limekuwa likichochea migogoro hiyo.

Alisema msimamizi wa mirathi anateuliwa tu kusimamia kuhakikisha wahusika wanapata haki yao lakini kutokana na tamaa ya baadhi yao hutaka kuchukua sehemu ya mirathi husika.

"Kuna watu wanadhani ukiandika wosia unajichulia. Si kweli kwa sababu mbona kuna zaidi ya wosia 1,000 zimesajiliwa kwetu RITA tangu mwaka 2008 lakini ni wosia 96 tu zimekuja kuchukuliwa baada ya wahusika kufariki dunia. Kwa hiyo kuandika wosia si kwamba unajichulia kifo," alisema.

Alisema mbali na RITA mhusika anaweza kuandika wosia na kuutunza kwenye taasisi mbalimbali zikiwemo benki au kwa wanasheria wanaotambulika.

Kuhusu leseni za viongozi wa dini wanaofungisha ndoa, Angela alisema wanalazimika kupata leseni ya kutoa huduma hiyo kwa mujibu wa sheria.

Alisema wanalazimika kufanya hivyo kisheria kwani ndoa inapofikia wakati imeshindikana inakuwa rahisi kwa taratibu za kisheria kufuatwa.



# CCM Arusha wamchagua Sokoine kuwa mjumbe NEC

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha, wamemchagua Namelok Sokoine, kuwa mjumbe wa Halmashauri Kuu ya chama hicho Taifa (NEC), baada ya kuwashinda wagombea wenzake tisa.

Uchaguzi huo ulifanyika juzi katika ukumbi wa mikutano wa CCM mkoani hapa baada ya mwaka jana kufutwa kutokana na kubainika kwa dosari mbalimbali.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo, Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, alimtangaza Namelock kuwa mshindi kwa kupata kura 39 na kumwangusha mpinzani wake wa karibu ambaye ni mfanyabiashara wa madini ya tanzanite, Hussein Gonga aliyepata kura 16.

Pinda alisema wajumbe waliopiga kura walikuwa 67, huku nafasi ya tatu ilishikwa na Daniel Palangyo, alikuwa akitetea nafasi ya NEC kwa kupata kura tano.

Nafasi ya nne ilishikwa na Judith Mollel aliyepata kura tatu, Elibahati Lowassa na David Lemilla waliopata kura mbili na wagombea wengine Novatus Makunga, Prof. Samweli Irira na Abdullazi Mawia hawakupata kura.

Kadhalika, Pinda ambaye ni mlezi wa CCM Mkoa Arusha, aliwataka wajumbe kumpa ushirikiano Namelok, katika kuifanya kazi yake vizuri.

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, Namelok, aliwataka wana CCM kuvunja makundi akisema CCM ni chama kimoja.

Naye Gonga, aliwashukuru viongozi wa chama hicho kwa jinsi walivyoendesha uchaguzi wa wazi na huru na yote aliyotaka kuyafanyia kazi iwapo angeshinda sasa atayapeleka kwa Namelok.

Pia, aliahidi kuwa atashirikiana naye ikiwamo suala la kutengeneza ajira kwa vijana na kinamama ili wajikwamue kiuchumi.

Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Arusha, Zelothe Stephen, aliwataka wana CCM kumpa ushirikiano na kusema kuwa kilichobaki ni kuijenga chama na siyo vinginevyo.



Mkuu wa Idara ya Udhibiti Ubora wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga Bombo, Joseph Nzige (kulia), akitoa mafunzo ya uboreshaji wa mazingira ya mtoa huduma kwa dhana ya maboresho kwa ajili ya ufanisi (5S-KAIZEN) kwa maofisa TEHAMA wa hospitali hiyo, jana. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

# Rufani kupinga faini mifugo kuingia Ngorongoro mwezi ujao

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA.

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha, Mei 10 mwaka huu inatarajia kuanza kusikiliza rufa ni ya kupinga utozaji wa faini ya Sh.100,000 kwa kila ng'ombe mmoja watakaokutwa wameingia ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Katika kesi hiyo waomba rufani ni wakazi wawili wa Ngorongoro ambao wanaiomba Mahakama kuzuia utozaji wa faini ya Sh.100000 kwa kila ng'ombe kwa kuwa ni batili na ni kinyume cha sheria.

Wakazi hao wanadai (NCAA), haina mamlaka ya kutoza faini kwenye sehemu ambazo zimeanzishwa na sheria ya wanyamapori kwa kuwa aliyepewa mamlaka ni Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Hata hivyo wanadai kuwa kutoza faini ya Sh.25,000 kwa kondoo ni batili kwa kuwa ni kinyume cha sheria, pia faini ya Sh.milioni 13 ni kinyume cha sheria kwa kuwa kiwango hicho hakipo kisheria.

Katika kesi hiyo mawakili wa waomba rufaa ni Joseph Oleshangay na Denis Moses na wajibu rufaa ni Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Mkurugenzi wa Wanyamapori na Jamhuri.

# Wazazi waagizwa kuhakiki vyumba wanavyolala watoto

**Na Anjela Mhando,** SIHA

WAZAZI na walezi katika kata za Ngarenairobi, Miti Mirefu pamoja na Induumet wilayani Siha, mkoani Kilimanjaro wameagizwa kuhakiki vyumba wanavyolala watoto nyakati za usiku ili kuwalinda kufanyiwa vitendo vya ukatili.

Agizo hilo limetolewa jana na Mjumbe wa Kampeni ya Shujaa wa Maendeleo Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA), wilayani Siha, mkoani Kilimanjaro, Emanueli Shenzua, baada ya tukio la watoto wawili wa darasa la nne na la saba katika Shule ya Msingi Mwangaza kunajisiwa na watu wasiojulikana walipofungua mlango na kuingia ndani nyakati za usiku.

Akizungumza na wanafunzi wa shule hiyo pamoja na walimu, aliwataka wazazi na walezi kuhakikisha milango inafungwa kwa komeo badala ya misumari ambayo inafunguka kwa urahisi ili kuwakinga watoto kufanyiwa ukatili wa kijinsia.


"Nyumba nyingine kwenye hizi kata zimejengwa kwa kutumia mbao na mabanzi na milango yake inafungwa kwa misumari hivyo, inatoa urahisi kufungua ndiyo sababu nimeagiza waweke komea.

"Wanafunzi hawa walifanyiwa ukatili ukiangalia milango ilikuwa imefungwa kwa ndani na msumari na kutoa nafasi kwa watu wasiojulikana kufungua milango na kuwatoa ndani watoto hao na kwenda kuwafanyia unyama na kisha kuwarudisha ndani," alisema.

Katibu wa Siasa na Uenezi wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Wilaya ya Siha, Robart Mirisho, aliwataka wanafunzi kusali kwa imani zao kwa kuwa matukio hayo yanaripotiwa sehemu mbalimbali.

"Tujifunze kusali wakati wa kulala na kuamka asubuhi unamwambia Mungu ninatoka sasa kuelekea shuleni unifunike na ulinzi wako kwa kuwa hakuna kinachoshindikana,"alisema.

Hata hivyo, Katibu wa SMAUJATA, wilayani humo, Bahati Chume, alisema wataendelea kutoa elimu ya ukatili katika shule zote za msingi na sekondari ili wanafunzi wakue katika afya njema na taifa liweze kusonga mbele.



# Miaka miwili ya Samia shule 242 zajengwa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKURUGENZI wa Elimu na Utawala Ofisi ya Rais TAMISEMI, Vicent Kayombo amesema katika kipindi cha miaka miwili serikali imejenga shule 242 kwa lengo la kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani.

Amesema kati ya idadi hiyo shule 232 ni za kata, 10 ni shule maalumu kwa ajili ya wasichana zote zikiwa na thamani ya Sh.bilioni 143.

Aliyasema hayo wakati wa mdahalo wa kufunga mkutano wa tisa wa maofisa elimu mikoa na halmashauri (REDEOA) uliofanyika jana jijini Mwanza.

Kayombo alisema kati ya idadi hiyo, shule 158 za kata tayari zimepokea wanfunzi wa kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2023 na shule 10 za wasichana kitaifa nazo tayari zimepokea wanafunzi wa kidato cha kwanza na wanaendelea na masomo.

Kayombo alisema kuwa shule hizo 10 za wasichana zinatarajia kupokea wanafunzi wa kidato cha tano kwa mwaka wa masomo 2023 na tayari serikali imetenga Sh.bilioni 70 kutoka kwa wafadhili kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kidato cha tano katika shule hizo.

"Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 tayari serikali imetenga Sh.bilioni 187 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za sekondari 184 kwenye kila wilaya, hivyo maofisa elimu kazi yenu kwa sasa ni kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora kupitia miundombinu inayoendelea kuwekwa na serikali," alisisitiza.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Pulina Nkwama alisema licha ya serikali kuendelea kuboresha na kuongeza miundombinu tayari imetoa ajira kwa walimu 24,343, huku walimu 161,432 wakipandishwa madaraja sambamba na walimu 20,032 wamebadilishiwa muundo wa kiutumishi baada ya kuongeza elimu zao.

Waziri wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Angellah Kairuki, aliwataka maofisa hayo kurudi katika maeneo yao na kuhakikisha wanasimamia na walinda mila, desturi na tamaduni za Watanzania kwa kuhakikisha wanafunzi wanapata maadili wanapokuwapo shuleni.

Kadhalika, aliwataka kuendelea kusimamia na kufuatilia stahiki za walimu ili kuwapa motisha katika shughuli zao za ufundishaji pamoja na kulinda mali za serikali ikiwa ni pamoja na kutunza vitendea kazi vikiwemo vishikwambi walivyopatiwa walimu ili viendelee kuwasaidia katika shughuli za uelimishaji.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki (kushoto) akipokea tuzo kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Maofisa Elimu Mikoa na Wilaya Tanzania (REDEOA), Mwalimu Germana Mung'aho iliyotewa na umoja huo kwa lengo la kutambua mchango wa Rais katika kuboresha sekta ya elimu nchini, wakati wa kufunga mkutano mkuu wa tisa wa REDEOA jijini Mwanza juzi. **PICHA: VITUS AUDAX.**

# KACU yatangaza kiama kwa watoroshaji tumbaku

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) mkoani Shinyanga, kimewatangazia kiama wakulima watakaobainika kutorosha mitumba ya zao la tumbaku wakati wa masoko na kwenda kuuza nje ya wilaya.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mwenyekiti wa chama hicho, Hamisi Majogolo wakati akizungumza na wakulima wa zao hilo kutoka vyama vya msingi 10 vya Kata ya Bukomela na Uyogo Halmashauri ya Ushetu na kuwakumbusha namna ya kupanga madaraja pamoja na ufungaji wa mitumba yake.

Alisema katika kipindi hiki zao hilo limepanda bei kutoka kilo moja kuuzwa Sh.3,862 kwa mwaka jana hadi Sh. Sh.4,682 kwa mwaka huu.

Hivyo aliwataka wakulima kuendelea kuwa waadilifu na kuacha tabia za kuharibu zao hilo kwa kulichanganya na uchafu pamoja na kuuza nje ya wilaya hali inayofifisha vyama hivyo.

Akizungumza kwa niamba ya wenyeviti wa vyama vya msingi (AMCOS), Mwenyekiti wa Ngokolo, Ntano Sambi alisema, atahakikisha anawasimamia wakulima wake katika kupanga madaraja na kufunga vema, ili kutochanganya safi na chafu.

Mteuzi Mfawidhi kutoka Bodi ya Tumbaku Mkoa wa Kahama, Lucas Zenza alisema ufungaji wa madaraja unapofanyika mapema tumbaku inakuwa bora na uzito unaohitajika katika masoko.

Mmoja wa wakulima wa zao hilo, Amos Stephan alisema katika msimu huu pembejeo za kukuzia na kupandia zilichelewa kuwafikia hali ambayo iliwatia hofu ya kufikia malengo ya kuzalisha kilo milioni 17.

# Taasisi yafuturisha wafungwa, mahabusu Gereza la Kahama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAFUNGWA pamoja na mahabusu waliopo katika Gereza la Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga wamepewa futari na Taasisi ya Ibadhi Kahama Foundation kwa kushirikiana na Kamati ya Masjid Al-Wahaab.

Mbali na kufuturisha, taasisi hiyo ilikabidhi mchele kilo 200, maharage kilo 100, sukari kilo 45, mafuta ya kula lita 30, chumvi boksi nne, tambi boksi moja,tende boksi mbili pamoja na sabuni boksi tano kwa ajili ya kufulia mavazi yao na kuogea ili kuwa nadhifu muda wote wa funga zao. Akikabidhi msaada huo kwa Mkuu wa Gereza, Hamza Abdallah, Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Issa Al-Habsy alisema wafungwa na mahubusu wana haki ya kusaidiwa katika funga zao kama yalivyo makundi mengine ili kutimiza moja ya nguzo tano za dini ya kislamu.

Alisema utaratibu wa kusaidia makundi mbalimbali yasiyojiweza ili kufanikisha funga zao ikiwa ni sehemu jukumu la kila muumini wa dini hiyo na kuwaomba watu wengine wenye uwezo kujitokeza na kusaidia makundi yenye uhitaji.

"Futari tuliyotoa kwa wenzetu inathamni ya Sh. milioni 1.5 lengo letu ni kuhakikisha hawapati vikwazo vyovyote katika funga zao mpaka wanamaliza,"alisema Issa.

Akipokea msaada huo Mkuu wa Gereza la Wilaya ya Kahama alisema gereza hilo lina waumini wengi wa dini ya kislamu na wote wamefunga na wanahitaji msaada wa futari ili kufanikisha funga yao kama yalivyo makundi mengine katika jamii.

Aidha, alisema atahakikisha msaada huo unatumika katika matumizi yaliyopangwa na kuwanufaisha wafungwa na mahabusu wote waliofunga na kuwasihi watu wengine kujitokeza kutoa msaada kwa wafungwa.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU

## HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA SERIKALI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2023/2024



**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (MB)**
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKU
(SERS, BUNGE NA URATIBU)



**MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO (MB)**
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKU
(KAZI, VIJANA, NA WENYE ULEMAVU)



**MHE. UMMY NDERIANANGA (MB)**
NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKU
(SERS, BUNGE NA URATIBU)



**MHE. PATROBAS PASCHAL KATAMBI (MB)**
NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKU
(KAZI, VIJANA, NA WENYE ULEMAVU)





**MHE. JIM JAMES YONAZ**
KATIBU MKUU, OFISI YA WAZIRI MKU
(SERA, BUNGE NA URATIBU)

**MHE. KASSIM M. MAJALIWA (MB)**
WAZIRI MKUU



**MHE. PROF. JAMAL ADAM KATUNDU**
**KATIBU MKUU, OFISI YA WAZIRI MKUU**
(KAZI, VIJANA, NA WENYE ULEMAVU)





# HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA SERIKALI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2023/2024

**UTANGULIZI**

***Shukrani***

**1.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge za Utawala, Katiba na Sheria; Afya na Masuala ya UKIMWI; Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na Bajeti zilizochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge, sasa naliomba Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2022/2023 na Mwelekeo wa Kazi zake kwa mwaka 2023/2024. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2023/2024.

**2.** ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa fadhila zake ambazo zimetuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2022/2023 na mwelekeo wake kwa mwaka 2023/2024 tukiwa wenye afya njema.

**3.** ***Mheshimiwa Spika***, itakumbukwa kuwa huu ni Mkutano wa 11 wa Bunge la 12 ambao ni mahsusi kwa ajili ya mjadala wa bajeti. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuitumie vyema fursa hii kutoa maoni na ushauri ili kuisaidia Serikali kuimarisha utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/2024. Napenda kuwahakikishia kuwa Serikali itapokea maoni na ushauri wenu na kuyafanyia kazi kwa maslahi mapana ya wananchi.

***Salamu za Pole***

**4.** ***Mheshimiwa Spika***, nchi yetu kwa nyakati tofauti imekumbwa na maafa na matukio mbalimbali yaliyosababisha athari mbalimbali zikiwemo vifo, majeruhi, na uharibifu wa mali na mazingira. Nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa na mali zao katika maafa. Aidha, ninamwomba Mwenyezi Mungu awajalie majeruhi wote uponyaji wa haraka na aendelee kuwapumzisha kwa amani wale waliopoteza maisha.

**Salamu za Pongezi**

**5.** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuongoza vyema na kupata maendeleo na mafanikio makubwa katika kipindi kifupi cha miaka miwili ya uongozi wake. Mafanikio hayo ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu na huduma za afya, maji, elimu, umeme na uchukuzi, kuboresha hali ya chakula na lishe na kuimarisha hali ya kisiasa nchini na mahusiano ya kimataifa.

**6.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutokana na uongozi wao makini na jitihada zao katika kuhakikisha Taifa letu linapata maendeleo.

**7.** ***Mheshimiwa Spika***, hivi karibuni, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya teuzi na mabadiliko ya baadhi ya watendaji wakuu wa taasisi na viongozi wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mabadiliko hayo, yamelenga kuimarisha utendaji kazi Serikalini ikiwa ni pamoja na utoaji huduma bora na kushughulikia kero mbalimbali za wananchi.

**8.** ***Mheshimiwa Spika***, ninawapongeza viongozi na watendaji wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kushika nyadhifa mbalimbali. Kipekee, niwapongeze Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu; Mheshimiwa George Boniface Simbachawene Mbunge wa Kibakwe na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega Mbunge wa Mkuranga na Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma almaarufu Mwana FA, Mbunge wa Jimbo la Muheza kwa kuteuliwa kushika nafasi ya Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Ninawatakia kila la kheri viongozi wote walioteuliwa katika utekelezaji wa majukumu yao mapya.

**9.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, nitumie fursa hii kuwasisitiza wateuliwa wote kuzingatia maelekezo mbalimbali ya Mheshimiwa Rais yakiwemo aliyatoa kwenye semina ya viongozi iliyofanyika hivi karibuni, Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 pamoja na mipango ya kitaifa na kimataifa katika utekelezaji wa majukumu yao. Aidha, natoa rai kwa viongozi hao kuhakikisha wanatanguliza mbele maslahi ya Taifa na kuwahudumia wananchi ipasavyo.

**10.** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge hili kwa hekima na umahiri mkubwa. Nimpongeze pia Mheshimiwa Naibu Spika kwa namna ambavyo ameendelea kusimamia shughuli za Bunge kwa uwezo mkubwa. Waheshimiwa Wabunge wenzangu hakika mtakubaliana nami kuwa Viongozi hawa ni makini sana na wameonesha ukomavu mkubwa wa kisiasa wakati wote wakiendesha vikao vya Bunge hili. Nitoe wito kwetu sote tuendelee kuwapa ushirikiano ili waendelee kuliongoza vema Bunge letu na kulifanya liendelee kuheshimika ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa *Dkt.* Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria; Mheshimiwa Stansilaus Nyongo, Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI; Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalumu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na wajumbe wote wa kamati hizo kwa michango yao iliyosaidia kuboresha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninatambua ulifanya mabadiliko ya Wenyeviti na Wajumbe wa kamati za kudumu za Bunge. Nitumie fursa hii kuwapongeza sana wote walioteuliwa na kuwatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao. Vilevile, ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge lako tukufu kwa ushauri walioutoa wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Maoni na ushauri wao utazingatiwa vilivyo wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako Tukufu lilifanya uchaguzi wa wenyeviti wa Bunge ambao watakusaidia kuongoza vikao vya Bunge. Niwapongeze Mheshimiwa Najma Murtaza Giga Mbunge wa Viti Maaalum na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile Mbunge wa Mufindi Kusini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kuchaguliwa kuwa wenyeviti wa Bunge. Nawapongeza sana na kuwatakia majukumu mema ya kuliongoza Bunge.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri; Katibu Mkuu Kiongozi; Wakuu wa Mikoa; Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Makatibu Wakuu; Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Naibu Makatibu Wakuu; na Wakuu wa Wilaya, Idara, Mashirika, Wakala na Taasisi zote za Serikali kwa ushirikiano mkubwa mnaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kipekee, niwapongeze na kuwashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na taasisi zake kwa kufanya kazi kwa weledi, utaalamu na umahiri mkubwa na hivyo, kuwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**15.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya pekee, nawashukuru Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu); Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, Mbunge wa Kasulu Mjini na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Paschal Patrobas Katambi, Mbunge wa Shinyanga Mjini na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) na Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalumu na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

**16.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, nawashukuru sana Dkt. Jim James Yonazi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu); Prof. Jamal Adam Katundu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo; Wakuu wa taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu; Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu na wafanyakazi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia wakati nikitekeleza majukumu yangu. Aidha, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru Mheshimiwa George Boniface Simbachawene Mbunge wa Kibakwe na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dkt. John Antony Kiang'u Jingu, Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu na Bwana Kaspar Kaspar Mmuya, Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ushirikiano walionipa wakati wakiwa Waziri wa Nchi, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu mtawalia katika Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu). Ahsanteni na Hongereni Sana!

**17.** ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda pia kuzishukuru sekta binafsi, nchi rafiki, washirika wa maendeleo, taasisi na mashirika ya kimataifa na madhehebu ya dini kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za kuleta maendeleo. Serikali inatambua na kuthamini michango yenu hususan katika utekelezaji wa afua muhimu kwa kutoa misaada, mikopo nafuu na wakati mwingine utaalamu, kitendo ambacho kimekuwa chachu ya kuharakisha maendeleo ya nchi yetu.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya utangulizi huo, naomba kuwasilisha makadirio ya bajeti ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa vipaumbele vilivyobainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; maelekezo ya nyaraka za kisera za kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050, Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/2024.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2022/2023**

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo itakayoimarisha uchumi wa nchi na maendeleo ya watu. Hadi kufikia Januari, 2023 zimetolewa takribani Shilingi trilioni 8.64 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya reli, barabara, viwanja vya ndege, huduma za jamii na nishati. Utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:

**Mosi: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR)**

Serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 762.99 kutekeleza mradi huo ambapo kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) utekelezaji umefikia asilimia 97.91; kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) asilimia 92.23; kipande cha Mwanza - Isaka (km 341) asilimia 25.75; kipande cha Makutupora - Tabora (km 371) asilimia 4.59; na kuanza kwa ujenzi wa kipande cha Tabora - Isaka (km 165) na Tabora – Kigoma (Km 506).

**Pili: Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (MW 2,115)**

Serikali imetoa takribani Shilingi bilioni 869.93 kwa ajili utekelezaji wa mradi huu ambao umefikia asilimia 83. Zoezi la ujazaji maji katika bwawa lilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Desemba 2022. Hadi Februari, 2023 kiwango cha maji kimefikia mita 134.39 kutoka usawa wa Bahari ikilinganishwa na kiwango cha mita 163 kinachohitajika ili kuanza uzalishaji.

**Tatu:Uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania**

Utekelezaji wa mradi huu umegharimu takribani Shilingi bilioni 20.52. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na kulipa sehemu ya gharama za ununuzi wa ndege tano ambapo kati ya hizo, ndege moja ni aina ya Boeing 767-300F ya mizigo, ndege mbili aina ya Boeing 737-9, ndege moja aina ya Boeing 787-8 Dreamliner na ndege moja aina ya De Havilland Dash 8-Q400. Ndege nne kati ya hizo zinatarajiwa kuwasili nchini kabla ya Novemba, 2023 na ndege moja ya mizigo inatazamiwa kuwasili nchini hivi karibuni. Kuwasili kwa ndege hizo kutasaidia Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kutanua mtandao wa safari za ndani na nje ya nchi na hivyo kuchochea ukuaji wa sekta nyingine za uchumi kama utalii, biashara na kilimo.

**Nne: Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) lenye urefu wa km 1,443**

Takribani shilingi bilioni 30.39 zimetolewa ili kulipa fidia wananchi 7,486 kati ya 9,122 wanaopisha eneo la mkuza wa bomba; na Serikali imeendelea kulipa hisa za umiliki katika Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki hadi kufikia dola za Marekani milioni 131.0. Aidha, tayari kibali cha kuanza ujenzi wa Bomba la Mafuta kimetolewa Januari 2023. Vilevile, ujenzi wa karakana ya kuweka mfumo wa kupasha joto mabomba katika kijiji cha Sojo, Nzega Tabora umefikia asilimia 49.

**Tano: Mradi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi**

Takribani shilingi bilioni 39.84 zimetolewa ili kuendelea na ujenzi wa kiwanda ambao umefikia asilimia 75. Aidha, hekta 219 zimepandwa miwa na kufanya ukubwa wa eneo lililopandwa miwa kufikia hekta 2,974 sawa na asilimia 83 ya lengo la kupanda hekta 3,600. Kiwanda hicho kinatarajiwa kuongeza uzalishaji wa tani 50,000 za sukari kwa mwaka pindi kitakapoanza uzalishaji na hivyo kupunguza mahitaji ya kuagiza sukari nje ya nchi.

**Sita: Mradi wa Daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza)**

Takribani shilingi bilioni 93.09 zimetolewa kuendelea na ujenzi wa daraja hili ambao umefikia asilimia 63. Kukamilika kwa Daraja hili kutapunguza muda wa Wananchi kuvuka eneo la Kigongo – Busisi kutoka takribani masaa 2 mpaka dakika 4 kwa kutumia usafiri wa Gari na dakika 10 kwa watembea kwa Miguu. Aidha, daraja hili litakuwa na uwezo wa kupitisha magari ya aina yote wakati wote na kubeba uzito wa hadi tani 160.

**Saba: Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Viwanja vya Ndege**

Serikali ilitoa takribani shilingi bilioni 77.23 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ambapo utekelezaji umefikia asilimia 10.2. Kazi nyingine ni kukamilika kwa upanuzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na kufungwa kwa mfumo wa kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma; kukamilika kwa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Geita; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege vya Songea kwa asilimia 98, Iringa asilimia 42 na Musoma asilimia 43.

**HALI YA UCHUMI**

**20.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha takribani mwaka mmoja sasa, Dunia imekumbwa na msukosuko wa kiuchumi kutokana na vita inayoendelea baina ya nchi za Ukraine na Urusi. Vita hiyo ilianza wakati uchumi wa dunia ukiwa bado haujatengemaa kutoka kwenye madhara ya janga la UVIKO – 19. Kwa msingi huo, tumeshuhudia uchumi wa mataifa makubwa hususan katika bara la Ulaya ukiyumba na gharama za maisha kuongezeka kutokana na mfumuko wa bei za nishati na chakula duniani.

**21.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Duniani ya Januari, 2023, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imepungua kutoka asilimia 6.2 mwaka 2021 hadi asilimia 3.4 mwaka 2022. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajia kupungua na kufikia asilimia 2.9 mwaka 2023. Vilevile, kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea imepungua na kufikia asilimia 2.7 mwaka 2022 kutoka asilimia 5.4 mwaka 2021 na inatarajiwa kupungua na kufikia asilimia 1.2 mwaka 2023.

**22.** ***Mheshimiwa Spika***, uchumi wa nchi zinazoendelea na zinazoibuka kiuchumi ulipungua na kufikia asilimia 3.9 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2021. Aidha, ukuaji wa uchumi katika nchi zinazoendelea na zinazoibuka kiuchumi barani Asia, ikijumuisha China na India ulipungua na kufikia asilimia 4.3 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 7.4 mwaka 2021. Kwa upande wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji wa uchumi ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2021.

**23.** ***Mheshimiwa Spika***, kiwango cha wastani wa ukuaji wa Pato la Taifa kwa kipindi cha mwaka 2022 kwa nchi nyingi za ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ni asilimia 4.0 ikilinganishwa na wastani wa ukuaji wa asilimia 4.2 mwaka 2021. Aidha, wastani wa ukuaji wa uchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa ni asilimia 5.6 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2021. Hali hii imesababishwa na kupungua kwa uzalishaji na shughuli za kiuchumi katika nchi husika kwa mwaka 2020 kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo: utekelezaji wa masharti yaliyowekwa kuzuia maambukizi ya UVIKO-19 kama kufunga mipaka, kusitisha safari za ndege za kimataifa, kusitisha baadhi ya shughuli za kiuchumi zinazohusisha mikusanyiko na kuzuia watu kutoka nje.

**24.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na kusuasua kwa ukuaji wa uchumi wa dunia na mataifa ya Afrika hususan nchi za ukanda wa Jangwa la Sahara, Jumuiya za SADC na Afrika Mashariki, hali ya ukuaji wa uchumi kwa nchi yetu kwa kipindi cha robo ya kwanza hadi ya tatu ya mwaka 2022 imeimairika ikilinganishwa na mwaka 2021. Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2022, Uchumi wa Taifa ulikua kwa wastani wa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 4.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji chanya wa uchumi ulichangiwa na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ikiwemo: uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, barabara, reli na viwanja vya ndege; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan dhahabu na makaa ya mawe, kuongezeka kwa mikopo katika sekta binafsi ambayo imechochea shughuli za kiuchumi na kuongezeka kwa shughuli za utalii.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** ukuaji wa uchumi wa Tanzania kwa mwaka 2022 unatarajiwa kupungua hadi kufikia wastani wa asilimia 4.7 kutoka ukuaji wa asilimia 4.9 mwaka 2021 na kuongezeka hadi kufikia asilimia 5.3 mwaka 2023. Maoteo ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania yamezingatia hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kukabiliana na athari zitokanazo na vita kati ya Ukraine na Urusi ikiwemo: kuchochea uzalishaji katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na madini; uimarishaji wa miundombinu ya barabara mijini na vijijini, nishati na maji; uboreshaji wa huduma za jamii; kuendelea na utekelezaji wa miradi inayochachua shughuli za kiuchumi ikiwemo reli, upanuzi wa bandari, usambazaji umeme vijijini; na uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji. Hata hivyo, kulingana na utabiri wa hali ya hewa ambao umebainisha uwezekano wa kuwa na mvua chini ya wastani, hali hiyo inaweza kuathiri uzalishaji katika sekta ya kilimo, upatikanaji wa nishati ya umeme, na maji na hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi.

**Mfumuko wa Bei**

**26.** ***Mheshimiwa Spika***, madhara ya vita vya Urusi na Ukraine yamesababisha kuongezeka kwa kasi ya kupanda bei ya mafuta duniani na hivyo kuchangia kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usafirishaji na kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali.

**27.** ***Mheshimiwa Spika***, mfumuko wa bei nchini kwa mwaka 2022 ulifikia wastani wa asilimia 4.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2021. Hata hivyo, kiwango hiki kipo ndani ya malengo ya kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0 na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi wa kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Sababu zilizochangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei katika kipindi husika ni pamoja na: kupanda kwa bei za bidhaa ikiwemo mafuta ya kula, mbolea na petroli kufuatia kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia uliotokana na athari za vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine; na kupungua kwa upatikanaji wa mazao ya chakula nchini na nchi jirani kulikosababishwa na mabadiliko ya tabianchi hususan maeneo yanayotegemea mvua za vuli.

**28.** ***Mheshimiwa Spika***, mfumuko wa bei nchini unatarajiwa kuendelea kuwa tulivu na kubaki katika wigo wa tarakimu moja na ndani ya vigezo vya mtangamano wa kiuchumi vya kikanda kutokana na hatua zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ikiwemo: kuongeza bajeti katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na nishati ili kuchochea uzalishaji wa ndani na kupunguza nakisi ya urari wa biashara; usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti; utulivu wa thamani ya shilingi na kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini.

**UWEKEZAJI**

**29.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuimarisha uwekezaji hapa nchini. Katika mwaka 2022/2023, Serikali kupitia Bunge lako tukufu imetunga Sheria ya Uwekezaji Tanzania Namba 10 ya Mwaka 2022 ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kuweka mazingira bora ya uwekezaji. Aidha, Serikali imeendelea kuratibu mradi wa maandalizi ya Kongani ya Viwanda ya Kwala yenye ukubwa wa ekari 2,500 ambapo kiasi cha Dola za Kimarekani Bilioni tatu zinatarajiwa kuwekezwa. Mradi huu unatarajiwa kuzalisha jumla ya ajira za moja kwa moja 100,000, ajira zisizo za moja kwa moja 300,000 na bidhaa za takriban Dola za Marekani bilioni 6 kwa mwaka. Vilevile, Serikali inaendelea kuratibu maandalizi ya kongani na maeneo mengine ya kiuchumi ikiwemo, Kongani ya Magu na Misungwi pamoja na Eneo Maalumu la Kiuchumi Nala.

**30.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kutekeleza programu zinazolenga kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini. Programu hizi zinajumuisha kuboresha mazingira ya uondoshaji wa shehena bandarini ambapo Serikali inajenga Mfumo wa Pamoja wa Kielektroniki wa Uondoshwaji wa Shehena Bandarini. Aidha, Serikali imekamilisha mkakati wa uendeshaji wa mfumo huo na Mfumo wa Utoaji wa Vibali na Leseni za Mazao utakaounganishwa na Mfumo wa Pamoja wa Kielektroniki wa Uondoshwaji wa Shehena Bandarini kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa vibali na leseni za mazao.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki katika miradi na programu za maendeleo ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika kukuza uchumi. Aidha, Serikali itaendelea kufanya mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali inayohusu uwekezaji kwa lengo la kuweka mazingira bora ya uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na kukuza ushiriki wa Watanzania katika miradi ya kimkakati ya uwekezaji.

**SIASA**

**Hali ya Siasa na Kuimarika kwa Demokrasia Nchini**

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla hali ya siasa nchini ni tulivu na Vyama vya Siasa vinaendelea kutekeleza majukumu yao ikiwemo kufanya mikutano ya hadhara katika maeneo





mbalimbali nchini. Aidha, Serikali imeendelea kuratibu vikao vya maridhiano ya kisiasa na Vyama vya Siasa nchini ili kuleta umoja, amani na utulivu katika nchi yetu ambao umekuwa ni utamaduni wetu tangu Uhuru. Kipekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kunakuwepo na mtangamano wa kisiasa nchini unaojumuisha siasa safi, za kiustaarabu na zinazoheshimu mawazo ya kila mmoja wetu.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kukuza na kuimarisha demokrasia ya vyama vingi nchini, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imeratibu shughuli za Vyama vya Siasa kwa kuhakikisha kunakuwepo na fursa sawa katika shughuli za siasa nchini. Katika mwaka 2022/2023, Serikali imetoa ruzuku jumla ya shilingi bilioni 17.5 kwa Vyama vya Siasa sita vyenye sifa ya kupata ruzuku. Vyama hivyo ni NCCR-Mageuzi, CCM, CHADEMA, DP, CUF na ACT-Wazalendo. Hatua hii, imesaidia kuendeleza na kuimarisha uendeshaji wa shughuli za Vyama vya Siasa na demokrasia nchini.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, chaguzi ndogo za ubunge ziliendeshwa katika jimbo la Amani Zanzibar na Udiwani katika kata 12 Tanzania Bara. Chaguzi hizo zimefanyika kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo vifo na baadhi ya Waheshimiwa Madiwani kukosa sifa za kuendelea na nyadhifa hizo. Nitumie fursa hii kuvishukuru vyama vyote vilivyoshiriki chaguzi hizo kwani vimeonesha ukomavu mkubwa wa kisiasa. Kipekee nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa ushindi wa Jimbo la Amani pamoja na viti 12 vya udiwani katika chaguzi hizo.

**35.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, shughuli za maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 pamoja na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka 2024 zitaendelea. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kulifanyia maboresho Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; kuboresha mifumo ya menejimenti ya uchaguzi; kuendelea na mchakato wa marekebisho ya sheria za uchaguzi; kuandaa Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani; na kutoa elimu ya Mpiga kura kwa wananchi. Nitumie fursa hii kuwaomba Viongozi wa Vyama vya Siasa kuhamasisha Wanachama na Watanzania wote wenye sifa kujiandikisha kwenye Daftari hilo na kupata kitambulisho halali cha mpiga kura pale zoezi hilo litakapoanza rasmi.

**BUNGE**

**36.** ***Mheshimiwa* Spika,** katika mwaka 2022/2023, Ofisi ya Bunge imeendesha Mikutano Mitatu ya Bunge na Mikutano mitatu ya Kamati za Kudumu za Bunge. Katika kipindi hicho, jumla ya Maswali ya Msingi 460 pamoja na ya nyongeza 1,426 yaliulizwa Bungeni na kujibiwa na Serikali.

**37.** ***Mheshimiwa* Spika,** Bunge pia lilijadili na kupitisha miswada saba na maazimio mawili ya Kimataifa yanayotokana na Kamati za Kudumu za Bunge na hatimaye kuwasilishwa Serikalini kwa utekelezaji. Vilevile, Kamati za Kudumu za Bunge zilifanya uchambuzi wa Miswada ya Sheria, Sheria ndogo, Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali na ufuatiliaji wa utekelezaji wa afua za UKIMWI.

**38.** ***Mheshimiwa* Spika,** katika mwaka 2023/2024, Ofisi ya Bunge itaendelea kusimamia shughuli za mikutano minne ya Bunge na mikutano minne ya Kamati za Kudumu za Bunge. Kuratibu ushiriki wa Wabunge katika Mikutano ya Kimataifa ikiwemo Bunge la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bunge la Umoja wa Afrika na Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Aidha, Ukumbi wa Bunge utaendelea kuimarishwa pamoja na kukarabati Jengo la kumbi za Bunge na majengo ya Ofisi.

**MAHAKAMA**

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni azma ya Serikali ya awamu ya sita kuhakikisha haki inapatikana kwa wananchi wote bila kujali hadhi ya mtu, uchumi wala kabila. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imeendelea kufanya maboresho mbalimbali ya kiutendaji pamoja na ujenzi wa miundombinu muhimu ya mahakama kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji wa mahakama na kuimarisha mifumo ya utoaji haki.

**40.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Serikali imekamilisha miradi ya ujenzi wa Mahakama tatu za hakimu mkazi katika Mikoa ya Lindi, Songwe na Katavi. Aidha, ujenzi wa Mahakama za Wilaya 28 katika Wilaya za Same, Mwanga, Tandahimba, Nanyumbu, Namtumbo, Mvomero, Gairo, Ngara, Kilombero, Mkinga, Kakonko, Buhigwe, Uvinza, Butiama, Rorya, Itilima, Busega, Mbogwe, Nyang'hwale, Kyerwa, Misenyi, Tanganyika, Kaliua, Manyoni, Bunda, Kilindi, Rungwe na Sikonge umekamilika. Vilevile, ujenzi wa mahakama ya mwanzo katika Wilaya ya Kilindi eneo la Kimbe na ukarabati wa Mahakama Kuu ya Tabora pamoja na Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi umekamilika.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa Mahakama nne za Wilaya za Ulanga, Ubungo, Liwale na Kwimba pamoja na Mahakama za Mwanzo saba za Kinesi, Mahenge, Luilo, Newala, Usevya, Nyakibimbili na Kabanga. Kwa upande mwingine, inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la makao makuu Jijini Dodoma, nyumba za majaji na ukarabati wa jengo la zamani la makao makuu Dodoma na jengo la mahakama Wilaya ya Maswa.

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha mifumo ya utoaji haki, Serikali imeongeza majaji wa mahakama ya rufaa kutoka 16 hadi 24 na wa mahakama kuu kutoka 78 hadi 98. Vilevile, idadi ya mahakimu iliongezeka kutoka mahakimu 245 hadi 293.

**43.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Mahakama imesikiliza na kukamilisha mashauri 134,989. Ufanisi huu umechangiwa na ongezeko la watendaji katika mahakama, kuendesha mashauri na mikutano kwa njia ya mtandao na kukamilika kwa miundombinu muhimu ya Mahakama.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu kwa lengo la kusogeza huduma za Mahakama karibu na wananchi ili huduma hizo zipatikane kwa wakati na gharama nafuu.

**SEKTA ZA UZALISHAJI**

**Kilimo**

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika sekta ya kilimo ili kuinua Pato la Taifa na la mtu mmoja mmoja. Aidha, hatua mbalimbali zenye lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara zimeendelea kuchukuliwa. Hatua hizo ni pamoja na: kuwezesha wakulima kupata mbegu bora zinazoendana na hali ya hewa nchini; kutoa ruzuku ya pembejeo hususan mbolea na mbegu; kuwezesha upatikanaji wa teknolojia mpya na zana za kisasa; kuimarisha huduma za ugani; kuongeza eneo la umwagiliaji kwa kuanzisha skimu mpya na kukarabati skimu za umwagiliaji zilizopo; na upatikanaji wa masoko ya mazao ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha wakulima wananufaika na mauzo ya mazao.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imesaini Mikataba 31 yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 284.14 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji. Mikataba hiyo inahusu ujenzi wa mabwawa nane, skimu mpya 13 na ukarabati wa skimu za umwagiliaji 17. Ujenzi na ukarabati wa skimu hizo utaongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 50,930 na hivyo kufanya eneo la umwagiliaji kufikia hekta 778,210.6 kutoka hekta 727,280 mwaka 2021/2022.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na changamoto za hali ya hewa, hali ya upatikanaji wa chakula cha kutosha katika maeneo yote nchini imeendelea kuimarika. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2022/2023, uzalishaji wa mazao ya chakula kitaifa ulikuwa tani milioni 17.4 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya tani milioni 15.1. Uzalishaji huo umeihakikishia nchi utoshelevu wa chakula kwa asilimia 115 kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2023/2024.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na uwepo wa ziada ya mazao ya chakula. Nitoe wito kwa Watanzania kuhifadhi mazao ya nafaka kwani utengamano wa hali ya chakula nchini umeendelea kuwepo kutokana na ziada inayotokana na mazao yasiyo ya nafaka.

**49.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha hali ya chakula inaendelea kuimarika. Hadi Januari, 2023, tani 29,084.21 za mahindi zilisambazwa katika Halmashauri 59 zilizopata changamoto ya upungufu wa chakula kwa mwaka 2022/2023. Mahindi hayo yaliuzwa kwa bei ya chini ya soko ili kuimarisha upatikanaji wa chakula katika maeneo hayo.

**50.** ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na hatua hizo, Serikali imeendelea kuratibu upatikanaji wa mbolea, mbegu bora na viuatilifu kwa wakati ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo. Hadi Februari, 2023, upatikanaji wa mbolea umefikia tani 407,333 sawa na asilimia 58.33 ya mahitaji ya tani 698,260. Upatikanaji huo umechangiwa na tani 28,672 zilizozalishwa ndani, tani 251,697 zilizoingizwa kutoka nje ya nchi na tani 126,963 ambazo ni bakaa ya msimu wa 2022/2023. Serikali inaendelea kuhakikisha mbolea iliyobaki inapatikana na kusambazwa kwa wakulima kwa wakati ili kukidhi mahitaji ya kila mkoa na kupunguza makali ya bei.

**51.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali katika kukabiliana na changamoto ya uzalishaji wa ndani wa mafuta kula, imetoa tani 591.1 za mbegu za alizeti kwa wakulima wa Mikoa ya Singida, Dodoma, Kagera, Mbeya na Mwanza kwa utaratibu wa ruzuku. Hatua hiyo, itasaidia kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kuagiza kutoka nje ya nchi. Vilevile, imegawa lita 63,606 za viuatilifu katika mikoa 15 nchini ili kuthibiti viwavijeshi, nzi wa matunda na ndege waharibifu aina ya Quelea quelea. Hatua hiyo imesaidia kuokoa ekari 159,015 za mazao mbalimbali yakiwemo mahindi na mpunga.

**52.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kasi ya kutoa huduma kwa wakulima inaongezeka, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za ugani kwa kutoa mafunzo na vitendea kazi kwa maafisa ugani. Licha ya hayo, imeanzisha Kituo Cha Huduma kwa Wateja. Kituo hicho kimeshatoa huduma ya ushauri na taarifa za kilimo kwa wakulima na wadau wapatao 12,248. Aidha, kwa kupitia mfumo wa M-Kilimo, wakulima 7,269,101 na Maafisa Ugani 9,985 wamesajiliwa kwa ajili ya huduma za ushauri wa kitaalamu. Teknolojia hii itawawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi kuyafikia masoko ya mazao kwa njia ya simu.

**Kuimarisha Ushirika**

**53.** ***Mheshimiwa* Spika,** Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuimarisha ushirika nchini. Hatua hizo ni pamoja na kutoa mafunzo kwa watendaji, kuimarisha udhibiti na usimamizi wa Vyama vya Ushirika; kuhamasisha Wananchi kujiunga au kuanzisha Vyama vya Ushirika; kuimarisha upatikanaji wa masoko ya ndani na nje ya Nchi; kukuza matumizi ya TEHAMA na kufanya kaguzi.

**54.** ***Mheshimiwa* Spika,** kutokana na hatua hizo, mauzo kuipitia Vyama vya ushirika yameongezeka ambapo hadi Januari 2023, zimeuzwa jumla ya tani milioni 1.83 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.7 ikilinganishwa na tani 597,298 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.5 mwaka 2021/2022 kutoka kwenye mazao ya tumbaku, korosho, pamba, kahawa, ufuta, kakao, mkonge, chai, mbaazi, soya, zabibu, miwa na maharage.

**Benki ya Maendeleo ya Kilimo**

**55.** ***Mheshimiwa* Spika,** kwa upande wa uwezeshaji, Benki ya Maendeleo ya Kilimo imefanikiwa kutoa mikopo ya moja kwa moja yenye thamani ya shilingi bilioni 78.54 kwa wakulima 119,797 wanaojishughulisha na kilimo, mifugo na uvuvi. Aidha, kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo imetoa dhamana ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 12.95 na kunufaisha wananchi 961 katika Mikoa 20 katika shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi.

**56.** ***Mheshimiwa* Spika,** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuongeza uzalishaji na tija; kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji, na upatikanaji wa pembejeo. Vilevile, itaendelea kuimarisha huduma za ugani na upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo na kuwajengea uwezo wakulima wadogo.

**Mifugo**

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuimarika kwa huduma za ugani ikiwemo utoaji elimu kwa umma kuhusu ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa wa kibiashara umesababisha kuongezeka kwa uzalishaji wa maziwa kufikia lita bilioni 3.62 katika mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na lita bilioni 3.4 mwaka 2021/2022. Aidha, uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kwa asilimia 4.3 kutoka tani 769,966.66 mwaka 2021/2022 hadi tani 803,264.32 mwaka 2022/2023. Vilevile, jumla ya vipande milioni 14.19 vya ngozi vyenye thamani ya Shilingi bilioni 31.11 vilizalishwa ikilinganishwa na vipande milioni 13.56 vyenye thamani ya Shilingi bilioni 28.5 vilivyozalishwa mwaka 2021/2022.

**58.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Serikali imenunua pikipiki 1,200 na magari 13 ili kurahisisha utoaji wa huduma za ugani katika ngazi ya Kata na Vijiji. Vilevile, Serikali imewezesha mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani 487 na Wataalam Wawakilishi 28 kutoka Sekta Binafsi katika kanda nane. Mafunzo hayo yalihusu Mpango wa Mabadiliko wa Sekta ya Mifugo, Ufugaji bora na wa Kibiashara, Fursa za Uwekezaji katika Sekta ya Mifugo, Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za Ugani, Uboreshaji wa Kosaafu za Mifugo, Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo, Uendelezaji wa malisho na upatikanaji wa maji.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** vifo vya mifugo vinavyotokana na magonjwa yanayoenezwa na kupe vimepungua kwa takriban asilimia 60. Mafanikio hayo yametokana na hatua ya Serikali kuimarisha huduma za mifugo pamoja na ujenzi wa miundombinu muhimu ikiwemo majosho ya kuogesha mifugo.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha sekta ya mifugo kwa kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo, malisho, maji na vyakula vya mifugo. Halikadhalika, Serikali itaboresha huduma za utafiti na mafunzo ya taaluma za mifugo pamoja na kuanzisha na kuendeleza vituo atamizi vya uwekezaji vya vijana.

**Uvuvi**

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuinua kipato cha wananchi wake, kuimarisha upatikaji wa samaki na uendelevu kupitia ukuzaji wa viumbe maji. Katika mwaka 2022/2023, tani 28,856.87 za samaki zilivuliwa kutoka katika ukuzaji viumbe maji ikiwemo ufugaji kwenye mabwawa na vizimba. Kiasi hicho cha samaki kiliwezesha mauzo ya nje ya nchi yenye thamani ya Shilingi bilioni 238.49. Vile vile, tani za mwani 4,134.6 zenye thamani ya Shilingi bilioni 4.34 zilizalishwa na kuuzwa nje ya nchi.

**62.** ***Mheshimiwa* Spika,** katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kuboresha hali ya masoko ya samaki nchini kupitia ujenzi wa masoko mbalimbali ya samaki. Masoko yaliyoboreshwa ni pamoja na Zingibari (Halmashauri ya Mkinga), Kipumbwi (Pangani), Ng'ombo (Nyasa), Manda (Ludewa), Maporomoko (Tunduma), Kyamkwikwi (Muleba), Nyamikoma (Busega) pamoja na Mialo ya kupokelea samaki katika Halmashauri za Momba (Masuche), Nkasi (Karungu) na Chato (Chato beach).

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo, malisho, vyakula vya mifugo na maji. Vilevile, itatoa kipaumbele katika kuimarisha afya ya mifugo, kuboresha huduma za ugani, kuanzisha na kuendeleza vituo atamizi vya uwekezaji vya vijana, kuimarisha huduma za utafiti na mafunzo ya taaluma za mifugo.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali itaendelea kuimarisha Shirika la Uvuvi Tanzania, usimamizi na udhibiti wa ubora, usalama na viwango vya samaki na mazao ya uvuvi pamoja na kuimarisha huduma za utafiti, mafunzo na ugani. Aidha, Serikali itaimarisha miundombinu ya masoko ya samaki, vituo vya kuendeleza ukuzaji wa viumbe maji na kuanza ujenzi wa meli za uvuvi katika bahari kuu.

**MALIASILI NA UTALII**

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha sekta za maliasili na utalii kupitia utekelezaji wa programu mbalimbali ili kukuza utalii, kuitangaza nchi yetu na vivutio vyake kitaifa na kimataifa pamoja na kuimarisha mchango wa sekta hizo kwenye pato la Taifa. Katika mwaka 2022/2023, programu mbalimbali zimeendelea kutekelezwa ikiwemo Programu ya Tanzania - *The Royal Tour na* utangazaji wa vivutio vya utalii kupitia matukio mbalimbali na vyombo vya habari ikiwemo *Tanzania Safari Channel*.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na jitihada hizo, idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kutoka watalii 922,692 katika mwaka 2021 hadi kufikia watalii takriban milioni 1.4 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 57.7. Vilevile, idadi ya watalii wa ndani imeongezeka kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi watalii milioni 2.4 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 199.5. Aidha, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti imeendelea kuwa hifadhi bora duniani ambapo kwa miaka minne mfululizo kuanzia mwaka 2019 hadi 2022 imepata tuzo ya dhahabu ya utoaji wa huduma bora iliyotolewa na *European Society for Quality Research*.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro, kumekuwa na changamoto ya ongezeko la watu, mifugo, makazi holela na shughuli za kibinadamu hivyo kukosekana kwa uwiano baina ya uhifadhi, ukuzaji wa utalii na maendeleo ya jamii. Hali hiyo imekuwa ikitishia uendelevu wa hifadhi na ustawi wa maisha ya watu wanaoishi katika hifadhi hiyo kutokana na sheria za uhifadhi kutoruhusu shughuli nyingi za kiuchumi na kimaendeleo katika eneo hilo. Ili kutatua changamoto hiyo, Serikali iliendesha zoezi la hiari la kuondoa makazi na shughuli za kibinadamu ndani ya Hifadhi kwa kuhamisha wenyeji waliokuwa tayari kuhama kwenda kwenye maeneo yaliyotengwa katika Kijiji cha Msomera katika Halmashauri za Wilaya za Handeni na Kilindi Mkoani Tanga.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi hilo limefanyika kwa umakini mkubwa na kwa kuzingatia haki za wanaohama. Hadi kufikia Januari, 2023 jumla ya kaya 1,524 zenye watu 8,715 na mifugo 32,842 zilikuwa zimejiandikisha kwa ajili ya kuhama kwa hiari kwenda Kijiji cha Msomera. Kati ya kaya hizo, kaya 551 zenye watu 3,010 na mifugo 15,521 tayari zimehamishwa kwa hiari kwenda Msomera.

**69.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ikiwemo utalii wa fukwe, mikutano na matukio, meli, michezo na utamaduni. Vievile, itaendelea kuimarisha miundombinu katika maeneo ya hifadhi, kukarabati majenzi ya kale na kuyatangaza kidijitali pamoja na kutekeleza mikakati ya kuongeza thamani ya mazao ya misitu.

**MADINI**

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Madini ili kuhakikisha inanufaisha wananchi na kuongeza mchango wa sekta hiyo kwenye Pato la Taifa. Katika mwaka 2022/2023, Serikali ilianzisha vituo 26 vya ununuzi wa madini na kutoa jumla ya leseni tano za uchenjuaji wa madini. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 409.66 sawa na asilimia 85.43 ya lengo la shilingi bilioni 479.51 zilikusanywa kutokana na mrabaha, ada ya ukaguzi, mauzo ya madini kwenye masoko na vituo na ada ya leseni za uchimbaji.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuhamasisha biashara na uwekezaji katika Sekta ya Madini; kuwaendeleza wachimbaji wadogo; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kusimamia mifumo ya ukaguzi wa shughuli za migodi; na kuzijengea uwezo taasisi zinazosimamia sekta hiyo.

**NISHATI**

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza azma yake ya kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii kwa kuhakikisha wananchi wake wanapata nishati ya umeme, mafuta na gesi kwa uhakika na bei nafuu.

**73.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa pili. Hadi Machi, 2023 asilimia 76.7 ya Vijiji vya Tanzania Bara vimeunganishwa na huduma ya umeme. Utekelezaji wa miradi hiyo ikiwa ni pamoja na mkakati wa kuboresha upatikanaji wa nishati bora na safi ya kupikia kwa wananchi wanaoishi vijijini inaendelea vizuri na ipo katika hatua mbalimbali.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imekamilisha ufungaji wa mitambo mitatu yenye uwezo wa kuzalisha Megawati 135 katika mradi wa Kinyerezi I *Extension*. Kufungwa kwa mitambo hiyo kumeongeza uwezo wa mitambo kufua umeme katika gridi ya Taifa kwa asilimia 7.52. Aidha, uboreshaji wa mtandao wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme nchini umesaidia kuboresha maisha ya watu kwa kutoa fursa za kiuchumi na kijamii.

**Mafuta na Gesi**

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutimiza azma ya kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi kupikia ifikapo mwaka 2033, kimeundwa kikosi kazi cha Taifa kuchakata na kutoa suluhu ya afua ya nishati safi ya kupikia ambacho nakisimamia mimi mwenyewe. Hii ni kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia. Kazi zinazoendelea ni pamoja na kuandaa rasimu ya Dira ya Taifa ya miaka 10 ya kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na Rasimu ya Mpango Mkakati.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa gesi, Serikali inaendelea kufanya tafiti katika vitalu vya mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati ikiwa ni pamoja na kuimarisha Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia na Mkakati wa matumizi ya nishati jadidifu na tungamotaka.

**77.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kukamilisha utekelezaji wa miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati ya umeme, mafuta na gesi. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu na kusambaza umeme katika vitongoji 36,336 vya Tanzania Bara.

**ARDHI**

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Ardhi imeendelea kuwa kiungo wezeshi kwa shughuli za sekta nyingine za uzalishaji ikiwemo viwanda, kilimo, mifugo, maliasili, utalii, madini na miundombinu. Katika, mwaka 2022/2023, Serikali imeandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya Vijiji 110 katika Halmashauri za Wilaya 16 na Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya tatu za Kigoma, Nsimbo na Ngorongoro. Idadi hii inafanya kuwa na jumla ya Vijiji 2,673 vyenye Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuwezesha na kuandaa Mipango ya Matumizi ya ardhi ya Vijiji, Wilaya na Kanda; utatuzi wa migogoro ya ardhi; kuboresha Mfumo wa Taarifa za Matumizi ya Ardhi Nchini; na kupanga, kurasimisha na kumilikisha ardhi kwa wananchi.

**USAFIRI NA USAFIRISHAJI**

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** miundombinu ya usafiri na usafirishaji ni msingi wa uchumi wa Taifa na inatoa huduma muhimu kwa wananchi wetu. Usimamizi thabiti wa miundombinu hiyo unaipa fursa Serikali kuongeza thamani ya huduma na rasilimali fedha zinazoonekana moja kwa moja kwa manufaa ya jamii.

**Barabara na Madaraja**

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imejenga jumla ya kilomita 317.65 za barabara kwa kiwango cha lami ambazo zimehusisha barabara kuu, barabara za mikoa na wilaya. Ujenzi huo umesaidia kurahisisha utoaji wa huduma ya usafiri na usafirishaji katika maeneo tofauti nchini na umezingatia uendelevu kwa watumiaji wa sasa na wa baadaye.

**82.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inatambua umuhimu wa kupunguza msongamano wa magari katika majiji na miji ili kuongeza ufanisi katika utendaji na utekelezaji wa majukumu ya wananchi na ukuaji wa uchumi wa Taifa. Katika hatua za kuhakikisha kuwa huduma za uchukuzi zinaboreshwa, Serikali inaendelea na Awamu ya Pili, Tatu, Nne na Tano ya ujenzi wa barabara na Miundombinu ya Mabasi yaendayo Haraka Mkoani Dar es Salaam na ujenzi wa barabara za mchepuo (bypass) katika Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Maswa.

**83.** ***Mheshimiwa Spika***, Awamu ya Pili (BRT II) ya ujenzi huo inayohusisha barabara ya Kilwa kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam kuelekea Mbagala na barabara ya Kawawa kutoka makutano ya Magomeni kupitia Chang'ombe hadi makutano ya barabara ya Kilwa umefikia asilimia 82. Mradi huu una barabara zenye urefu wa kilomita 20.3; vituo vya mabasi 29; Barabara za juu mbili; majengo mawili ya *Terminal*; *Depot* moja na *Feeder station* nne.

Aidha, Awamu ya Tatu (BRT III) inayohusisha Barabara ya Nyerere kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi Gongolamboto yenye urefu wa kilomita 23.6 imekamilika kwa asilimia 5.

**84.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Jiji la Dodoma, ujenzi wa barabara ya mchepuko ya Dodoma imelenga kupunguza foleni ya magari katikati ya Jiji kutokana na magari yanayosafiri katika Ushoroba wa kati na Ushoroba wa Barabara Kuu ya *Trans-Africa 4* inayoanzia Cape Town, Afrika Kusini hadi Cairo, Misri. Mradi huu wenye barabara yenye urefu wa jumla ya kilomita 112.3 umefikia kwa asilimia 17 katika sehemu ya kwanza na sehemu ya pili imefikia asilimia 22. Aidha, ujenzi wa Barabara ya Mchepuo Maswa (Maswa Bypass) yenye urefu wa kilomita 11.3 kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 72.

**Vivuko**

**85.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kujenga vivuko vipya na kukarabati vivuko vilivyochakaa nchini ili kuwaondolea kero ya usafiri wananchi wanaotegemea vivuko ili kuharakisha na kurahisisha shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Katika mwaka 2022/23, Serikali imeendelea na ujenzi wa vivuko vipya vya Kisorya – Rugezi, Ijinga – Kahangala, Bwiro – Bukondo na Nyakarilo – Kome. Vilevile, ujenzi wa vivuko vya Buyagu – Mbalika na Magogoni – Kigamboni ambao upo kwenye hatua za ununuzi. Aidha, ukarabati wa vivuko vya MV Musoma, MV Kazi, MV TEMESA na MV Tanga umekamilika kwa asilimia 100 na ukarabati wa vivuko vya MV Misungwi, MV Nyerere, MV Kilombero, MV Mara, MV Ujenzi, MV Kitunda, MV Ruhuhu, MV Old Ruvuvu na MV Magogoni unaendelea.

**Viwanja vya Ndege na Usafiri wa Anga**

**86.** ***Mheshimiwa Spika***, usafiri wa anga ni kiungo muhimu katika kuchangia ukuaji wa pato la mtu binafsi na Taifa kwa ujumla. Usafiri huu umeendelea kutengeneza fursa za ajira zilizo rasmi na zisizokuwa rasmi, kuimarisha upatikanaji wa huduma za usafiri wa uhakika, na hivyo kutoa mchango muhimu katika maendeleo ya kiuchumi. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika uimarishaji na uboreshaji wa huduma za usafiri wa anga nchini.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mwaka 2022/2023 imeendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato. Kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja hiki kutarahisisha usafirishaji wa watu na bidhaa kutoka na kuingia katika Jiji la Dodoma, kati ya Tanzania na nchi mbalimbali; kukuza utalii na uchumi na kuongeza fursa za ajira. Aidha, ujenzi huo utakapokamilika pamoja na kuimarisha usafiri anga kwa kuruhusu ndege kubwa na za kimataifa kutua, utasaidia kufanya Jiji la Dodoma kuwa Jiji la kisasa na kimataifa.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usafiri wa anga, mashirika ya ndege ya *KLM, Eurowing, Edelweissairline* na Saudia *Airline* yameanza kutoa huduma za usafiri wa anga kuanzia Tanzania. Hatua hizi zitaendelea kuimarisha sekta ya utalii na hivyo kuongeza mchango wa sekta hiyo kwenye mapato na ukuaji wa uchumi.

**Reli**

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imefanya ununuzi wa vifaa vya uendeshaji wa Reli ya SGR ambapo utengenezaji wa mabehewa 59 ya abiria umefikia asilimia 92. Kati ya mabehewa hayo, 14 yaliwasili nchini

Novemba, 2022 na 45 yaliyobaki yanatarajiwa kuwasili Mei, 2023. Aidha, utengenezaji wa vichwa vya treni 17 vya umeme na seti 10 za treni (Electric Multiple Unit - EMU) kwa ajili ya treni ya abiria umefikia asilimia 31.6 na seti moja ya treni hizo inatarajiwa kuwasili Juni, 2023. Aidha, utengenezaji wa mabehewa 1,430 ya mizigo umefikia asilimia 35. Upatikanaji wa vifaa hivyo utaboresha na kuongeza kiwango cha ubebaji mizigo na kupunguza gharama za usafiri na usafirishaji, na hivyo kupunguza gharama za maisha.

**90.** ***Mheshimiwa Spika*** Aidha, katika mwaka 2022/2023, pamoja na uendelezaji wa ujenzi wa Reli ya SGR, Serikali imeendelea na ukarabati wa njia ya Reli ya Kati kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma. Mkataba wa ukarabati wa njia ya reli ya Kaliua-Mpanda ulisainiwa Novemba, 2022.

**Usafiri katika Maziwa Makuu**

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za usafiri na usafirishaji katika maziwa makuu, Februari, 2023, meli ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu iliyo katika Ziwa Victoria ilishushwa majini kwa ajili ya ukamilishaji. Meli hiyo inatarajiwa kuanza kutoa huduma katika mwaka 2023/2024. Aidha, ukarabati wa meli ya MV Umoja katika Ziwa Victoria na MT Sangara katika Ziwa Tanganyika unaendelea. Kukamilika kwa meli hizo kutaboresha huduma za usafiri wa abiria na mizigo kwa njia ya meli; kufungua masoko mapya ndani na nje ya nchi; kurahisisha shughuli za kibiashara, uzalishaji wa mazao, uvuvi, madini; na kuchochea utalii katika maeneo ya maziwa makuu.

**Bandari**

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza Mradi wa Bandari Kavu ya Kwala ambapo ujenzi wa barabara ya zege yenye urefu wa kilomita 15.5 kutoka Vigwaza umefikia asilimia 98 na ujenzi wa Bandari umefikia asilimia 87. Kukamilika kwa bandari hiyo na kuanza kutumika kutapunguza msongamano wa mizigo na magari katika Bandari ya Dar es Salaam, kuongezea nafasi ya kuhifadhi mizigo na kupunguza muda wa magari kusafirisha mizigo. Hali hiyo itaiwezesha Bandari ya Dar es Salaam kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na hivyo kuongeza mapato kwa bandari na wafanyabiashara.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, sekta ya usafiri na usafirishaji itaendelea kukamilisha ujenzi wa miundombinu na uboreshaji wa huduma za usafiri kwa njia reli, anga, barabara na majini. Aidha, Serikali imeamua kwa dhati kuanza ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo kwa kuhamisha wananchi waliolipwa fidia, wanaotakiwa kupisha ujenzi wa bandari na kuanza maandalizi ya ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya bandari ya Bagamoyo ikiwemo barabara, reli na umeme.

**MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

**94.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya mawasiliano na teknolojia ya habari nchini kwa lengo la kuongeza chachu ya maendeleo ya jamii, siasa, usalama na uchumi kwa kuzingatia mabadiliko ya teknolojia ulimwenguni.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kutekeleza Mfumo wa Anwani za Makazi kwa kuzingatia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyatoa tarehe 08 Februari 2022 wakati wa uzinduzi wa "Operesheni Anwani za Makazi". Utekelezaji wa Mfumo huo umefanyika nchi nzima ambapo hadi Februari 2023 jumla ya taarifa milioni 12.66 za Anwani za Makazi zikijumuisha majengo na viwanja zimekusanywa. Utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi umewezesha utambuzi wa mtu, kitu au jengo lilipo na hivyo kuimarisha usalama na kurahisisha utoaji wa huduma na ufikishaji wa bidhaa mahali stahiki. Aidha, Serikali inaendelea na uhakiki wa taarifa za anwani za makazi zilizokusanywa ili kuboresha taarifa hizo.

**96.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi wa minara 1,201 katika kata 1,087 zenye vijiji 3,378. Kwa upande wa Zanzibar ujenzi wa minara 42 umekamilika na kufanya eneo lote la Zanzibar kuwa na mawasiliano ya simu. Aidha, Serikali imesaini mikataba ya ujenzi wa minara katika kata 1,242 zenye vijiji 3,654 Tanzania Bara. Kukamilika kwa miradi hiyo kutafanya Taifa kuongeza usikivu katika mawasiliano ya njia ya simu na usafirishaji wa taarifa kwa kasi na kiwango kinachokusudiwa. Nitoe wito kwa Watanzania wote kuendelea kuchangamkia fursa zinazotokana na matumizi ya teknolojia ya mawasiliano katika kujenga uchumi wa kidijitali.

**Uchumi wa Kidijitali**

**97.** ***Mheshimiwa Spika***, ni ukweli usiopingika kuwa fursa za kidijitali na uchumi zimekuwa zikiongezeka ulimwenguni. Fursa hizo zimewezesha ushiriki wa watu wengi na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kimtandao. Vilevile, maendeleo ya kidijitali yamerahisisha mawasiliano ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa kupunguza gharama, kuokoa rasilimali muda na upatikanaji wa taarifa na fursa mbalimbali.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu huo, Serikali katika mwaka 2023/2024 itaendelea na maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali ili kuhakikisha nchi yetu haibaki nyuma katika ulimwengu wa kidijitali na kuwa wananchi wananufaika na fursa zitokanazo na uchumi huo. Kwa upande mwingine itaendelea kujenga misingi ya matumizi ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuendeleza na kuboresha Mfumo wa Kidijitali wa Mfumo wa Anwani za Makazi.

**HUDUMA ZA JAMII**

**Elimu**

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** tangu awali, Serikali ya Awamu ya Sita imejipambanua katika kuinua viwango vya elimu kwa kuweka mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia. Hii ni pamoja na kuhakikisha kila mtoto wa Tanzania anapata fursa ya kusoma na kumaliza mzunguko wa elimu kama inavyotakiwa. Ili kutekeleza azma hiyo, Serikali imeendelea kujenga, kukarabati na kukamilisha miundombinu ya kutolea elimu katika ngazi mbalimbali.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea na ujenzi wa shule mpya 231 za sekondari, upanuzi wa shule kongwe 18 za sekondari, ujenzi wa shule mpya sita za Msingi, ujenzi wa vyumba vya madarasa 1,072 katika shule kongwe za Msingi, na ujenzi wa nyumba za walimu 809 ambapo kati ya nyumba hizo, 298 ni za walimu wa shule za msingi na 511 za walimu shule za sekondari. Aidha, imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa shule za wasichana za bweni kidato cha tano na sita katika mikoa yote Tanzania bara ambapo ujenzi wa shule 10 kati ya 26 umekamilika.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea pia kutoa mikopo na kuongeza wigo wa upatikaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu sambamba na kuboresha miundombinu ya vyuo vya elimu ya juu nchini. Katika mwaka 2022/2023, kiasi cha shilingi bilioni 654 zilitengwa kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ikilinganishwa na shilingi bilioni 570 zilizotengwa mwaka 2021/2022. Aidha, idadi ya wanufaika imeongezeka kutoka 177,605 mwaka 2021/2022 hadi 202,877 mwaka 2022/2023.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeongeza kiwango cha posho ya kujikimu ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka shilingi 8,500 hadi shilingi 10,000 kwa siku. Mafanikio haya ni kielelezo tosha cha umakini, uzalendo, maono na mapenzi makubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuboresha ustawi wa maisha ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu. Kwa upande mwingine, kupitia Samia Scholarship, Serikali imetoa ufadhili kwa wanafunzi 244 wa kike wenye ufaulu wa juu ili kusoma katika vyuo vikuu mbalimbali katika fani za Utabibu, Uhandisi, Sayansi, Teknolojia na hisabati. Ama kwa hakika mama anajali!

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuhuisha Mitaala ya Elimu na kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi na elimu ya juu.

**Maji**

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji ikiwa ni pamoja na kuhifadhi na kulinda vyanzo vya maji, kujenga mabwawa makubwa, ya kati na madogo katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuongeza uwezo wa nchi kuhifadhi maji na kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo ya mijini na vijijini.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza dhamira yake ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji mijini na vijijini inafikia asilimia 95 na 85 mtawalia mwaka 2025. Hadi kufikia Februari, 2023, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini imeongezeka kutoka asilimia 86 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 88 na vijijini imeongezeka kutoka asilimia 72.3 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 77.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko la hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini na vijijini limetokana na kukamilika kwa miradi 36 ya maji mijini na miradi 382 ya maji vijijini inayonufaisha wananchi zaidi ya milioni mbili. Aidha, miradi mingine 139 mijini na 647 vijijini ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya maji vijijini na mijini ikiwemo miradi ya miji 28; ujenzi wa bwawa la Kidunda; kuanza ujenzi wa Bwawa la Farkwa; kujenga mabwawa ya ukubwa wa kati; kuanza ujenzi wa miradi ya uondoshaji wa majitaka; na kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za maji ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**Afya**

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni azma ya Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma bora za afya. Kwa msingi huo, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika sekta ya afya kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha utoaji wa huduma hizo. Mikakati hiyo ni pamoja na ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika kutekeleza azma yake kusogeza huduma za afya karibu na wananchi, imekamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya kanda Mtwara; na Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Mara, Songwe, Shinyanga, Geita na Katavi. Aidha, imekamilisha ujenzi wa hospitali 59 za halmashauri, ukarabati wa hospitali kongwe 19 za halmashauri na ujenzi wa maboma ya zahanati 300. Tayari vituo hivyo vimeanza kutoa huduma.

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya za dharura, Serikali imejenga majengo ya huduma za dharura katika hospitali za kanda na kufikisha hospitali 36 zenye huduma hiyo kutoka hospitali 7 mwaka 2020. Mafanikio haya yamepatikana kutokana na jitihada za makusudi za Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwani kwa mara ya kwanza tangu uhuru, nchi yetu imeweka historia ya kuwa na mfumo wa huduma za dharura kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Taifa. Awali huduma hizo zilikuwa zinapatikana katika ngazi ya Kanda na Taifa pekee. Uwepo wa huduma za dharura katika hospitali zetu utapunguza vifo kwa asilimia 40.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatambua kuwa, ujenzi wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya hauwezi kuwa na tija pasipokuwa na watumishi wenye weledi, vifaa, vifaatiba na vitendanishi. Kutokana na ukweli huo, hadi kufikia Februari, 2023, Serikali imesambaza vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 44.3 pamoja na kuajiri watumishi wa kutoa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, kupitia Programu ya Mfuko wa Pamoja wa Afya, jumla ya shilingi bilioni 48.35 zimetolewa kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za afya.

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya, kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, kuimarisha utoaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi, kuimarisha huduma za afya ya uzazi na kudhibiti magonjwa ya mlipuko. Vilevile, itaendelea kutoa mafunzo kwa wataalam wa sekta ya afya katika ngazi za ubingwa na ubingwa bobezi.

**HUDUMA KWA MAKUNDI MAALUM**

**Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu**

**113.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuboresha huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ambapo mwaka 2022/2023 ilitenga jumla ya shilingi bilioni 3.46 kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa vyuo vya Watu Wenye Ulemavu vya Mtapika (Masasi – Mtwara), Luanzari (Tabora), Sabasaba (Singida) na Yombo (Dar es Salaam). Ukarabati huu umewezesha Chuo cha Luanzari kuanza kutoa mafunzo kwa kudahili wanafunzi 400 baada kufungwa kwa zaidi ya miaka kumi.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ufanisi wa upatikanaji, utunzaji, uchakataji na utumiaji wa taarifa za Watu wenye Ulemavu, Serikali imetengeneza Mfumo wa Kielektroniki wa Watu Wenye Ulemavu. Mfumo huo utawezesha kumsajili na kumtambua mtu mmoja mmoja mwenye ulemavu, mahali alipo, shughuli anayoifanya na mahitaji yake. Vilevile, utawawezesha kuunganishwa na huduma mbalimbali zikiwemo kupata cheti za kuzaliwa, matibabu, kuandikishwa shule ya awali na msingi, mikopo ya asilimia mbili inayotokana na mapato ya ndani ya halmashauri na vifaa saidizi.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile Serikali imeandaa Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu wa Mwaka 2022. Mwongozo huo utasaidia kuhakikisha masuala ya usawa, haki, fursa na huduma kwa Watu Wenye Ulemavu yanaimarishwa katika nyanja zote za maendeleo.

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mwaka 2023/2024 imepanga kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu kujiajiri na kuajiriwa kwa kuongeza fursa za mafunzo ya ufundi stadi na marekebisho kutoka watu 460 hadi 1,400.

**Huduma kwa Wazee**

**117.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuwatambua na kutoa huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi na matibabu kwa wazee wasiojiweza 268 wanaoishi katika makazi 14 ya wazee ya Kibirizi, Njoro, Kolandoto, Bukumbi, Ipuli, Fungafunga, Mwanzange, Misufini, Nunge, Nyabange, Kilima, Sukamahela, Magugu pamoja na Nandanga. Ninatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi kwa ujumla kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuwahudumia wazee na hii ni namna bora ya kutambua umuhimu na michango waliyotoa katika ujenzi wa Taifa hili.

**ULINZI NA USALAMA**

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu imeendelea kuwa shwari bila uwepo wa matukio hatarishi. Katika kuhakikisha hali ya usalama nchini inaendelea kuimarishwa, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vimeendelea kulinda mipaka ya nchi; kudumisha amani, usalama wa raia, mali zao na kufundisha wananchi ulinzi wa umma.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi letu limeendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika katika operesheni mbalimbali za ulinzi wa amani. Katika mwaka 2022/2023, vikosi vyetu vilipeleka waangalizi wa kijeshi, wanadhimu na makamanda kwenye nchi zenye migogoro za Lebanon, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Msumbiji. Ushiriki huo ni muhimu kwa kuwa unalitambulisha Taifa kimataifa, kuwaweka askari wetu tayari kila wakati, kujifunza teknolojia mpya na kushirikisha vijana katika kuleta Amani.

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutambua, kusajili na kutoa vitambulisho vya Taifa ili kuwezesha upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kiusalama. Aidha, hivi karibuni Serikali imefanya marekebisho ya Kanuni za Usajili na Utambuzi wa Watu za Mwaka 2023 ili kuwawezesha Watanzania kuendelea kutumia Vitambulisho vya Taifa bila kuwa na ukomo wa matumizi. Hatua hii inapunguza usumbufu na gharama kwa wananchi na Serikali.

**121.** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kutoa wito kwa watoa huduma wote zikiwemo Ofisi za Balozi mbalimbali hapa nchini kuendelea kutambua na kutoa huduma stahiki kwa wananchi wenye vitambulisho vya Taifa bila kujali tarehe za ukomo zilizo kwenye vitambulisho hivyo.

**122.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kuviimarisha na kuviongezea uwezo vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuvipatia vifaa na zana bora za kisasa. Vilevile, Jeshi litaendelea kuwajengea vijana wa Kitanzania ukakamavu, uzalendo na uwezo wa kujitegemea.

**MASUALA YA KAZI NA WAFANYAKAZI**

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kazi na wafanyakazi kwa kusimamia viwango vya kazi pamoja na masuala ya afya na usalama mahali pa kazi. Katika mwaka 2022/2023, jumla ya kaguzi 3,327 za viwango vya kazi zilifanyika sawa na asilimia 69.31 ya kaguzi 4,800 zilizopangwa kufanyika. Vilevile, kaguzi 96,693 zinazohusu afya na usalama mahali pa kazi zilifanyika ambapo kumekuwa na ongezeko la upimaji wa afya kutoka Wafanyakazi 125,616 mwaka 2021/2022 hadi Wafanyakazi 169,735 mwaka 2022/2023. Kufuatia kaguzi hizo, waajiri 173 waliokiuka sheria za kazi walichukuliwa hatua.

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine, Serikali imeimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Kushughulikia Maombi ya Vibali vya Kazi. Uimarishaji wa mfumo huo, pamoja na mambo mengine umechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufanisi katika utoaji wa vibali vya kazi nchini. Mathalani, hadi kufikia Februari, 2023 jumla ya vibali vya kazi 8,576 vilitolewa sawa na asilimia 92.14 ya maombi ya vibali 9,307 yaliyopokelewa.

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Sheria za kazi, uratibu wa ajira za wageni na masuala yote yanayohusu usalama na afya mahali pa kazi. Aidha, Serikali itaendelea, kutoa elimu na ushauri kwa wafanyakazi, waajiri na vyama vyao ili kuwa na rasilimali watu imara na yenye tija kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

**HIFADHI YA JAMII**

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya Hifadhi ya Jamii imekuwa na mchango mkubwa kwenye uchumi pamoja na ustawi kwa wananchi. Aidha, hadi Februari, 2023 deni la shilingi trilioni 2.17 limelipwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF). Fedha hizo ni stahili ya mafao kwa wanachama waliorithiwa kutoka uliokuwa Mfuko wa PSPF Mwaka 1999.

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Mfuko wa PSSSF umelipa mafao kwa wastaafu, wategemezi na wanufaika wengine wapatao 41,939 yenye thamani ya shilingi trilioni 1.074 na pensheni ya kila mwezi ya shilingi bilioni 507.28 sawa na wastani wa shilingi bilioni 63.41 kila mwezi kwa wastaafu 158,351. Aidha, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umelipa mafao ya shilingi bilioni 438.32 kwa wastaafu, wategemezi na wanufaika wengine wapatao 66,628. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 72.3 zililipwa kama pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu 27,570 ikiwa ni wastani wa shilingi bilioni 9.04 kwa kila mwezi.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mapenzi makubwa aliyonayo kwa wananchi wake, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alielekeza kurejesha michango ya watumishi walioondolewa kazini kwa kughushi vyeti. Utekelezaji wa maelekezo hayo umeanza ambapo hadi sasa jumla ya watumishi 11,896 wamerejeshewa michango yao yenye thamani ya shilingi bilioni 35.02 kupitia PSSSF na NSSF. Mifuko hiyo inaendelea kuwalipa watumishi hao kadri inavyopokea taarifa kutoka kwa waajiri.

**129.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kujenga mazingira wezeshi kwa waajiri, kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji, na kupunguza gharama za uendeshaji ili kukuza uchumi wa nchi na kulinda rasilimali watu. Hatua hizo ni pamoja na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kupunguza kiwango cha uchangiaji kwa Waajiri wa Sekta Binafsi kutoka asilimia 0.6 hadi asilimia 0.5.

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kuhakikisha wananchi wengi wanajumuishwa katika mpango wa Hifadhi ya Jamii wa uchangiaji. Natoa wito kwa sekta isiyo rasmi ikiwemo mama/baba lishe, machinga, bodaboda, wakulima, wavuvi, wafugaji, na wengineo kujiunga na mifuko hiyo kwa manufaa yao ya baadaye.

**Ukuzaji wa Fursa za Ajira na Ujuzi**

**131.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuratibu masuala ya uzalishaji wa fursa za ajira nchini kupitia utekelezaji wa miradi ya kielelezo, kujenga mazingira wezeshi kwa wawekezaji na kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi. Katika mwaka 2022/2023, jumla ya fursa za ajira 547,031 zilizalishwa. Kati ya hizo, ajira 321,363 zilizalishwa kupitia Serikali na utekelezaji wa miradi ya maendeleo na 225,668 kupitia sekta binafsi.

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuchukua hatua ili kuhakikisha wahitimu wa mafunzo ya ujuzi wanaunganishwa na fursa za kujiajiri. Utaratibu huo utamwezesha mhitimu wa mafunzo ya ujuzi kupata sehemu ya uzalishaji yenye viwango vinavyohitajika chini ya usimamizi wa watalaamu wenye uzoefu katika fani husika kwa kipindi maalumu cha miezi 6 hadi 12 kutegemeana na aina ya fani.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuwezesha na kuratibu masuala ya ukuzaji wa fursa za ajira na kazi za staha kwa kuboresha na kutekeleza Sera, Mikakati na Mipango mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili kuhakikisha nguvu kazi ya Taifa inapata fursa za kujiajiri au kuajiriwa ili kuchangia katika maendeleo ya Taifa.

**UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali zinazolenga kuwawezesha wajasiriamali kukuza mitaji yao na kufikia masoko makubwa kupitia Vituo vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Katika mwaka 2022/2023, jumla ya shilingi bilioni 326.6 zimetolewa kwa wajasiriamali 903,763. Kati yao wanawake ni 478,994 sawa na asilimia 53 na wanaume 424,769 sawa na asilimia 47. Upatikanaji wa fedha hizo umewawezesha wajasiriamali kuanzisha na kukuza biashara zao. Aidha, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*Women Development Fund - WDF*), mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 663.4 ilitolewa kwa Wanawake 96 ili kuwawezesha kiuchumi.

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuwaunganisha wajasiriamali na fursa za kiuchumi. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha vituo vya uwezeshaji ili kuchochea shughuli za kiuchumi kwa wananchi.

**MAENDELEO YA VIJANA**

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuwawezesha vijana ili kujiari, kushiriki kwenye shughuli za maendeleo na kuchangia katika pato la Taifa. Katika mwaka 2022/2023, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.88 kwa ajili ya kuwezesha miradi 85 ya vijana katika sekta za kilimo, viwanda na biashara kwenye halmashauri 28. Aidha, Serikali imetoa mafunzo ya ujasiriamali, usimamizi, kurasimisha na kuendeleza biashara kwa vijana 2,497 walio katika Mikoa ya Kagera, Dodoma, Katavi, Shinyanga na Lindi.

Vilevile, kazi ya kuboresha Mwongozo wa Utoaji mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana imekamilika na Mfuko unatoa mikopo kwa vijana walio katika vikundi, mtu mmoja mmoja na Kampuni.

**137.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande mwingine, Serikali imeendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili kupitia Mpango wa Jenga Kesho Iliyo Bora. Mpango huo unalenga kuongeza ushiriki wa vijana katika sekta ya kilimo kwa kuwapatia mafunzo, mashamba, mitaji na kuwaunganisha na fursa za masoko. Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango huo imeanza mkoani Dodoma katika Shamba la Chinangali II lenye ukubwa wa ekari 400. Aidha, zaidi ya hekta 47,000 zimeshapatikana katika mikoa mbalimbali nchini na upimaji udongo unaendelea.

**138.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi, Serikali imetoa fursa za mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri au kuajiriwa kwa vijana 14,542 katika fani mbalimbali kupitia mafunzo ya uanagenzi, uzoefu wa kazi, ufugaji wa samaki na viumbe maji na kilimo cha kisasa kwa njia ya vizimba.

**139.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha uwezo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana katika kutoa mikopo na mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana wengi ili kuwawezesha kujiajiri na kuchangia uchumi wa Taifa. Vilevile, itaanzisha kampeni ya kuwashawishi vijana kushiriki katika kilimo

**MASUALA MTAMBUKA**

**Sensa ya Watu na Makazi 2022**

**140.** ***Mheshimiwa Spika***, nchi yetu ilitekeleza zoezi la Sensa ya Watu na Makazi tarehe 23 Agosti, 2022. Zoezi hilo lililojumuisha sensa ya watu na makazi, anwani za makazi na majengo lilifanyika kwa mafanikio makubwa na wananchi kuonesha ushirikiano wa hali ya juu. Matokeo ya awali ya Sensa ya Watu na Makazi yalizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Oktoba, 2022. Matokeo hayo ya awali yamechangia kwa kiasi kikubwa katika maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2023/2024. Aidha, Serikali imekamilisha ripoti nane ambazo zimejikita kwenye mgawanyo wa idadi ya watu kwa umri na jinsi. Ripoti hizi zitasaidia kuongeza wigo wa matumizi ya takwimu.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa wito kwa viongozi wenzangu na wananchi kuwa tuendelee kuhamasisha matumizi ya matokeo ya sensa ya watu na makazi, majengo na anwani za makazi katika biashara, shughuli za kijamii na mipango ya maendeleo ya nchi. Aidha, nitumie fursa hii kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano mkubwa ambao Waheshimiwa Wabunge walionesha wakati wa utekelezaji wa zoezi la Sensa. Nawashukuru wenyeviti wa kamati za Sensa katika ngazi mbalimbali kwa uongozi wao mahiri, Makamisaa wa Sensa na wadau mbalimbali kutoka sekta ya umma na binafsi na wananchi wote katika kuunga mkono juhudi za Serikali katika kufanikisha Sensa ya Watu na Makazi, Majengo na Anwani za Makazi.

**Mapambano Dhidi ya Rushwa**

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kupambana na vitendo vya rushwa na ufisadi ambapo nguvu kubwa ilielekezwa kwenye uzuiaji wa vitendo hivyo. Hadi kufikia Februari, 2023, kesi za rushwa zipatazo 696 zikiwemo kesi mpya 203 ziliendeshwa mahakamani. Kati ya kesi hizo, kesi 248 ziliamuliwa mahakamani na watuhumiwa 142 walikutwa na hatia.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya Maendeleo 810 yenye thamani ya Shilingi trilioni 6.89 umefanyika. Kutokana na ufuatiliaji huo, miradi 119 yenye thamani ya shilingi billioni 46.04 ilionekana kuwa na kasoro mbalimbali katika utekelezaji na inaendelea kufanyiwa uchunguzi ili hatua stahiki zichukuliwe.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendeleza mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi kwa kuweka kipaumbele katika kuzuia vitendo vya rushwa. Serikali pia itatoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya vitendo vya rushwa kupitia programu ya TAKUKURU-RAFIKI.

**Mapambano Dhidi ya UKIMWI**

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** sote tunafahamu UKIMWI umeendelea kuwa miongoni mwa majanga makubwa duniani kwa miongo kadhaa. Serikali kwa kutambua ukweli huo, imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za mapambano dhidi ya ugonjwa huo. Jitihada hizo ni pamoja na kuandaa mikakati na kutekeleza afua mbalimbali za kupunguza maambukizi, unyanyapaa pamoja na vifo vitokanavyo na janga hilo.

**145.** ***Mheshimiwa Spika***, kama mtakumbuka katika maadhimisho



ya Siku ya UKIMWI Duniani ya Mwaka 2022 yaliyofanyika Mkoani Lindi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Mkakati wa Tano wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa Mwaka 2021/2022 – 2025/2026. Mkakati huo umelenga kuhakikisha kuwa malengo ya sifuri tatu yatafikiwa ifikapo mwaka 2030. Malengo hayo ni kudhibiti maambukizi mapya ya VVU, kukomesha unyanyapaa na kutokomeza vifo vitokanavyo na UKIMWI.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na jitihada zilizofanyika ikiwemo matumizi ya dawa za ARV, afua za kinga zinazotekelezwa na wadau mbalimbali nchini na afua za mabadiliko ya tabia, tohara ya kitabibu kwa wanaume na kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, maambukizi mapya ya VVU kwa watu wazima (miaka 15 na zaidi) yameshuka kutoka 110,000 mwaka 2010 hadi 54,000 mwaka 2022. Wakati huo huo, vifo vinavyotokana na UKIMWI vimepungua kwa asilimia 55 kutoka vifo 65,000 mwaka 2010 hadi 29,000 mwaka 2022. Vilevile, maambukizi mapya kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto yameshuka kutoka asilimia 18 mwaka 2010 hadi asilimia 7 mwaka 2022.

**147.** ***Mheshimiwa Spika***, matumizi ya dawa za kufubaza Virusi Vya UKIMWI kwa WAVIU wanaojua hali zao za maambukizi yameongezeka kutoka asilimia 95 mwaka 2016 hadi asilimia 98 mwaka 2022. Hadi kufikia Desemba 2022 WAVIU zaidi ya milioni 1.5 walikuwa kwenye huduma za tiba na matunzo. Aidha, WAVIU wanaofahamu hali zao za maambukizi na wapo kwenye matibabu ni asilimia 99 na WAVIU waliopo kwenye matibabu na wamefubaza VVU ni asilimia 98. Mafanikio haya ni makubwa ikilinganishwa na malengo ya Kimataifa ya kufikia 95-95-95.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana, bado kuna mambo mengi yanayohitaji kufanyika ili kufikia azma yetu ya kumaliza kabisa janga la UKIMWI. Kwa kutambua hilo, Serikali itaendelea kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI, na kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za UKIMWI pamoja na afua nyingine mahsusi za kudhibiti janga hilo. Kwa upande mwingine, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutekeleza afua za mapambano dhidi ya UKIMWI. Nitumie fursa hii kushukuru sana asasi za kiraia na wadau wa maendeleo kwa michango yao katika mapambano ya kutokomeza UKIMWI nchini.

**Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya**

**149.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa kutambua madhara ya dawa za kulevya kwa nguvu kazi hapa nchini, imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika mapambano dhidi ya dawa hizo. Katika mwaka 2022/2023, imeendesha oparesheni za kuwakamata wanaojihusisha na biashara hiyo pamoja na kuzuia mianya ya kusafirisha na kusambaza dawa hizo. Katika oparesheni hizo watuhumiwa 7,113 pamoja na kilogramu 20,450.30 za dawa za kulevya zilikamatwa. Dawa hizo ni *heroin* kilogramu 53.01, *cocaine* gramu 843.55, bangi kilogramu 12,869.39, mirungi kilogramu 7,525.53, na aina nyingine ya dawa za kulevya *(Methamphetamine na Mescaline)* gramu 1,024.7. Aidha, iliteketeza ekari 69 za bangi katika maeneo mbalimbali nchini na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya matumizi ya dawa za kulevya.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeimarisha huduma za matibabu kwa watumiaji wa dawa za kulevya kwa kuongeza idadi ya kliniki zinazotoa huduma kwa waathirika wa dawa za kulevya kutoka 9 mwaka 2020/2021 hadi kliniki 15 zinazohudumia waathirika zaidi ya 14,500 mwaka 2022/2023. Licha ya hayo, Serikali kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi imewezesha Waraibu wa Dawa za Kulevya waliopata nafuu wapatao 245 kupata mafunzo ya ujuzi kupitia vyuo vya VETA, Don Bosco na SIDO.

**151.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kusimamia na kuratibu uendeshwaji wa Nyumba za Upataji Nafuu 44 Nchini, kuzijengea uwezo Asasi za Kiraia 65 ambazo zinatoa elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya kwa jamii, kuandaa Mwongozo wa Utoaji Elimu kuhusu Tatizo la Dawa za Kulevya Nchini ambao umezinduliwa tarehe 02 Julai, 2022 kwa lengo la kuwapatia elimu na mbinu sahihi kulingana na mahitaji ya makundi mbalimbali ya kijamii. Nitoe wito kwa wadau wote mkiwemo Waheshimiwa Wabunge wenzangu, asasi za kiraia, viongozi wa dini, vyombo vya habari na jamii nzima kushirikiana na Serikali kutoa elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya ili kuokoa kizazi cha sasa na kijacho.

**Uratibu wa Maafa**

**152.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuhakikisha nchi inakuwa stahimilivu dhidi ya majanga kwa kuweka utaratibu mzuri wa kushughulikia masuala ya maafa hapa nchini. Ili kuweka utaratibu huo, Serikali imetunga Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 6 ya Mwaka 2022; Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022-2027; Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa Mwaka 2022; Mkakati wa Taifa wa Afya Moja wa Mwaka 2022-2027; na Mwongozo wa Taifa wa Kupambana na Vitendo vya Kihalifu katika Bahari na Maziwa Makuu wa Mwaka 2022. Kama mtakumbuka, Nyaraka hizo nilizizindua tarehe 09 Februari, 2023 kwa ajili ya utekelezaji.

**153.** ***Mheshimiwa Spika***, nyaraka hizo zimeweka utaratibu wa kuhakikisha Wizara, Idara, Taasisi za Umma na zisizo za Umma, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinashiriki kikamilifu katika kutekeleza shughuli za kuzuia na kupunguza madhara ya majanga. Aidha, zimeweka pia utaratibu wa kujiandaa, kukabiliana na kurejesha hali iliyotoweka pindi maafa yanapotokea. Nitoe wito kwa taasisi husika kuandaa mipango kazi na taratibu za usimamizi wa maafa pamoja na ushughulikiaji wa dharura.

**154.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, jumla ya wajumbe 555 wa Kamati za Usimamizi wa Maafa na Waratibu wa Maafa walipata mafunzo ya kuimarisha uwezo wa utendaji kazi katika Mikoa ya Arusha, Morogoro, Kilimanjaro, Lindi, Mtwara na Singida. Aidha, jumla ya wavuvi 344 katika mwambao wa Ziwa Victoria na vijana 40 wa kujitolea katika Mikoa ya Dodoma, Iringa, Songwe na Tabora walipata mafunzo ya uokoaji, yaliyowaongezea uwezo wa kukabiliana na maafa kwa wakati.

**155.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza ushirikiano na nchi nyingine katika kushughulikia masuala ya maafa ikiwemo nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Tanzania imekuwa nchi ya kwanza kusaini mkataba wa kuanzisha Kituo cha Huduma za Binadamu na Operesheni za Dharura cha Kanda ya SADC. Lengo la kuanzisha kituo hicho ni kusimamia utoaji wa huduma na misaada ya kibinadamu kwa nchi wanachama. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, masuala ya majanga hayana mipaka na yanahitaji jitihada za pamoja katika kuyashughulikia.

**156.** ***Mheshimiwa Spika***, kama mtakumbuka, katika kuendeleza uhusiano na nchi nyingine, hivi karibuni nchi yetu imeungana na mataifa mengine duniani kutoa misaada ya kibinadamu kwa nchi zilizopatwa na maafa makubwa yaliyosababisha vifo na majeruhi, uharibifu wa mali na mazingira. Nchi hizo ni pamoja na Malawi iliyokumbwa na mafuriko yaliyosababishwa na kimbunga Freddy kilichotokea tarehe 13 Machi 2023 na nchi ya Uturuki iliyokumbwa na tetemeko la ardhi mwezi Februari mwaka huu. Misaada iliyotolewa kwa nchi ya Malawi ni pamoja na mahindi tani 1,000, mablanketi 6,000, mahema 50, fedha taslimu shilingi milioni 705, dawa za binadamu na helkopta 2 kwa ajili ya kusaidia uokoaji. Aidha, fedha taslimu dola za Marekani milioni moja zilitolewa kwa nchi ya Uturuki.

**157.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea na ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa Jijini Dodoma, kuimarisha maghala ya vifaa vya misaada ya kibinadamu kwa kuongeza vifaa na kuendelea kutoa misaada kwa waathirika wa maafa.

**Uratibu wa Masuala ya Lishe**

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za lishe ili kuimarisha afya na hivyo kuwezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo. Kutokana na umuhimu wa masuala ya lishe, tarehe 30 Septemba, 2022 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisaini mikataba na Wakuu wa Mikoa yote Tanzania Bara kwa lengo la kuhakikisha kipaumbele kinatolewa kwenye masuala ya lishe ikiwa ni pamoja na kuhakikisha halmashauri zinatenga shilingi 1,000 kwa kila mtoto chini ya miaka mitano. Vilevile, alielekeza fedha zinazopangwa kutekeleza afua za lishe kutolewa kwa wakati na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa, ikiwa ni pamoja na kuimarisha uhamasishaji wa utekelezaji wa afua za lishe bora na kuweka mikakati ya kuhakikisha vyakula vinavyohitajika kukamilisha lishe vinapatikana katika ngazi zote.

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** maelekezo hayo ya Mheshimiwa Rais yaliongeza chachu ya utekelezaji wa masuala ya lishe sambamba na malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa Masuala ya Lishe wa Mwaka 2021/2022 - 2025/2026. Aidha, katika Mkutano wa Nane wa Wadau wa Lishe Kitaifa, uliofanyika Disemba, 2022 Mkoani Mara, Mkakati wa Sekta Binafsi unaoainisha mikakati ya sekta hiyo kuiunga mkono Serikali kuimarisha hali ya lishe nchini ulizinduliwa.

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na jitihada mbalimbali za Serikali na wadau, yapo baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ambayo ni pamoja na kupungua kwa udumavu kutoka asilimia 34.4 mwaka 2015/2016 hadi asilimia 30 mwaka 2022 na kupungua kwa kiwango cha ukondefu kutoka asilimia 4.5 hadi 3.3 katika kipindi hicho.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Pili wa Kitaifa wa Masuala ya Lishe wa Mwaka 2021/2022 - 2025/2026. Nitoe wito kwa wananchi kuzingatia ulaji sahihi wa vyakula mchanganyiko kama tunavyoelekezwa na wataalamu wetu wa masuala ya Lishe. Vilevile, niwaombe Wadau wa Maendeleo na Sekta Binafsi kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuimarisha hali ya lishe nchini.

**Mazingira**

**162.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita katika kuweka msisitizo wa uhifadhi wa mazingira imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali pamoja na maboresho ya Sera na Sheria ili ziwiane na mahitaji ya sasa ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Katika kutelekeza azma hiyo, Serikali imeandaa Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032) kwa lengo la kutoa mwongozo wa hatua za kuchukua ili kutatua changamoto za mazingira nchini kwa kuzingatia sehemu husika na hatua mahsusi zinazopaswa kuchukuliwa.

**163.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Serikali imeandaa Kanuni za Biashara ya Kaboni za Mwaka 2022 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali kupitia GN 636 kwa lugha ya Kingereza na GN 637 kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, Serikali imeandaa Mwongozo kwa ajili ya kutoa maelekezo mbalimbali kuhusu ushiriki wa wadau katika biashara hiyo.

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine Serikali imeratibu ushiriki wa nchi katika mikutano ya kimataifa. Mikutano hiyo imekuwa na mafanikio na munafaa kwa Taifa letu ambapo kupitia Mkutano wa 27 wa Nchi wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi, Tanzania imepata miradi ya nishati jadidifu ambayo itafadhiliwa na Benki ya Dunia, Taasisi ya Afrika 50 na Shirika la Nishati la Afrika kwa kushirikiana na kampuni ya *China Renewable Energies*.

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kuchukua hatua za kupunguza uharibifu wa mazingira. Aidha, itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira, mabadiliko ya tabianchi na fursa ya biashara ya kaboni. Vilevile, itaratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu mabadiliko ya Sheria na Sera ya Mazingira.

**UCHUMI WA BULUU**

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kuhamasisha wananchi juu ya kuibua fursa zilizo kwenye Uchumi wa Buluu kupitia matumizi endelevu ya rasilimali maji kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira na ushirikishwaji wa jamii. Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kuendelea kukamilisha Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu pamoja na Mkakati wa Utekelezaji. Sera hiyo italenga kukuza uwekezaji katika rasilimali za Uchumi wa Buluu; kuongeza fursa za ajira na kazi za staha kupitia shughuli za Uchumi wa Buluu; na kuwa na usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za Uchumi wa Buluu unaozingatia misingi ya utawala bora.

**Utawala Bora**

**167.** ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeendelea kujenga uelewa wa pamoja kwa wadau wote hususan wananchi kuhusu masuala ya kisheria, upatikanaji wa haki zao, kuongeza uwazi na kupunguza gharama. Vilevile, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kukamilisha rasimu ya Awali ya ufasiri wa Sheria Kuu 219 na Sheria Ndogo 148 kwa lugha ya Kiswahili. Zoezi la ufasiri wa Sheria Kuu na Sheria Ndogo zote kutoka lugha ya Kingereza kwenda lugha ya Kiswahili ili kupanua wigo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya Sheria katika vyombo vya utoaji haki ikiwemo Mahakama, Mabaraza na vyombo vingine vyenye jukumu la kutoa haki linaendelea.

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kutekeleza Kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia, kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala na kuendelea kutafsiri sheria kutoka Lugha ya Kiingereza kuwa lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha wananchi kuelewa mwenendo wa mashauri yanayowahusu na hivyo kuweza kupata haki zao.

**MFUMO WA SERIKALI WA TEHAMA**

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha matumizi ya Mfumo wake wa TEHAMA wa kubadilishana taarifa ambapo hadi sasa jumla ya mifumo 60 ya Taasisi 55 imeunganishwa na inabadilishana taarifa. Utekelezaji huo pia ni maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa na mifumo michache inayobadilishana taarifa. Uunganishaji wa mifumo hiyo umeongeza tija na ufanisi katika kuwahudumia wadau hususan wananchi.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kurahisisha utendaji kazi kwa kutumia Mfumo wa TEHAMA, kupunguza gharama za kutoa huduma ili kutoa unafuu kwa wananchi pamoja na kuimarisha mifumo inayobadilishana taarifa.

**UKATILI DHIDI YA WATOTO**

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za kupinga ukatili dhidi ya watoto shuleni na nje ya shule. Katika mwaka 2022/2023, hatua zilizochukuliwa ili kupinga ukatili huo ni pamoja na kuunda madawati 1,393 ya ulinzi na usalama wa mtoto katika shule za msingi na sekondari kwenye Mikoa ya Rukwa, Arusha, Tanga, Dar es Saalam, Pwani, Shinyanga, Dodoma na Geita. Vilevile, Mabaraza ya Watoto 560 yameundwa kwa lengo la kutoa fursa kwa watoto kutoa maoni yao kwa uhuru na kuwajengea uwezo wa kujiamini, kujieleza na kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu haki na ustawi wa watoto.

**172.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Serikali imeendelea kuhamasisha jamii kushiriki katika ulinzi na usalama wa mtoto ili kutokomeza ukatili dhidi ya watoto. Aidha, kupitia jitihada mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (2021/2022 - 2024/2025), wananchi wameendelea kuhamasishwa kujitolea kwa hiari kupambana na vitendo vya ukatili ikiwa ni pamoja na kutambua wajibu wao juu ya ulinzi wa mtoto kuanzia ngazi ya familia.

**173.** ***Mheshimiwa Spika***, nitoe rai kwa Mamlaka zinazohusika chini ya uratibu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kuimarisha mfumo wa ushughulikiaji wa matukio ya ukatili dhidi ya watoto ndani na nje ya shule unaowajumuisha wasimamizi wa shule, wazazi, walezi na jamii na kuandaa Mfumo jumuishi wa kukusanya taarifa na takwimu za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

**MUUNGANO**

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kushughulikia changamoto mbalimbali zinazojitokeza kwa lengo la kuulinda, kuuenzi na kuudumisha Muungano wetu. Katika mwaka 2022/2023, jumla ya hoja nne kati ya nane zilipatiwa ufumbuzi na kuondolewa katika orodha ya hoja za Muungano. Vilevile, Serikali iliandaa kitabu kinachoitwa "Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo". Kitabu hiki kimepatiwa ithibati kwa ajili ya kutumika kama kitabu cha ziada kwa shule za sekondari nchini ili kuendelea kukuza uelewa kuhusu Muungano.

**175.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zitaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuendelea kutatua changamoto zilizosalia kwa lengo la kuulinda, kuuenzi na kuudumisha Muungano wetu.

**USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA**

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** sote tumeshuhudia kuimarika kwa mahusiano yetu na nchi nyingine, jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa chini ya Rais wetu mpendwa Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan. Kuimarika kwa ushirikiano huo kumetokana na Serikali kuendelea kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje inayoweka msisitizo katika kutekeleza diplomasia ya kiuchumi.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mahusiano na mataifa mengine duniani, Viongozi wetu Wakuu wakiongozwa na Rais wetu wameshiriki katika ziara mbalimbali ambazo zimeiletea manufaa makubwa nchi yetu. Mathalan, Mwezi Novemba 2022, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitembelea nchini China kufuatia mwaliko uliotolewa na Mheshimiwa Xi Jinping, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China. Vilevile, Viongozi wetu Wakuu wameshiriki katika ziara mbalimbali za kikazi katika nchi za Marekani, Qatar, Ethiopia, Kenya, Misri, Oman, Afrika Kusini, Rwanda, na Burundi.

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia ziara hizo, nchi yetu imenufaika katika uboreshaji wa miundombinu, huduma za jamii, biashara, uwekezaji, uchumi wa kidijitali, maendeleo ya kijani, uchumi wa buluu, uvuvi, fedha, utalii, afya na kilimo.

**179.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza diplomasia ya kiuchumi, Serikali imeratibu majadiliano ya awamu ya pili ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA) kwa upande wa Afrika Mashariki. Ushiriki wa nchi yetu katika eneo huru la biashara utachochea ukuaji wa uchumi na biashara, kukuza ushiriki wetu katika biashara ya Dunia na kujenga uwezo wa kuongeza thamani ya bidhaa kupitia sera bora za kukuza teknolojia, ubunifu na ushindani.

**180.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kufungua nchi kiuchumi kwa kuvutia uwekezaji na kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo nchini; kuimarisha mahusiano ya kikanda na kimataifa na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji katika sekta mbalimbali za maeneo ya kipaumbele hususan Uchumi wa Buluu na kidijitali.

**SERIKALI KUHAMIA DODOMA**

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutekeleza kwa vitendo zoezi la Serikali kuhamia Dodoma kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma za Serikali kwa wananchi.

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea na Awamu ya Pili ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Mji wa Serikali Mtumba. Ujenzi huo umefikia wastani wa asilimia 60. Aidha, kazi nyingine zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato kitakachogharimu shilingi bilioni 165 na ujenzi wa barabara ya mzunguko ya nje yenye urefu wa kilomita 112.3 kwa gharama ya shilingi bilioni 221. Kwa upande wa Balozi na Jumuiya za Kimataifa, balozi za nchi za Ujerumani, Ufaransa, China na Umoja wa Mataifa zimefungua Ofisi ndogo Jijini Dodoma.

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kukamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara, Ofisi za Taasisi na miundombinu ya kudumu kwenye Mji wa Serikali pamoja na kuendelea kuratibu uhamiaji wa Taasisi.

**SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO**

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kutambua umuhimu wa kukuza utamaduni, sanaa na michezo imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha sekta hiyo kwa kuzingatia kuwa sekta hii ni chachu ya kuendeleza utamaduni wa Kitanzania, utambulisho wa Taifa, chanzo kikubwa cha ajira, huimarisha afya pamoja na kuchangia katika pato la Taifa.

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Tanzania Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kusajili vituo 30 vya kufundisha Kiswahili. Kati ya hivyo: vituo 10 vipo katika Balozi za nchi yetu nchini Korea Kusini, Ufaransa, Italia, Mauritius, Nigeria, Sudan, Zimbabwe, Uholanzi, Cuba na Umoja wa Falme za Kiarabu; vituo vinne nje ya Balozi zetu katika nchi za Afrika Kusini, Italia, Ujerumani na Ethiopia na vituo 16 vya kufundisha lugha hiyo vimeanzishwa nchini. Aidha, kwa upande mwingine Tanzania imesaini makubaliano na nchi ya Afrika Kusini kuwezesha nchi hiyo kutumia Kiswahili kuwa Lugha ya kujifunza na kufundishia katika elimu ya msingi.

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ili kuwawezesha wasanii kuendeleza kazi zao kwa kuwapa mikopo na elimu ya ujasiriamali. Hadi kufikia Februari, 2023 tayari imeshatoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.07 kwa wanufaika 45 ambao ni wasanii na wadau wa sanaa. Mikopo hiyo imewawezesha wasanii na wadau wa sanaa kuandaa kazi bora na zenye uwezo wa kuhimili ushindani katika soko la sanaa.

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa nafasi hii, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa motisha kwa vilabu vya ndani vinavyoshiriki mashindano ya kimataifa kupitia ***Goli la Mama*** ambapo amekuwa akitoa shilingi milioni tano kwa kila goli linalofungwa. Sote tumeshuhudia *Simba Sports Club* almaarufu *Wekundu wa Msimbazi* wakijitwalia kitita cha shilingi milioni 50 wakati huo huo klabu ya *Young Africans Sports Club* almaarufu *Timu ya Wananchi* wakijitwalia shilingi milioni 45.

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninavipongeza sana vilabu hivyo kwa kufika hatua ya robo fainali katika michuano ya Klabu Bingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Barani Afrika. Ni matumaini yetu sote kuwa vilabu hivyo na vingine vinavyoshiriki mashindano ya kimataifa vitaendelea kujituma na kupambana ili vikombe vya ushindi vije nyumbani.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kuratibu Programu ya ukarabati wa viwanja vya michezo katika shule 56 katika mikoa yote Tanzania Bara; kuratibu Programu ya Sanaa na michezo ya kuanzia ngazi ya Mtaa kwa Mtaa kuelekea ngazi za juu ikiwemo *"Taifa Cup"*; kutenga maeneo ya michezo kwa lengo la kujenga miundombinu ya mchezo na kuimarisha michezo katika ngazi za mikoa na wilaya; kuhakikisha kazi za sanaa na utamaduni zinazoandaliwa zinazingatia maadili ya jamii na Taifa kwa ujumla; na kuendelea kutambua maeneo ya urithi wa utamaduni na ukombozi katika mikoa na halmashauri za wilaya kwa lengo la kulinda, kuhifadhi na kuendeleza maeneo hayo ili kuinua utalii wa kiutamaduni na kiukombozi nchini.

**HITIMISHO**

**190.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea kuratibu utekelezaji wa Sera na shughuli za Serikali ili kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi; kuratibu shughuli za maafa nchini; kuratibu Shughuli za Serikali Bungeni; kushughulikia kero na malalamiko mbalimbali ya wananchi; kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Serikali; na kuratibu masuala yanayohusu Kazi, Maendeleo ya Vijana, Ajira, Hifadhi ya Jamii na Huduma za Watu Wenye Ulemavu.

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** nimeeleza kwa muhtasari baadhi ya shughuli ambazo Serikali imetekeleza kwa kipindi kilichopita na mwelekeo wa kazi zitakazofanyika kwa mwaka 2023/2024. Kwa kuhitimisha, ninapenda kusisitiza mambo muhimu yafuatayo:

**Mosi:** Wizara, Taasisi za Serikali, Tawala za Mikoa na Halmashauri ziimarishe ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma pamoja na kutekeleza wa vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/2024 hususan miradi ya Kitaifa ya Kimkakati;

**Pili:** Wadau wote pamoja na Serikali kwa ujumla waendelee kutumia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 katika shughuli mbalimbali kama vile uwekezaji, biashara, tafiti na mipango mbalimbali ya maendeleo. Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Mwongozo wa Kitaifa wa Matumizi ya Matokeo ya Sensa ili kuongeza uelewa, uwazi na kupanua wigo wa matumizi ya matokeo ya sensa kwa Serikali, wananchi na wadau wote;

**Tatu:** Viongozi wote wa Serikali, dini, mila na Vyama vya Siasa wakemee kwa nguvu zote ushiriki wa sehemu yoyote ya jamii katika matendo yasiyoendana na mila, tamaduni na desturi za Watanzania. Hii ni pamoja na wazazi na walezi wote kushiriki kikamilifu katika makuzi na malezi bora ya watoto yatakayosaidia kuwaepusha na vitendo viovu;

**Nne:** Serikali na Taasisi ziendelee kuhakikisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini yanaendelea kuimarishwa ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi;

**Tano:** Wizara na Taasisi ziendelee kutenga fedha kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji na tathmini katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wataalam wanaotekeleza jukumu hilo. Lengo ni kuwezesha utendaji wenye matokeo na kufanikisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi;na

**Sita:** Viongozi wa siasa, dini na wadau wengine wahamasishe wananchi kushiriki kikamilifu katika maandalizi na uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024.

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2023/2024**

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/2024, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 173,733,110,000**; kati ya fedha hizo, **shilingi 121,364,753,320** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 52,368,356,680** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 165,627,897,000** kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 160,458,877,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 5,169,020,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.





# Moto wateketeza vibanda vya wajasiriamali

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MOTO umeteketeza vibanda zaidi ya 20 vya wajasiriamali eneo la Block T Kata ya Iyela jijini Mbeya, huku Jeshi la Zimamoto na Uokoaji likitupiwa lawama kuchelewa eneo la tukio.

Tukio hilo lilitokea Aprili 5 majira ya saa moja asubuhi na kusababisha hasara kubwa kwa wajasiriamali kutokana na mali zao kuteketea kwa moto.

Akizungumza eneo la tukio, Kasto Sanga alisema kibanda chake kilichokuwa na bidhaa mbalimbali kimeteketea na mali zote hali iliyomsababishia hasara kubwa kwa sababu ni sehemu aliyoitegemea kuendesha maisha yake.

"Mpaka sasa sijui chanzo cha moto huu kumeibua maswali mengi kwa sababu vibanda hivi havijaunganishwa na nishati ya umeme wala mamantilie ambaye tungedhani kwamba amesahau kuzima moto, hivyo kuna kipande cha moto alichokisahau," alisema Sanga.

Francis Ngailo shuhuda wa tukio hilo alisema tangu moto huo ulivyozuka ni zaidi ya saa tatu lakini hakuna gari la zima moto na ukoaji lililofika licha ya kwamba walitoa taarifa.

Kutokana na hali hiyo alilitupia lawama Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuchelewa kufika eneo la tukio kunusuru mali zao na kuteketeza vibanda 26.

"Tangu saa moja asubuhi tumetoa taarifa waje kutusaidia lakini cha ajabu wanakuja saa tatu wakati mali na vibanda vyetu vimeteketea vyote, muda huu ndiyo wamekuja na gari lao,"alisema Ngailo.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara hao, Exavery Msigwa alisema moto huo umeteketeza vibanda 26 kati ya 246.

Alisema huenda vibanda hivyo vimeungua kutokana na kipisi cha sigara ambacho yawezekana kilitupwa na mmoja wa vijana wanaotengeneza sofa eneo hilo.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mbeya, Kondo Mohamed Magoma, alikiri gari la zimamoto kuchelewa kufika eneo la tukio kwa sababu hakukuwa na gari kwenye ofisi hizo.

Alisema baada ya kupata taarifa walilazimika kufuata gari Uwanja wa Ndege wa Songwe kilometa zaidi ya 20 kutoka Mbeya Mjini, hali iliyosababisha kuchelewa kufika eneo la tukio.

Alisema baada ya kufika eneo la tukio walikuta wananchi wakiwa na hasira,i huku wakiwatupia lawama bila kufahamu sababu za kuchelewa.

Alisema: "Tulipata wakati mgumu baada ya kufika eneo la tukio, wananchi walitutolea lugha za kejeli na lawama wakidai ni wazembe tumechelewa kufika eneo la tukio pasipo kujua sababu ya kuchelewa ni nini".



Baadhi ya wajasiriamali wa barabara ya Madaraka, eneo la Block T, jijini Mbeya wakikusanya mabaki ya mabati, baada ya vibanda 26 kuteketea kwa moto juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA.**

## Mwenyekiti H/shauri apiga marufuku uchomaji mkaa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Bosco Mwanginde, amewataka viongozi wa halmashauri hiyo kushirikiana na wananchi kukomesha biashara ya uchomaji mkaa ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Akiwa ameambatana na uongozi wa Halmshauri ya Wilaya ya Chunya juzi walifika katika Kata ya Sangambi kwa ajili ya kujionea uharibifu wa mazingira uliofanywa na wananchi wanaochoma mkaa.

Alisema uharibifu mkubwa wa mazingira umefanyika na kuagiza hatua za haraka zichukuliwe wa wananchi watakaobainika kuhusika na kuwataka viongozi wa vijiji kusimamia sheria ndogo za utunzaji wa mazingira.

"Nadhani kila mmoja amejionea uharibifu wa mazingira katika eneo hili, watu wamekata miti kwa ajili ya kuchoma mkaa, sasa hili halikubaliki tukiendelea kufumbia macho Chunya itakuwa jangwa," alisema Mwanginde.

Akizungumza na wananchi wa Kata ya Sangambi kwenye Kitongoji cha Kambikatoto alisema hataki kuona kuna uchomaji wa mkaa eneo hilo na kwamba ikibainika mwenyekiti au mtendaji wa eneo hilo atawajibishwa.

Diwani wa Kata hiyo, Junjulu Ndete alikiri eneo hilo kuvamiwa na watu wanaochoma mkaa hali ambayo inahatarisha maisha ya binadamu na viumbe hao ambao hutegemea misitu kuishi.

Alisema kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira uliofanywa, alitoa hoja kwenye baraza la madiwani ambao kwa pamoja waliazimia kulisimamia suala hilo ili kunusuru uoto wa asili katika eneo hilo ili kuepukana na ukame

# Watu wenye ulemavu wapewa mafunzo kujikinga na VVU

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), imetoa mafunzo kwa watu zaidi ya 100 wenye ulemavu kwa ajili ya kujengewa uwezo wa namna ya kujikinga na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), uzazi wa mpango na namna ya kuanzisha na kuendesha shughuli zao za ujasiriamali.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, jana alifungua mafunzo hayo na kueleza kuwa nia ni kuhakikisha kundi hilo linathaminiwa katika jamii.

Alisema mafunzo hayo ni miongoni mwa utekelezaji wa majukumu katika kuwahudumia wananchi wakiwamo wenye ulemavu kupatiwa elimu ya afya ya uzazi ili kupunga idadi ya watoto wanaowataka.

"Kiu yangu ni kuona kundi hili linafanikiwa, natamani wajiamini na kutimiza malengo yao bila kujali mapungufu waliyonayo katika miili yao, ulemavu usikwamishe kufanya makubwa kwenye maisha,"alisema Dk. Mbwanji.

Aliongeza kuwa elimu ya ujasiriamali imelenga kuwasaidia kuanzisha miradi mbalimbali na namna ya kuiendesha ili kupata fedha zitakazosaidia kukidhi mahitaji kwenye familia zao.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu mkoani Mbeya (SHIVYAWATA), Damas Mwambeje alisema Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya imekuwa mstari wa mbele katika kulisaidia kundi hilo.

Alisema ni hospitali hiyo imeweka mazingira rafiki ya upatikanaji wa huduma za matatibu kwa watu wenye ulemavu ambapo wameajiri wakarimani.

Aliongeza kuwa mara kwa mara wamekuwa wakijengewa uwezo juu ya masuala mbalimbali ikiwamo utoaji wa huduma za matibabu.

Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Mkoa wa Mbeya, Tusajigwe Mwalwega alisema mafunzo hayo yamewafundisha kujiamini katika kutekeleza majukumu yake bila kujali hali walizonazo.

"Ulemavu siyo ugonjwa, tumejipanga kuhakikisha tunatimiza majukumu yetu ya kila siku, elimu ya afya ya uzazi itatusaidia kuwa huru kupanga muda wa kupata watoto na idadi wanayoitaka sambamba na kukabiliana na magonjwa yanayoambukizwa na yasiyoambukizwa,"alisema Tusajigwe.

Mtaalamu wa elimu ya ujasiriamali ambaye pia ana ulemavu wa macho, Luca Mahenge alisema licha ya kundi hilo kusahaulika kwenye jamii lakini hakukata tamaa katika kutimiza ndoto yake.

Mahenge ambaye pia ni mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Ufundi Iyunga ya jijini Mbeya alisema alianza shughuli za ujasiriamali tangu akiwa darasa la saba ambapo alianzisha mradi wa ufugaji wa simbilisi.

Alisema mpaka sasa ana miliki Taasisi ya TCDI ambayo inatoa elimu ya masuala mbalimbali inayohusu watu wenye ulemavu.



# HABARI ZANZIBAR

## Wawili mbaroni kukutwa na meno ya tembo 45

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kukutwa na meno ya tembo vipande 45.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Naibu Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai, Zuberi Chembere alisema watuhumiwa hao walikamatwa Machi 31 eneo la Fuoni Unguja katika nyumba moja ya kulala wageni.

Alisema watuhumiwa hao ambao majina yake hakuyataja, mmoja ni mkazi wa Bukoba Mkoa wa Kagera akiwa na mwenyeji wake mkazi wa Zanzibar.

Chembere alisema jeshi hilo lilifika katika nyumba hiyo ya kulala wageni (jina limehifadhiwa) wakiwa katika chumba namba 105 wakiwa na vipande hivyo vinavyodhaniwa ni meno ya tembo.

Alisema jeshi hilo lilipata taarifa kuhusu kuingizwa kwa meno hayo kwa kushirikiana na kikosi kazi cha kupambanan na ujangiri Tanzania Bara uliandaliwa mtego na ndipo siku hiyo waliwakamata wakiwa katika harakati za mauziano.

Aidha, alisema uchunguzi wa shauri hilo unaendelea kwa kushirikiana na kikosi kazi cha kupambana na ujangiri Tanzania Bara pamoja na ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar. Alisema uchunguzi utakapokamilika watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani kujibu mashtaka hayo.

"Napenda kutoa wito na onyo kwa wananchi kuacha kujihusisha na vitendo vya kiuhalifu na pia tunawaonya wahalifu wote kwamba Zanzibar sio uchochoro wa kupitisha bidhaa za magendo na zilizopigwa marufuku kwa mujibu wa sheria," alisema Chembere.

Hata hivyo alisema vyombo vya ulinzi na usalama vya baharini na nchi kavu viko macho saa yote kuhakikisha Zanzibar ni shwari na salama.




Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Polisi Zanzibar, Zuberi Chembera akizungumza na waandishi wa habari jijini Zanzibar jana, kuhusu watuhumiwa waliokamatwa na vipande 45 vya meno ya Tembo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Mkataba wasainiwa kusaidia usajili wa watoto kupata vyeti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar imesaini mkataba na Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii wa kusaidia usajili wa watoto kupata vyeti vya kuzaliwa.

Akizungumza jana hafla ya kusaini makubaliano hayo katika ofisi za wizara hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Abeda Rashid Abdullah, alisema wataunda timu ya pamoja na wakala huo kuhakikisha tatizo hilo linapata ufumbuzi.

"Kuna shida ya kuchelewa kuwasajili watoto wengi na kukosa haki zao za kupata vyeti vya kuzaliwa, kwahiyo tumeona kuna haja kuandaa mpango wa pamoja kuhakikisha tunashughulikia tatizo hili", alisema.

Abeida, alisema kuna changamoto ya baadhi ya wazazi kuwa na uelewa mdogo kuhusu umuhimu wa vyeti, hivyo jambo linalowafanya wengine kupuuza lakini hupata changamoto wanapokuwa na mahitaji mengine yanalazimisha mhusika awe na cheti cha kuzaliwa.

Alisema wizara hiyo ndiyo yenye dhamana na watoto wanawajibu kuhakikisha wanatoa elimu kwenye jamii kwa kushirikiana na ngazi zingine wakiwemo masheha.

Hivyo alitumia fursa hiyo kuwataka wazazi kuona umuhimu na kuhakikisha watoto wao wanapatiwa vyeti halisi vya kuzaliwa.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii, Makame Mussa Mwadini, alisema makubaliano hayo ya miaka mitatu yataleta matokeo chanya na kuhakikisha watoto wote ambao hawana vyeti hivyo na wanasifa za kuwa navyo wanavipata.

"Tunataka ifikapo mwaka 2030 pasiwepo na mtu ambaye hana cheti cha kuzaliwa wakati ana sifa zote", alisema.

Mkurugenzi Ustawi wa Jamii na Wazee, Hassan Ibrahim Suleiman, alisema wananchi wengi wamekuwa wakilalamika watoto kukosa vyeti vya kuzaliwa lakini kupitia makubaliano hayo wanaimani watapunguza tatizo hilo kwa kiasi kikubwa.

## Kamati yaridhia utekelezaji wa Wizara ya Kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kilimo, Biashara na Utalii ya Baraza la Wawakilishi, imesema imeridhia utekelezaji wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kupitia Idara ya Kilimo na Misitu kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2022/2023. Mwenyekiti wa kamati hiyo, Yussuf Hassan Iddi, aliyasema hayo baada ya kupokea ripoti za utekelezaji kwa kipindi cha miezi tisa kwa Idara ya Kilimo na Misitu.

Alisema pamoja na mafanikio hayo kuna haja ya wizara kuendelea kupambana katika masuala ya uzalishaji ili malengo ya wananchi kupitia wizara hiyo yafikiwe.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa Idara ya Misitu inapaswa kuendelee kushirikiana na jamii kuhakikisha msitu unaendelea kutunzwa ili kuendeleza hadhi ya uoto wa asili sambamba na kukinga na matukio ya moto na majanga mingine.

"Ushirikiano uliopo uendelee, serikali inapotoa elimu ya kutosha basi wenyewe wanakuwa tayari kutoa taarifa za wahalifu na kufanyiwa kazi haraka inavyowezekana, tunajua ni kazi ngumu lakini msichoke," alisema.

Waziri wa wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis, alisema ushirikiano wa taasisi za serikali pamoja jamii unasaidia uhai wa Msitu wa Hifadhi ya Ngezi kuwepo na kutoa manufaa kwa taifa.

Sambamba na hayo alisema kwa sasa wizara yake imeweka mikakati ya kuyaendeleza mashamba ya serikali yaliyo wazi kwa muda mrefu na kuyatumia kwa shughuli za kilimo ili kuongeza uzalishaji kuhakikisha upatikanaji wa chakula Zanzibar.

Mtendaji wa wizara hiyo, Massoud Bakar Massoud, akiwasilisha ripoti hiyo alisema wizara inatoa mafunzo kwa wafanyakazi na jamii juu ya hifadhi ya msitu, kufanya doria na kutatua migogoro ya eneo la hifadhi kwa kuielewesha jamii mipaka ya eneo hilo.

Alisema pamoja na jitihada zinazoendelea kuulinda msitu huo, kuna matatizo mbalimbali yanayowakabili ikiwemo uhaba wa wafanyakazi, wizi wa miti pamoja na kuchukuliwa kwa eneo katika sehemu ya msitu wa hifadhi ambalo lilitangazwa kuwa ni hifadhi tokea mwaka 1968.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.338 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late MARIAM FIDOLINI ZAMANI**
**and**
**In the matter of Application for letters of administration**
**by**
**MOSES THOMAS MILONGO**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner,
Objections to the grant should be filed on or before the 15th day of 05 2023
Dated at DAR ES SALAAM this 03 day of 04 2023

Senior Resident Magistrate

FORM 58
IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE
AT ONE STOP CENTRE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.338 OF 2023
In the matter of the Estate of the late MARIAM FIDOLINI ZAMANI
and
In the matter of Application for letters of administration
by
MOSES THOMAS MILONGO
GENERAL CITATION
(Rule 75)

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner,
Objections to the grant should be filed on or before the 15th day of 05 2023
Dated at DAR ES SALAAM this 03 day of 04 2023

Senior Resident Magistrate

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

AKIJA MWINJUMA WARIA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya MITSUBISH CANTER yenye usajili namba T 216 DDW, CHASSIS NAMBA: FH21GC551333. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: DAR/KIJ/RB/114921/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

AKIJA MWINJUMA WARIA anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji aina ya BAJAJ TVS KING yenye usajili namba MC 821 AUQ , CHASSIS NAMBA: MD6M14PK1F4A40999. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: DAR/KIJ/RB/114915/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ABDUL TAWABU AHMADA SALUM anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA CROWN yenye usajili namba T 844 DTP , CHASSIS NAMBA: GRS2000022354 na ENGINE NAMBA: 4GR0531427. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: MKB/RB/38/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

SIGHMAN SAFARI HAULAGE LIMITED anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SCANIA yenye usajili namba T 416 DWL, CHASSIS NAMBA: XLER6X20005267865 na ENGINE NAMBA: 6628843. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

SIGHMAN SAFARI HAULAGE LIMITED anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina yaTRAILER yenye usajili namba T 189 DWX, CHASSIS NAMBA: CV72960 . Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: MKB/RB/38/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

SIGHMAN SAFARI HAULAGE LIMITED anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SCANIA yenye usajili namba T670 DVD, ENGINE NAMBA:6600032 . Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: MKB/RB/38/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

SAMWEL ALOYCE NZUKI ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI AINA YA TOYO YENYE NAMBA ZA USAJILI **T296 BEC.** KWA ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA KARIBU CHA POLISI KWA KUTUMIA NAMBA . MORO/MORO/RB 80063/2023

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO........05..........OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE YOHANA KIMWERI MHOMBO**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOA LATER OF ADMINISTRATION**
**BY RASHID ABDALLAH JANI**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be field on or before the 13 day of April 2023
Dated at Korogwe this 23 day of March 2023

DISTRICT COURT KOROGWE

**SHEWAN LIMITED**
**(UNDER VOLUNTARY LIQUIDATION)**
**NOTICE IS HEREBY GIVEN to all CREDITORS and DEBTORS of SHEWAN LIMITED and the GENERAL PUBLIC that SHEWAN LIMITED is undergoing Voluntary Liquidation under the appointed liquidator WILFRED SAWAYA MAWALLA (ADVOCATE).**

All debtors of the company and all persons holding in their possession any asset/properties of the company to pay their debts to the liquidator at the address below not later than 12:00 noon 24th day of March 2023 and to surrender the assets and the said properties to the liquidator at the address below not later than 12:00 noon 24th day of March 2023. All creditors of the company are hereby given notice that they should submit their claims with supporting documents to the liquidator at the address below not later than 12:00 noon 24th day of March 2023 without fail.

**WILFRED MAWALLA (ADVOCATE)**
**THE LIQUIDATOR**
**Mawalla Road Mawalla Heritage Park**
**Mawalla Law Offices Plot No. 175/20**
**Arusha Tanzania P.O. Box 6101**
**Telephone/Facsimile +255 732 972 468**
**Cellular + 255 787050006**
**Electronic mail Wilfred.mawalla@mawalla.co.tz**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

ISSA HARUNA ISSA anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina MOHAMEDI SALIMU NCHASSY namba za usajili MC302CQY aina ya SINORAY.Chassis No. LD3PCK60L2009254. Engine No. SR162FMJ20079254.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/121921/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOSEPH PETER MHILU** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya BOXER yenye namba za usajili MC 165 CJY. Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/117375/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NO.09 LA MWAKA 2020**
**GREEN DIAMOND LIMITED......MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**TATA AFRICA HOLDINGS (T) LTD......MJIBU MAIMBI KWA GREEN DIAMOND LIMITED**

**DAR ES SALAAM.**
**Kuitwa shaurini**

Kwa kuwa Mwombaji aliyetajwa hapo juu, ameleta shauri la maombi ya Madai dhidi yako; Maombi ambayo maelezo yake yamelezwa katika nakala za maombi hayo zinapatikana katika Mahakama hii,
Hivyo basi unahitajika kuhudhuria katika Mahakama hii kupitia Wakili au Mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa kisheria, siku ya tarehe 25/04/2023 saa tatu (3:00) kamili asubuhi mbele ya Mhe.Jaji Kakolaki kujibu maombi haya dhidi yako.
Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo utarajia kutumia kwa ajili ya utetezi siku hiyo.
**ANGALIA**
Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.
HATI hii imetolewa kwa amri yangu na CHAPA ya Mahakama hii leo tarehe 06/04/2023.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU - DAR ES SALAAM**

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701

OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

MOB: +255 - 0677020701

E-mail: advertise@guardian.co.tz, Website: www.ippmedia.com

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## China yarusha makombora anga la Taiwan

**BEIJING,** China

CHINA imeanzisha mazoezi ya kijeshi kama njia ya kujibu mkutano uliotarajiwa kufanyika kati ya Rais wa Taiwan Tsai Ing-wen na Spika wa Bunge la Marekani Kevin McCarthy.

Viongozi hao walikutana jijini California juzi, wiki moja baada ya Rais Tsai kujulishwa kupokea tuzo ya uongozi.

Tsai alisifu ushirikiano wao wenye nguvu na wa kipekee, na McCarthy alijibu kwa kusisitiza mauzo ya silaha kwa Taiwan lazima yaendelee.

Serikali ya China, kwa upande wake, imeapa kutoa jibu la uthabiti na kutuma meli za kivita kwenye maji karibu na kisiwa hicho kinachojitawala.

Wakati wa ziara ya Rais Tsai nchini Marekani, uadui kati ya kisiwa hicho na China unaongezeka.

Kisiwa hicho ambacho China inadai kuwa sehemu ya eneo lake, ndicho kitovu kikubwa cha kutoelewana na Marekani.

Makombora ya China yaliruka juu ya kisiwa hicho huku Beijing ikitoa vitisho vya damu. **BBC**

## Putin azilaumu Marekani, Ulaya

**MOSCOW,** Russia

RAIS wa Russia, Vladimir Putin, ameyatuhumu mashirika ya usalama ya nchi za Magharibi kwa kuisaidia Ukraine kufanya kile alichokiita mashambulizi ya kigaidi nchini mwake.

Kiongozi huyo alisema hayo baada ya kuwapa makaribisho baridi mabalozi wa Marekani na Umoja wa Ulaya nchini humo.

Rais huyo wa Urusi alikuwa akizungumza katika mkutano wa baraza la usalama la Kremlin, lililo na jukumu la kuhakikisha uwepo wa utulivu katika maeneo manne ya Ukraine ambayo anadai kuyazingira mwaka jana. Matamshi hayo ya Putin yanakuja siku chache baada ya kutokea mlipuko katika mgahawa mmoja huko Saint Petersburg uliosababisha kifo cha mwanablogu anayeunga mkono vita vya Ukraine.

Hayo yakiarifiwa Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy amefanya ziara nchini Poland ili kutoa shukrani kwa nchi hiyo kwa kusimama na nchi yake tangu kuanza kwa vita hivyo.

Zelenskiy ameshikilia kwamba nchi bado inaudhibiti mji wa Bakhmut ambao wanajeshi wake wamepambana na mashambulizi ya Russia katika eneo la viwanda la mji huo.

Wakati huo huo, Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, alisema China ina jukumu kubwa la kurejesha amani nchini Ukraine. **DW**

# Iran, Saudi Arabia zaanza mazungumzo ngazi ya juu

**BEIJING,** China

MAWAZIRI wa Mambo ya Nje wa nchi za Iran na Saudi Arabia, wamefanya mazungumzo kwa mara ya kwanza tangu 2016.

Televisheni ya al-Ekhbariya ya Saudi Arabia, ilirusha video fupi ikimuonyesha mwanamfalme Faisal bin Farhan Al Saud na Hossein Amir-Abdollahian wakisalimiana walipokuwa nchini China.

Mwezi uliopita, mataifa hayo mawili yalikubaliana kurejesha uhusiano wa kidiplomasia wakati wa mazungumzo ya ngazi ya chini yaliyofanyika nchini humo.

Saudi Arabia ilikata uhusiano mwaka 2016 baada ya umati wa watu kuvamia ubalozi wake mjini Tehran, nchini Iran.

**Saudi Arabia pia imeishutumu Iran kwa kuwasaidia waasi wa Houthi kuishambulia.**

Kutokana na tukio hilo, Saudi Arabia ililipiza kwa kumnyonga kiongozi mashuhuri wa Kiislamu wa Shia.

Mvutano kati ya Saudi Arabia inayoongozwa na Sunni na Iran inayoongozwa na Shia, tangu siku nyingi umekuwa wa kiwango cha juu.

Mataifa hayo yenye nguvu kila mmoja inatumia nguvu ya vitisho kutafuta utawala wa kikanda.

Pia wanaunga mkono pande zinazohasimiana katika Mashariki ya Kati, ikiwa ni pamoja na Lebanon, Syria, Iraq na Yemen.

Huko Yemen, nchi ya Iran inaunga mkono waasi wa Shia wa Houthi walioiondoa serikali inayoungwa mkono na Saudi Arabia mwaka 2014. Saudi Arabia pia imeishutumu Iran kwa kuwasaidia waasi wa Houthi kuishambulia.

Katika tukio baya zaidi la aina yake, ndege zisizo na rubani na makombora zilishambulia vituo vikubwa vya mafuta vya Saudia mnamo 2019, na kusababisha uharibifu na usumbufu wa uzalishaji.

Saudi Arabia na mshirika wake Marekani waliilaumu Iran kwa shambulio hilo, jambo ambalo Iran ilikanusha.

Majaribio ya awali ya upatanisho hayakufaulu, lakini mwezi uliopita nchi hizo mbili zilisema zitafungua tena balozi ndani ya miezi miwili.

Pia walisema uhusiano wa kibiashara na usalama utaanzishwa upya.

Marekani ilikaribisha tangazo hilo kwa tahadhari, huku Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres akiishukuru China kwa kufanikisha makubaliano hayo. **BBC**



Mawaziri wa Mambo ya Nje, mwanamfalme Faisal bin Farhan Al Saud wa Saudi Arabia na Hossein Amir-Abdollahian kutoka Iran wakisalimiana wakati wa mkutano wao nchini China. **PICHA: REUTERS**

# Mahakama yaamuru jogoo kuchinjwa baada ya majirani kukosa usingizi

**ABUJA,** Nigeria

MAHAKAMA moja nchini Nigeria, imeamuru kuchinjwa kwa jogoo baada ya malalamiko ya majirani ambao walidai anaharibu mazingira kwa kupiga kelele.

Vyombo vya habari vya nchini humo vimeripoti kuwa mahakama katika mji wa Kano, ilitangaza jogoo huyo kuwa kero katika mtaa huo baada ya kuwika mara kwa mara.

Majirani wawili walisema kuwa walishindwa kupata usingizi kutokana na kelele za jogoo huyo.

Kulingana na tovuti ya Premium Times, mmoja wa majirani hao, Yusuf Muhammed, aliiambia mahakama kuwa kuwika kwa jogoo bila kuchoka ni kukiuka haki yake ya kupata usingizi mwanana.

Hata hivyo, mmiliki wa jogoo huyo, Isyaku Shuaibu, aliambia mahakama kwamba alinunua kuku huyo kwa ajili ya sherehe za Ijumaa Kuu, na akaomba apewe muda hadi siku kuu hiyo ndipo atamchinja kwa ajili ya familia yake.

Hakimu Halima Wali, alikubali ombi hilo lakini aliimuonya kuzuia jogoo huyo kuzurura eneo hilo na kuwasumbua wakazi.

Mmiliki huyo pia aliamriwa kuhakikisha anamchinja kuku huyo siku ya Ijumaa kama alivyoahidi au atakabiliwa na adhabu. **BBC**

# BETWAY YAPANIA KUKUZA SOKA NCHINI, YATOA VIFAA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Michezo ya Kubashiri ya Kimataifa, Betway Tanzania imezindua rasmi programu ya kutoa vifaa vya michezo kwa timu za soka za mtaani.

**Lengo la programu hiyo ni kusaidia maendeleo ya michezo nchini kwa kutoa vifaa kwa timu za soka ngazi ya chini itashuhudia klabu za mtaani zikikabidhiwa mipira, jezi pamoja na soksi.**

Baada ya kukabidhiwa vifaa hivyo timu hizo zitashindana katika michezo ya 'Kombe la Mbuzi' ambayo pia imeandaliwa na Betway Tanzania kama sehemu ya programu hiyo.

Zoezi la ugawaji wa vifaa vya michezo limezinduliwa Dar es Salaam mapema mwezi huu ambapo timu mbili kutoka wilaya ya Kinondoni zimeshakabidhiwa jezi na kuingia katika mashindano ya Kombe la Mbuzi.

Ofisa Uendeshaji wa Betway Tanzania, Jimmy Masaoe, amesema uamuzi wa kampuni hiyo kuangazia soka la mtaani ni sehemu ya kutoa mchango wake kwa jamii katika kukuza maendeleo ya sekta ya michezo nchini.

"Programu hii inaitwa Kits for Africa katika ngazi ya bara la Afrika. Katika programu hii Betway inatoa vifaa kwa timu za mtaani ili kusisimua michezo katika ngazi ya chini kwani huko ndiko ambako vipaji vinakozaliwa. Kwa hapa Tanzania, programu hii pia itakuwa na mchango mkubwa katika kuongeza thamani ya michezo katika ngazi za mitaa.

Tumeamua kwenda kufanya zoezi la kugawa vifaa katika vibanda vya kuonyesha michezo maarufu kama vibanda umiza na kufanya mashindano ya Kombe la Mbuzi katika viwanja vya mtaani kabisa ili kugusa vipaji vya mtaani moja kwa moja," alisema Masaoe.

Aliongeza anaamini hatua hiyo itaongeza motisha pamoja na kuwaunganisha wanamichezo na mashabiki wa michezo wa mpira wa miguu huku wakiamsha ari ya maendeleo ya mchezo huo.

Uzinduzi wa programu hii umefanyika Tegeta, Dar es Salaam ambapo timu mbili zilipata vifaa vya michezo pamoja na kushinda mbuzi.

Wabishi FC kutoka Tegeta na Geneva FC kutoka Bunju ndizo hupokea vifaa vya michezo na katika mechi ya uzinduzi, Wabishi FC waliwafunga Geneva FC mabao 2-1.

Nahodha wa Wabishi FC, Selemani Agustin, ameipongeza Betway Tanzania kwa mpango wake huo ambao utasaidia kuwahamasisha watu wengi kushiriki katika shughuli za michezo na kuwasaidia kuimarisha afya.

"Huu ni mpango mzuri unaowaunganisha wapenda michezo katika ngazi za mitaa na kuhamasisha watu wengi zaidi kushiriki katika michezo. Wakati mwingine, timu yetu inashindwa kuingia katika mashindano mbalimbali kutokana na ukosefu wa vifaa vya michezo, hivyo msaada huu kutoka kwa Betway ni muhimu sana kwetu."




Kikosi cha Wabishi FC cha Tegeta, Dar es Salaam baada ya kuibuka washindi wa mechi ya ufunguzi wa michuano ya Kombe la Mbuzi wakiwa na zawadi yao ya mbuzi wawili kutoka kwa wawakilishi wa Betway Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Azam FC, Mtibwa vitani Bara

**Na Saada Akida**

BAADA ya siku 23 kutochezwa kwa Ligi Kuu Tanzania kutocheza, kikosi cha Azam FC kinashuka kuwakabili Mtibwa Sugar katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Aggrey Morris, amesema maandalizi kuelekea mechi hiyo yanaendelea vizuri na anaamini mchezo utakuwa na ushindani kwa sababu ya ugumu wa wapinzani wao kila wanapokutana nao.

"Kikosi kipo vizuri na hatuna majeruhi lakini tutafanya mabadiliko katika timu kwa kuwapumzisha baadhi ya wachezaji na kuwapa nafasi ambao hawakuonekana uwanjani mara kwa mara," alisema kocha huyo.

Nahodha wa Azam FC, Bruce Kangwa, alisema mechi itakuwa ngumu kwa sababu Mtibwa Sugar watakuja kivingine tofauti na walivyokutana katika mechi iliyopita na kuibuka na ushindi.



"Mechi ya FA imeshapita na hii ni nyingine wapinzani wetu watakuwa wamejiandaa vizuri na kufanyia makosa yao ninaimani hawatakuwa Mtibwa Sugar wale tuliokutana nao, tutacheza kwa nidhamu kubwa ili kupata pointi tatu nyumbani," alisema Kangwa.

Naye Kocha Msaidizi wa Mtibwa Sugar, Awadhi Juma, alisema wataingia tofauti na walivyoingia katka mechi iliyopita ya Kombe la FA ambayo walipoteza.

# Simba Queens safi, Yanga Princess hoi

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake, Simba Queens wameendelea kujiimarisha baada ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya timu ngumu ya Fountain Gate Princess katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, huku watani wao wa jadi, Yanga Princess wakiangukia pua kwa kufungwa bao 1-0 dhidi ya Alliance Girls iliyokuwa nyumbani Mwanza.

Maafande wa JKT Queens wamekwea kileleni mwa msimamo kwa kuiengua Fountain Gate Princess baada ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ceasiaa Queens, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni Dar es Salaam.

Kama ilivyotegemewa, ilikuwa mechi ngumu kwa pande zote mbili na haikuwa rahisi kwa mashabiki kutabiri nani anaweza kuibuka na ushindi.

Iliwachukua wenyeji dakika 18 tu kupachika bao pekee ambalo liliwapeleka kifua mbele hadi kipindi cha kwanza kilipomalizika.

Simba Queens waliamka dakika 70 kwa kufunga goli la kusawazisha kwa penalti, iliyowekwa wavuni na Mkenya, Jentrix Shikangwa.

Bao hilo lilimfanya Shikangwa kufikisha magoli 11 kwenye kibindo chake, akiwa ndiye kinara wa kupachika mabao mpaka sasa kwenye Ligi Kuu.

Dakika sita kabla mechi kumalizika, Ruth Ingosi, mchezaji mwingine kutoka Kenya aliyesajiliwa pamoja na Shikangwa kipindi cha usajili wa dirisha dogo, alipachika mpira wavuni, akiandika bao la pili na muhimu kwenye kikosi cha Simba Queens.

Kwa matokeo hayo, Simba Queens inachupa kutoka nafasi ya tatu hadi ya pili ikiwa na pointi 30, huku Fountain Gate Princess iliyokuwa kileleni imeporomoshwa hadi nafasi ya tatu, ikisalia na pointi 29.

JKT Queens kwa sasa ipo kileleni katika ligi hiyo ikiwa na pointi 31, baada ya juzi kuichapa Ceasiaa Queens mabao 2-0.

Bao pekee lililofungwa na Elizabeth John dakika ya 28 lilitosha kuipa ushindi Alliance Girls na kuwaweka katika nafasi ngumu ya kutwaa taji la kwanza Yanga Princess ambayo sasa iko kwenye nafasi ya nne na pointi 22 wakati Alliance Girls inafuatia ikiwa na pointi 20.

Mechi nyingine ya ligi hiyo ilichezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha kwa The Tigers Queens kukubali kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Baobab Queens ya Dodoma.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MADDISON KUUZWA

KLABU ya Leicester inatazamiwa kutaka kupewa takriban pauni milioni 50 kumuuza kiungo mshambuliaji wa England, James Maddison, huku Tottenham Hotspur wakipewa nafasi kubwa ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Telegraph)***

### MESSI KUPEWA HISA

INTER Miami iko tayari kumpa mshambuliaji wa Paris St-Germain na Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 35, hisa za usawa katika klabu hiyo ili kumshawishi ajiunge msimu huu wa joto. ***(Independent)***

### ALONSO AIWANIA CHELSEA

KOCHA wa klabu ya Bayer Leverkusen ya Hispania, Xabi Alonso ameibuka kuwania nafasi ya kuinoa Chelsea baada ya Graham Potter kutimuliwa. ***(Guardian)***

### TIELEMANS ASAKWA

KLABU ya Arsenal imeanza mazungumzo na kiungo wa Leicester City na Ubelgiji, Youri Tielemans, 25. Newcastle United na Barcelona pia wanavutiwa na mchezaji huyo. ***(Football Insider)***

### KANTE MKATABA MPYA

CHELSEA imeanza mazungumzo na kiungo wa kati wa Ufaransa, N'Golo Kante, 32, kuhusu mkataba mpya. ***(Fabrizio Romano)***

### O'NEILL AWANIWA

KLABU ya Leicester City inamfikiria kocha mwenye uzoefu kama vile Martin O'Neill au Rafa Benitez kuchukua nafasi ya Brendan Rodgers hadi mwisho wa msimu. ***(Independent)***

### MAKOCHA ZAIDI

LEICESTER City imemtaja Graham Potter aliyetimuliwa Chelsea hivi majuzi, na kocha wa Brentford, Thomas Frank kama walengwa wa majira ya joto, huku kocha wa zamani wa Southampton, Ralph Hasenhuttl na Jesse Marsch aliyewahi kuichezea Leeds, pia akitajwa. ***(Sky Sports)***

### HUTTER NAE ATAJWA

KOCHA wa zamani Borussia Monchengladbach, Adi Hutter pia anaweza kuwa chaguo kwa Leicester. ***(Mail)***

### HANSEN ATAKIWA BURNLEY

KLABU ya Burnley inataka kumsajili winga wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Sontje Hansen, 20, msimu huu wa joto. ***(Football Insider)***


### NELSON MKATABA MPYA

ARSENAL Iko kwenye mazungumzo na wawakilishi wa Reiss Nelson, 23, kuhusu kuongeza mkataba wa mshambuliaji huyo wa England. ***(Fabrizio Romano)***

### LIVERPOOL KUMWAGA MPUNGA

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema klabu hiyo imekuwa na shughuli nyingi wakati wa mapumziko ya kimataifa ikipanga malengo ya msimu wa joto na iko tayari kutumia fedha nyingi katika soko la usajili. ***(Mirror)***

## DON… A SOKA MAGA… ULAYA




# RASHFORD: MAN UNITED ITARUDI KWENYE MSTARI

**MANCHESTER,** England

MARCUS Rashford anatamani kuona Manchester United ikirudi katika kiwango chake baada ya kurejea kwenye njia ya ushindi dhidi ya Brentford hapo juzi.

**Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alifunga bao pekee katika mchezo huo na kujipatia ushindi kwenye Uwanja wa Old Trafford na kumaliza msururu wa michezo mitatu bila ushindi katika Ligi Kuu England.**

United baada ya kushinda Kombe la EFL, ikaambulia kipigo cha aibu cha mabao 7-0 kutoka kwa Liverpool na kupoteza kwa Newcastle United na sare dhidi ya Southampton.

Kikosi cha Erik ten Hag kilikuwa na matokeo bora zaidi katika mashindano ya kombe hilo, kikisonga mbele katika Kombe la FA na Ligi ya Europa, lakini kushuka kwa kiwango katika Ligi Kuu England kulisababisha wasiwasi katika kusaka nafasi ya nne bora.

Kwa kuwa sasa kikwazo kimoja kimeondolewa na Rashford ana nia ya kuongeza kasi na kumaliza msimu akiwa juu.

"Tuko katika kipindi hicho cha msimu ambapo kila mchezo ni muhimu na tuna furaha kushinda na tunatumaini tunaweza kurejea tulipokuwa wiki chache zilizopita," alisema akiiambia BBC Sport.

"Kitu muhimu siku zote ni kushinda mchezo unaofuata, kila mmoja yuko wazi kuwa hatutacheza vyema kila wiki, lakini hakuna wakati wa kushuka viwango vyetu na tunatakiwa kuendelea kusukumana kila wiki.

"Tulikuwa na subira zaidi kutokana na kumiliki mpira; tulingoja hali ifaayo ili kushinikiza kupata ushindia.

"Tulikuwa watulivu na tuliendelea kuwasiliana kujaribu kuwazuia wachezaji wao wa kushambulia."

Ushindi wa United unawafanya kurejea juu ya Tottenham na kushika nafasi ya nne, wakiwa na pointi tatu mbele na kuwa na mchezo mkononi dhidi ya timu hiyo ya kaskazini mwa London, huku Rashford akielekeza nguvu zake kuhakikisha wanafuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

"Hilo ndilo lengo - tunataka kupata pointi nyingi kadri tuwezavyo na tutajaribu na kushinda kila mchezo," aliongeza.

"Lazima tuendelee kucheza vyema na kujituma vyema, tuendelee kujirekebisha vizuri na kusonga mbele kwa mechi inayofuata."

●●● Hilo ndilo lengo - tunataka kupata pointi nyingi kadri tuwezavyo na tutajaribu na...

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,099,1
MECHI KALI
AZAM
VERSUS
MTIBWA SUGAR
1 | 1.37
X | 4.11
2 | 7.25
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa · vodacom m-pesa · halopesa · airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# LAMPARD AKARIBIA KUREJEA CHELSEA

**LONDON,** England

FRANK Lampard anaonekana kukaribia kurejea Chelsea kama kocha wa muda hadi mwisho wa msimu huu.

Ripoti zinaonyesha kocha huyo wa zamani wa Everton yuko mbioni kutia saini tena kipindi chake cha pili cha kuinoa Stamford Bridge, ambacho kinaweza kuja kwa wakati wa mechi dhidi ya Wolves itakayochezwa kesho.

Lampard mwenye umri wa miaka 44 alikuwa uwanjani kushuhudia sare dhidi ya Liverpool Jumanne iliyopita, mechi ya kwanza kwa Chelsea tangu Graham Potter atimuliwe.

Potter alionyeshwa mlango wa kutokea Jumapili iliyopita baada ya kushindwa kwa mabao 2-0 na Aston Villa na kuiacha timu yake ikiwa nafasi ya 11 katika msimamo wa Ligi Kuu England.

Lampard, ambaye aliichezea klabu hiyo kati ya mwaka 2001 na 2014, alipata kazi ya ndoto yake kama kocha wa Blues Julai, mwaka 2019, lakini akafukuzwa miezi 18 baadaye.

Aliendelea kuchukua jukumu kule Goodison Park kabla ya kuondolewa Januari baada ya kuwa kocha chini ya mwaka mmoja.

Luis Enrique, ambaye inasemekana alisafiri kwa ndege kwenda London juzi kukutana na viongozi wa klabu hiyo na Julian Nagelsmann, aliyefutwa kazi hivi majuzi na Bayern Munich, wanahusishwa na kazi hiyo.



# Ancelotti: Madrid ilikuwa na kiwango bora kwa Barca

**BARCELONA,** Hispania

CARLO Ancelotti anaamini Real Madrid ilicheza "mechi bora" baada ya ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Barcelona kwenye Uwanja wa Camp Nou na kujihakikishia nafasi ya kucheza fainali ya Copa del Rey kwa ushindi wa jumla wa 4-1.

Madrid walikabiliwa na kibarua kigumu kuelekea nyumbani kwa wapinzani wao wa Clasico, ambao wanaongoza kwa pointi 12 dhidi ya vijana wa Ancelotti kwenye kilele cha LaLiga, wakikabiliwa na upungufu wa bao moja baada ya bao la kujifunga la Eder Militao lililoipa Barca ushindi wa 1-0 katika mchezo wa kwanza uliochezwa Bernabeu.

Lakini Vinicius Junior alisawazisha bao hilo kabla ya mapumziko na Karim Benzema akafunga hat-trick kipindi cha pili na kuiongoza Madrid kuibuka na ushindi mnono na kutinga fainali dhidi ya Osasuna itakayochezwa Mei 6, mwaka huu.

Ancelotti alifurahishwa na ushujaa wa mkondo wa pili wa timu yake, akiwaambia waandishi w habari katika mkutar wake baada ya mech "Ulikuwa mchezo kami Unaposhinda 4-0 hapa jambo zuri sana.

"Tulicheza mchez mzuri. Bao la kwanza lili adilisha kila kitu, tulipa nafasi zaidi katika mabad liko. "Ilikuwa ngumu kid go mwanzoni, lakini katil kipindi cha pili tulifany vizuri sana. Hatukuogop waliposhinikiza na tuliju jinsi ya kutumia nafasi k tika mabadiliko.

"Tulicheza mechi k mili."

## HABARI MICHEZO

164,188/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 08/04/23 | 17:00 | Fulham FC vs West Ham United | 2.55 | 3.15 | 2.60 |
| 02. 08/04/23 | 17:30 | Sampdoria Genoa vs US Cremonese | 2.24 | 3.10 | 3.10 |
| 03. 08/04/23 | 19:30 | Hellas Verona vs Sassuolo Calcio | 2.50 | 3.10 | 2.70 |
| 04. 08/04/23 | 19:30 | Torino FC vs AS Roma | 3.15 | 2.95 | 2.31 |
| 05. 08/04/23 | 21:45 | Lazio Rome vs Juventus Turin | 2.60 | 2.90 | 2.80 |
| 06. 08/04/23 | 21:45 | KAA Gent vs Union Saint-Gilloise | 2.46 | 3.35 | 2.60 |
| 07. 09/04/23 | 14:00 | Olympique Lyon vs Stade Rennes | 2.25 | 3.30 | 2.90 |
| 08. 09/04/23 | 15:00 | Real Valladolid vs RCD Mallorca | 2.47 | 2.90 | 2.95 |
| 09. 09/04/23 | 15:30 | FC Emmen vs NEC Nijmegen | 2.80 | 3.30 | 2.35 |
| 10. 09/04/23 | 16:00 | AC Ajaccio vs AJ Auxerre | 2.70 | 2.90 | 2.65 |
| 11. 09/04/23 | 16:00 | Montpellier HSC vs Toulouse FC | 2.28 | 3.40 | 2.80 |
| 12. 09/04/23 | 16:00 | ESTAC Troyes vs Clermont Foot 63 | 2.55 | 3.20 | 2.60 |
| 13. 09/04/23 | 16:30 | Borussia Monchengladbach vs VfL Wolfsburg | 2.26 | 3.50 | 2.75 |
| 14. 09/04/23 | 18:30 | Liverpool FC vs Arsenal FC | 2.46 | 3.45 | 2.55 |
| 15. 09/04/23 | 18:30 | VfL Bochum vs VfB Stuttgart | 2.85 | 3.20 | 2.34 |
| 16. 09/04/23 | 19:30 | UD Almeria vs Valencia CF | 2.75 | 3.15 | 2.43 |
| 17. 09/04/23 | 19:30 | Standard Liege vs KRC Genk | 2.70 | 3.45 | 2.32 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 07/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4624 | Nacional Madeira vs Oliveirense | 2.26 | 3.17 | 2.97 |
| 14:30 | 3065 | Millwall vs Luton Town | 2.47 | 2.95 | 2.90 |
| 15:00 | 5105 | Vorskla Poltava vs FC Ingulets | 2.01 | 3.19 | 3.34 |
| 15:00 | 5629 | Rotherham vs West Bromwich | 4.40 | 3.40 | 1.76 |
| 15:00 | 5889 | Saint George FC vs Sidama Bunna SC | 1.34 | 4.87 | 6.84 |
| 16:00 | 3503 | FK Radnicki 1923 vs Radnicki Nis | 2.25 | 2.98 | 3.03 |
| 16:00 | 4074 | Gais vs IK Brage | 2.07 | 3.41 | 3.41 |
| 16:00 | 5037 | Singida BS FC vs Polisi Tanzania | 1.41 | 3.83 | 7.07 |
| 16:00 | 5411 | Gabala vs Zira | 2.25 | 2.95 | 3.15 |
| 16:30 | 2447 | Persik Kediri vs PS Tni | 1.90 | 3.34 | 3.50 |
| 16:30 | 2796 | Persepam MU vs Arema | 2.15 | 3.18 | 3.03 |
| 16:30 | 5913 | PSS Sleman vs Bali Utd Pusam | 2.90 | 3.35 | 2.02 |
| 17:00 | 1333 | Stoke City vs Bristol City | 1.77 | 3.55 | 4.10 |
| 17:00 | 1480 | Blackburn vs Norwich City | 2.76 | 3.11 | 2.46 |
| 17:00 | 2313 | Blackpool vs Cardiff | 2.70 | 3.05 | 2.55 |
| 17:00 | 2344 | Reading vs Birmingham | 2.76 | 2.91 | 2.61 |
| 17:00 | 2935 | Watford vs Huddersfield | 1.68 | 3.45 | 4.90 |
| 17:00 | 3386 | Sheffield Utd vs Wigan | 1.47 | 4.01 | 6.21 |
| 17:00 | 3731 | Swansea vs Coventry | 2.22 | 3.26 | 3.01 |
| 17:00 | 5970 | QPR vs Preston | 2.27 | 3.10 | 3.05 |
| 18:00 | 4274 | Arba Minch Kenema vs Mekelakeya | 2.65 | 2.91 | 2.65 |
| 18:00 | 4654 | Backa Topola vs Vojvodina | 1.94 | 3.24 | 3.49 |
| 18:00 | 4912 | Salernitana vs Inter | 6.39 | 4.39 | 1.42 |
| 18:30 | 1543 | Santa Clara vs FC Vizela | 3.57 | 3.27 | 2.00 |
| 19:00 | 4871 | Azam vs Mtibwa Sugar | 1.37 | 4.11 | 7.25 |
| 19:30 | 2552 | Sunderland vs Hull City | 1.97 | 3.31 | 3.56 |
| 19:30 | 4512 | Lugo vs Tenerife | 3.99 | 3.15 | 1.92 |
| 20:00 | 1097 | Lecce vs Napoli | 5.15 | 3.39 | 1.66 |
| 20:00 | 2997 | Benfica vs Porto | 1.91 | 3.47 | 3.67 |
| 20:30 | 1080 | Dinamo Bucuresti vs FC Otelul Galati | 2.24 | 2.93 | 3.09 |
| 20:30 | 4085 | Konyaspor vs Antalyaspor | 1.98 | 3.42 | 3.48 |
| 20:30 | 5480 | SuperSport Utd vs TS Galaxy FC | 1.79 | 3.09 | 4.82 |
| 21:00 | 2256 | NAC Breda vs Den Bosch | 1.49 | 4.28 | 5.22 |
| 21:00 | 2968 | Groningen vs Utrecht | 3.16 | 3.31 | 2.12 |
| 21:00 | 3995 | Jazira Abu Dhabi vs Al Nasr Dubai | 1.71 | 3.55 | 4.12 |
| 21:00 | 4563 | Almere City vs Jong AZ Alkmaar | 1.49 | 4.10 | 5.61 |
| 21:00 | 4898 | Telstar vs Jong Ajax | 2.04 | 3.49 | 3.13 |
| 21:00 | 5719 | Dordrecht vs Jong PSV | 2.97 | 3.28 | 2.21 |
| 21:45 | 1325 | Brugge vs RFC Seraing | 1.11 | 8.06 | 17.12 |
| 21:45 | 4468 | St Patricks vs Cork City | 1.75 | 3.38 | 4.10 |
| 21:45 | 4803 | Bohemians FC vs Shamrock Rovers | 3.34 | 3.24 | 1.99 |
| 21:45 | 4892 | Partick Thisle vs Queens Park | 2.06 | 3.34 | 3.24 |
| 21:45 | 4960 | Dundalk FC vs Sligo Rovers | 2.29 | 2.92 | 3.02 |
| 22:00 | 1052 | Lens vs Strasbourg | 1.42 | 4.29 | 6.59 |
| 22:00 | 1116 | Middlesbrough vs Burnley | 2.55 | 3.26 | 2.55 |
| 22:00 | 1222 | Al Shabab Riyadh vs Al Hilal Riyadh | 2.72 | 3.62 | 2.35 |
| 22:00 | 2629 | Villarreal B vs Malaga | 2.01 | 3.25 | 3.50 |
| 22:00 | 3200 | Sevilla FC vs Celta Vigo | 2.12 | 3.26 | 3.21 |
| 22:00 | 5576 | AC Milan vs Empoli | 1.37 | 4.58 | 7.17 |
| 22:30 | 4146 | Boavista vs Vitoria Guimaraes | 2.48 | 3.06 | 2.81 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# CAG AANIKA MADUDU UWANJA UHURU, MKAPA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amebaini kuwapo na utendaji usioridhisha wa viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru, unatokana na matengenezo yasiyotosheleza, usimamizi duni, na ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya matengenezo.

**Kichere ametahadharisha hali hiyo itakayoleta athari kubwa katika mapato, ushiriki wa mashabiki na utendaji wa timu.**

CAG amependekeza Menejimenti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuweka mpango wa matengenezo na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa usalama ili kuboresha usalama wa viwanja, kuvifanya vidumu miaka mingi na kuokoa upotevu wa mapato.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana kuhusu ripoti hiyo 2021/22, Kichere alisema ujenzi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa ulikamilika mwaka 2007 na kuanza kufanya kazi tangu mwaka huo, wakati Uwanja wa Uhuru ulijengwa mwaka 1959 na kukamilika mwaka 1960 na matengenezo makubwa yalifanywa mwaka 2016.

Hata hivyo, alisema amebaini mapungufu kadhaa kuhusiana na utendaji wa viwanja ambayo yanahitaji usimamizi wa menejimenti.

"Miundombinu na vifaa duni, viti vimevunjika na havijarekebishwa, hii inaweza kuwakatisha tamaa mashabiki kuhudhuria mechi na inaweza kuathiri mapato na nimebaini hali isiyoridhisha kuhusu miundombinu ya choo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa," alisema Kichere.

Alisema matengenezo yasiyotosheleza, uangalizi duni wa uwanja kutokana na kutokuwepo kwa mpango wa matengenezo wa mali ambao umesababisha usalama kuwa mdogo kwa sababu viyoyozi havifanyi kazi vizuri na usambazaji wa maji na mfumo wa usafi haukufanya kazi kwa njia inayoridhisha.

"Nimebaini taratibu za kiusalama hazifanyi kazi kwenye mfumo wa utambuaji wa moto na mfumo wa tahadhari (alarm system) katika Uwanja wa Benjamin Mkapa huku mfumo wa kuzima moto kwa maji haufanyi kazi kwa Uwanja wa Uhuru," aliongeza.

## Simba, Ihefu

INATOKA UK. 24

kuwapeleka kwa mkopo nyota hao wawili, wote raia wa Nigeria baada ya kuonekana hawana nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Wekundu wa Msimbazi.

Naye Kocha Msaidizi wa Ihefu, Zuberi Katwila, alisema wamewaandaa wachezaji wao vyema kuelekea mechi hiyo na anaamini watavuna matokeo bora.

Katwila alisema nyota wao wako kamili kiufundi na kisaikolojia kukutana na Simba na kutamba 'wembe' waliotumia kuwanyoa Yanga na Azam huenda pia ukawageukia Simba.

Baada ya mechi ya leo, Simba itasafiri kuifuta Ihefu katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Aprili 10, mwaka huu kwenye Uwanja wa Highland Estates ulioko Mbarali.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Zainab Mohamedi 'Dudu' (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Fountain Gate Princess katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma juzi. Simba ilipata ushindi wa mabao 2-1. **PICHA: SIMBA SC**

## *Simba, Yanga SC na mechi za kiumeni*

INATOKA UKURASA 24

"Ninaimani Rivers United ya sasa sio ile tuliyokutana nayo mwaka jana, itakuwa timu tofauti, tunaamini sisi wenyewe tunauwezo kupambana kufanya vizuri katika michezo yote miwili kwa sababu tunataka kusonga mbele," alisema Kaze.

Rais wa Yanga, Hersi Said, alisema klabu imeongeza kitita cha bonasi kwa wachezaji wa timu hiyo endapo watasonga mbele katika michuano hiyo ya kombe la Shirikisho Afrika.

Hersi alisema baada ya kumfahamu mpinzani wao sasa wanatarajia kufanya kikao na benchi la ufundi kwa ajili ya kuweka mipango kuelekea mechi hiyo ili malengo yao ya kutinga nusu fainali ambayo kila Mwanayanga anahitaji kuona yatimie.

"Tumefurahi kupangwa na Rivers United, naomba niwahakikishie Wanayanga, tutawapiga kwao Nigeria na hapa nyumbani tutawapiga," alisema Hersi.

Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, alisema sasa wanaenda kulipa kisasi katika mechi hiyo.

"Tuliowasubiri tumekutana nao, tunaenda kulipa kisasi, mwaka jana walituondoa, sasa tunarudi uwanjani kufanyia kazi madhaifu yetu kwa ajili ya mechi hiyo, hatutarudia makosa," alisema Mayele.

Michezo
Ijumaa Aprili 7, 2023
Nipashe




'Man Utd itarudi kwenye mstari' UKURASA 21

# SIMBA SC, YANGA NA MECHI ZA KIUMENI

## Vigogo hao wa soka nchini watamba historia bora...

Adam Fungamwango na Saada Akida

BAADA ya droo ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika kutoka hapo juzi, makocha wa Simba na Yanga wametamba msimu huu ni wa timu za Tanzania kuweka heshima katika michuano hiyo.

**Simba inayoshiriki Ligi ya Mabingwa Afrika itakutana na Waarabu wa Morocco, Wydad Casablanca na itaanzia nyumbani Aprili 21 na 23, mwaka huu na wataenda kurudiana wiki moja baadaye wakati Yanga inayochuana katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakutana na Rivers United ya Nigeria.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' alisema hakuna mchezo mwepesi katika mashindano ya Ligi yaMabingwa Afrika na hasa ikifika hatua ya robo fainali.

Robertinho alisema kikosi chake kiko tayari kupambana na Waarabu hao na anaamini wachezaji wanafahamu malengo ya kusonga mbele ya timu yao.

"Sio mechi rahisi, tunatakiwa kujipanga na kutumia mechi tunazocheza za nyumbani kujiweka vizuri kwa ajili ya maandalizi ya mechi yetu hiyo dhidi ya Waydad ambao ni mabingwa watetezi," alisema Robertinho na aliongeza;

Kwanini tusiende nusu fainali kama tunajipanga vizuri, wachezaji wakiwa makini na kufuata maelekezo tuliyowapa, ninaimani kubwa ya kombinesheni ya wachezaji akiwamo Chama (Clatous), Saido (Ntibazonkiza)," alisema kocha huyo.

Aliongeza kabla ya mechi yao dhidi ya Wydad, watakuwa na mechi tatu mkononi za nyumbani ambazo zote anahitaji kupata matokeo mazuri.

"Baada ya mechi hizo tutacheza mechi yetu ya dabi dhidi ya Yanga, pia tunahitaji kupata ushindi na kutumia michezo yote hiyo kufanyia kazi makosa yao ikiwamo mashambulizi ya kushtukiza, ikiwa ni maandalizi ya kuwakabili Wydad hapa nyumbani," alisema kocha huyo.

Aliongeza ni faida kubwa kuanza kucheza nyumbani kwa sababu wanahitaji kutumia vizuri uwanja wa nyumbani kwa kutafuta ushindi katika mechi hiyo kabla ya kwenda kumalizia majukumu ugenini.

"Tumepangiwa mpinzani mgumu, nikisema mgumu nina maana halisi ya ugumu, ni timu ambayo imetuzidi kwa kila kitu, kuna dakika 90 za soka ambazo mara nyingi huwa hazijali sana hilo, badala yake zinaangalia timu imejipanga vipi kwa mchezo husika na kama sisi tutajipanga vizuri, kumbuka miaka 20 iliyopita Simba iliwatoa mabingwa watetezi wa Kombe la Afrika (Zamalek), wakiwa kwao, enzi za kina, Juma Kaseja, tunataka kurudia historia ile," alisema Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally.

Naye Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema wanawafahamu wapinzani wao vizuri na anaimani timu zote zilizofika hatua ya robo fainali ni nzuri lakini sasa rasmi wanaanza kujiandaa kuwakabili Rivers United.

Kaze alisema watakuwa makini zaidi katika mechi zote mbili kwa sababu wanakutana na timu ambayo msimu uliopita iliwaondoa katika mashindano hayo ya CAF.

INAENDELEA UKURASA 23




Mshambuliaji wa Yanga, Bernard Morrison akifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Geita Gold itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Simba, Ihefu kibaruani FA

Na Adam Fungamwango

MASHINDANO ya Kombe la FA yanatarajiwa kuendelea tena leo kwa Wekundu wa Msimbazi kushuka kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam kuwakaribisha Ihefu SC kutoka Mbarali, Mbeya.

Mechi hiyo imeondolewa kwenye Uwanja wa Uhuru uliokuwa utumike awali kutokana na kuwa na matumizi mengine.

Itakuwa ni mechi ya tatu ya robo fainali ya mashindano hayo, baada ya Singida Big Stars na Azam FC kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo ambayo bingwa hupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Singida Big Stars iliitwanga Mbeya City mabao 4-1, na Azam FC ikaisulubu Mbeya City magoli 2-0, mechi iliyochezwa Azam Complex.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili jana mechi hiyo itakuwa ngumu kutokana na kikosi cha Ihefu kuundwa na wachezaji wengi wakongwe na wazoefu.

"Ihefu ni timu nzuri, ilichokuwa inakosa ni muunganiko, lakini sasa ina wachezaji wazuri wenye uwezo, ndiyo maana iliweza kuzifunga timu zote za Dar es Salaam zilizokwenda kule, Yanga, Azam na KMC, kwa maana hiyo sisi tutaingia kwa tahadhari, lakini pia tunataka tuwaonyeshe sisi ni wakubwa," alisema Ahmed.

Ihefu itaingia katika mchezo huo ikiwa imepunguzwa nguvu kutokana na wachezaji wao Wanigeria, Victor Akpan na Nelson Okwa, kutocheza kwa sababu ya makubaliano ya timu zote mbili wakati wanapeana nyota hao.

"Akpan na Okwa ni wachezaji wetu ambao wapo Ihefu kwa mkopo na katika makubaliano yetu hawatacheza kwenye mechi yoyote ambayo wao watacheza dhidi yetu," alisema Ahmed.

Alisema Simba iliamua

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >